**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |

| | |
|---|---|
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 23 Machi, 2015**

*(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari:** Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka Hati mezani Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2013/2014. Mheshimiwa, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 27**

**Kuwepo Shimo Kwenye Eneo la Darajani Mnadani**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba swali langu ambalo kuwa limepata kitanda kwa muda mrefu, swali Nam. 27 ni suala la muda mrefu sana katika chombo hiki cha wananchi, naomba hivi sasa nafikiri Serikali itakuwa imeshajipanga kwa suala hili ni la muda mrefu na ukizingatia Serikali hapa inakusanya pesa nyingi na imechukua muda mrefu kuwatumikia wananchi. Kwa swali hili naomba muhusika au dhamana wa swali hili nipo tayari kusikiliza jawabu na wananchi.

Kwa muda mrefu sasa eneo la Marikiti Mnadani kumekuwa na shimo kwenye sehemu ya njia ya kuelekea Masomo *Bookshop*.

a. Kuna hatua gani zimechukuliwa kufanya marekebisho eneo hilo.

b. Kwa nini matengenezo ya eneo hilo yamechukuwa muda mrefu, Je, wahusika hawalioni shimo hilo au wamepuuza.

**Mhe. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye kifungu (a) na (b) na kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Mji linakabiliwa na changamoto kubwa ya wizi wa mifuniko ya makaro na miundombinu mengine ya chuma, waya na alama mbali mbali unaofanywa na baadhi ya wahalifu kwa ajili ya kuuza kama chuma chakavu. Tatizo hili linaathiri sana maendeleo ya Mji wetu kwani fedha nyingi zinatumika kugharamia matengenezo au kurejeshea vifaa vinavyoibiwa. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako tukufu na

wananchi tushirikiane kuzuia wizi huu kwani wengi wanaofanya vitendo hivi ni wapiga kura wetu au tunaishi nao jirani. Tukishirikiana tutaweza kulipunguza au kuliondoa kabisa tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali kama kama ifuatavyo:-

a. Mhe. Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa ni kwamba wahusika walikuwa wakitafuta kwanza aina ya mifuniko ambayo ni madhubuti yenye kubeba uzito unaohitajika na mifuniko ambayo haitawavutia wezi wa mifuniko ya chuma na kwa sasa baada ya kupatikana mifuniko hiyo, tayari shimo hilo limeshafunikwa.

b. Mhe. Naibu Spika, shimo hilo halijapuuzwa na limeshafanyiwa kazi kama nilivyoeleza katika jibu (a).

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini ningeomba sana Mawaziri au Manaibu Waziri wanapojibu maswali kabla wa kujibu wakenda *physically* lile eneo kwanza wakaona ukweli na hali halisi. Mhe. Waziri, ulikuwa na mwendo huu mzuri sana nilikuuliza swali la Forodhani na ukalifanyia kazi asubuhi ukenda na ukakiri.

Mhe. Naibu Spika, ukweli hicho chuma kimewekwa labda siku tatu tu na kimoja kiko juu na kimoja kiko chini na bado eneo liko wazi na gari inayoingia pale kuelekea Masomo *Bookshop* unachangishwa shilingi mia tano. Bado kuna watembea kwa miguu usalama wao sio mzuri, chuma kimewekwa juzi swali lina karibu miaka miwili na pako wazi eneo lile. Ni lini utakwenda mwenyewe ukaone *physically* lile eneo bado pamoja na usalama wanaotembea kwa miguu hauridhishi na Katiba zetu zote mbili zinakataza ni haki ya kulinda usalama wa raia. Hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa *culvert* liloibiwa limechukua muda mrefu lini mtafanya ukaguzi wa maeneo mengine kama haya.

**Mhe. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nimeshakagua katika maeneo yote ambayo yana matatizo ya wizi wa mifuniko ya makaro ndani ya Mji wa Zanzibar. Huo ni wajibu wangu na mimi nauelewa wajibu wangu, kwa hiyo, tayari nimeshafanya kazi hiyo.

Mifuniko hii imewekwa siku ya tarehe 19 Machi, 2015 na sio siku tatu kutoka leo kama alivyosema Mhe. Mwakilishi. Lakini kwa kujali usalama wa raia na mali na afya zao, ndio maana Baraza la Mji kwa kushirikiana na wizara yangu tunafikiria utaratibu mwengine wa aina nyengine ya mifuniko ya makaro badala ya ile ya chuma. Kwa hiyo, kazi ya kuyapima mashimo ambayo yana makaro ya chuma inaendelea kufanyika ili tutengeneze mafuniko ya zege ili kwanza kujikinga na wezi ambao wanavutika sana na mifuniko ya chuma.

Pili, tuwe na uhakika wa mifuniko tutakayoiweka itadumu katika kipindi cha muda mrefu ili isije ikaleta athari kwa kuwaumiza wananchi ambao wanapita kwa miguu.

**UTARATIBU**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Waziri, swali la pili nafikiri labda hukulifahamu Kiswahili nilichokizungumza. Ni lini utakwenda kutembea ukaliona lile eneo lilozibwa ni moja na bado moja limeachwa, ni lini utakwenda na niko tayari kushirikiana na wewe kwenda ukaona ukweli na uhalisia ukoje pale, tukafanya ziara hiyo kama Jumapili au Jumatatu, lakini isijekuwa kama ziara ya Naibu Waziri wa Afya ikaota mbawa.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Waziri ni lini mtakwenda kupaona hapo pahala.

**Mhe. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, nadhani utaratibu sijui na mimi nipige utaratibu kwa sababu suala la mwanzo nilisema nimeshakagua maeneo yote ambayo yana matatizo ya mifuniko hiyo, la kama anataka Mhe. Mwakilishi, nifuatane mimi na yeye tukimaliza maswali twende mimi na yeye. (*Makofi*)

**Nam. 28**

**Malipo Makubwa kwa Cheti cha Mazao**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, swali linalofuata kwanza niishukuru Serikali hasa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini watendaji wake wote niwapongeze baada ya suala hili kuliona kwa uzito wake na wakalifuatilia na wakaona ukweli wake na kuanza kupunguza gharama za mazao. Baada ya maelezo hayo ya kuwashukuru watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, naomba Serikali itoe jawabu kwa faida tu ya wananchi waliokuwa hawajapata kusikia, lakini kwa kweli suala limeshafanyiwa kazi, niishukuru Serikali kwa kufuatilia. Naomba majibu.

Imebainika kuwa wananchi wengi wa vijijini wakati wa kusafirisha mazao yao kama vile ndimu, pilipili, mananasi na kadhalika hulazimika kukata cheti kuanzia shs. 3,000/- hata kama mazao hayo wamepewa zawadi au wanapeleka sokoni, lakini baada ya mauzo faida inayopatikana huwa haifikii gharama walizotumia.

a. Je, kuna sheria yoyote inayoelekeza utozwaji wa ada hii usiokuwa na uwiano.

b. Hatuoni kuwa tunawarudisha nyuma wakulima wanaojituma kwa shida kwa kuwatoza zaidi ya thamani ya wanachosafirisha.

c. Serikali inatoa kauli gani kwa wakulima wanyonge kutozwa zaidi ya thamani ya mazao yao, huku ukizingatia kilimo ndio ajira na Serikali haiwezi kuwaajiri.

**Mhe. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 27 lenye kifungu (a) na (b) na kabla ya kumjibu swali hilo naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa vyeti vya mazao umekuwepo siku nyingi ukiwa na lengo la kudhibiti wezi wanaoiba mali za watu na kuzisafirisha sehemu mbali mbali, kuzuia magendo na kuweka kumbukumbu na takwimu za mazao yanayozalishwa katika eneo husika. Mara baada ya kuanzishwa upya mfumo wa Serikali za Mitaa na kuchaguliwa masheha wakiwa watendaji katika ngazi za awali za mfumo wa Serikali, walipewa jukumu la kusimamia vyeti vya mazao na kiasi kinachotozwa kwa cheti kimoja ni shilingi elfu moja na mia tano.

Mhe. Naibu Spika, vyeti vya mazao vinatozwa kwa Sheria ya *Decree* ya Kanuni ya mazao ya mwaka 1937. Ambapo kuna vitabu maalum vya risiti vinavyotolewa na Wizara ya Fedha, vitabu hivi vya risiti hupewa masheha kwa lengo la kurahisisha huduma hii kwa wananchi. Kufuatia kutungwa kwa sheria mpya ya Serikali za Mitaa Nam. 8 ya mwaka 2014, masuala haya yatawekewa mfumo bora na wa kisasa zaidi ili kuleta uwiano wa thamani na kiasi kinachotozwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, maswali yake yenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a. Sheria hiyo inamtaka kila anayesafirisha mazao achangie ada ya shilingi 1000/=kwa msimu mdogo na shilingi 1500/- kwa msimu mkubwa na sio shilingi 3000/=kama alivyosema Mhe. Mwakilishi pamoja na kwamba hapo mwanzo ilikuwa ikitozwa shilingi 3000/=.

b. Bei ya shilingi elfu moja mia tano (1500/=) inayotozwa haiwarudishi nyuma wakulima, ada ya usafirishaji inahitajika ili angalau kurudisha gharama za uchapishaji na gharama nyengine zinazohitajika kwa maendeleo ya wananchi wenyewe katika maeneo ya wakulima. Gharama kubwa itakuwa kwa mkulima vikikosekana au kuondoshwa kwa vile wezi watapata fursa kubwa ya kuwaibia mazao yao na kuyasafirisha bila wezi hao kubainika.

c. Kama nilivyoeleza hapo awali bei ya cheti cha mazao kwa sasa ni elfu moja mia tano na iwapo kuna mtu anatoza zaidi ya bei hiyo basi namtaka aache mara moja suala hilo.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ulisema usharidhika mbona umesimama tena.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nitakuwa sijafanya haki kwanza kama sikuipongeza Serikali kwa hatua waliyoichukua ambayo imefanana na kilio cha wananchi wangu ambacho kimekuwa cha muda mrefu. Lazima hapo tuzungumzie ukweli niishukuru Serikali kwa hatua iliyochukua na kufanana na suala ambalo imekuwa kilio kwa wananchi wangu. Baada ya maelezo hayo nataka niulize swali moja tu la nyongeza.

Serikali haioni haja ya kuondosha hiyo shilingi 1500/- ili kufurahisha wananchi wake kutokana na kazi ngumu waliyoifanya hasa suala la kilimo hasa ukizingatia wananchi wa Jimbo la Muyuni kutokana na kilimo cha umwagiliaji wa ndimu.

**Mhe. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nipokee pongezi kwa niaba ya Serikali kutoka kwa Mhe. Mwakilishi.

Lakini la pili, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi na wananchi wa Muyuni kwa jumla na wananchi wengine wa Zanzibar kwamba ada na kodi mbali mbali zimewekwa kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya wananchi katika maeneo yao. Kwa hiyo, kuitaka Serikali iondoshe kabisa ada, nadhani haitakuwa sahihi. Suala lilikuwa ni bei kubwa na Serikali imezingatia kwa kuwajali wananchi wake na tumepunguza.

Hivi sasa hivi kuna Mradi wa *MIVAP* ambao unajenga barabara ziendazo kwa wakulima. Halmashauri ya Wilaya ya Kusini inatakiwa ichangie jumla ya milioni 50,000,000 katika mradi huo. Sasa iwapo kama tutaziondosha kabisa kutaipunguzia Halmashauri uwezo wa kuweza kuchangia kwa maslahi ya wananchi na wakulima wenyewe. Sasa namuomba Mhe. Mwakilishi, akubaliane na Serikali kwamba bado bei hii iliyopo iendelee kutumika. Ahsante sana.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana katika maelezo yake Mhe. Waziri alisema kuwa vyeti bado tutatumia *Decree* ya 1937, kama tutatumia *Decree* hiyo basi bei tunayolipa ya vyeti ni kubwa mno kwa kuwa *Decree* haijafanyiwa marekebisho, kwa sababu kwa *Decree* cheti itakuwa ni kasma ya shilingi moja bei yake kama tutatumia *Decree* hiyo. Je, haoni Mhe. Waziri kwamba kuna haja *Decree* hiyo kufanyiwa marekebisho.

**Mhe. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, kwanza Sheria ya *Decree* ya mwaka 1937 haikuweka viwango vya ada, ilikuwa imeweka utaratibu wa kutoa vyeti na taasisi inayohusika ilikuwa inaruhusiwa kuweza kutunga *by-laws* ili kuweka viwango vya ada. Kwa hiyo, hatuifati sheria ya mwaka 1973 kwa kuweka viwango vya ada, isipokuwa sheria iliweka utaratibu wa kuiwezesha Halmashauri au Manispaa kutunga sheria ndogo ndogo ili kuweka viwango vya ada.

Lakini la pili, kama nilivyosema katika jibu langu mama kwamba tayari tumeshatunga ya *Local Government* ya mwaka 2014. Kwa hiyo, utaratibu wote ule uliokuwa ukitumika kule na kwa sababu sheria hizi tayari nimeshazitangaza, maana yake ile Sheria ya *Decree* tena haitumiki sasa hivi, itatumika sheria hii na itategemea zile *by-laws* ambazo zitatungwa na Halmashauri na Manispaa au *Local Government* nyengine. Ahsante sana.

**Mhe. Salum Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa majibu niliyoyapata kwa namna bei ya vyeti inavyobadilika na kuwa wahusika ni Halmashauri.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kubadilisha kitu kunataka utafiti na utaalamu na kwa sababu tumeshuhudia kuwa hao wanaohusika na mikato siku hizi kila unapokwenda unakatwa pesa ambayo haihusiki au hailingani na ile thamani ya kitu chenyewe. Mimi swali langu ni kuwa, Mhe. Waziri, haoni kuwa iko haja ya kuwa na wataalamu maalum katika Serikali hii kwa kuangalia mazingira yalivyo na hali ya wakulima wetu walivyo ili kuweza kuweka bei za vyeti ambazo zinalipika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba Serikali kuu na hata wizara yangu inayo wataalamu wa kutosha kwa

kushirikiana na wataalamu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Fedha kujua thamani ya mazao ambayo yanatozwa vyeti.

Vile vile, ieleweke kwamba ada hizi zinapitishwa rasmi na Mabaraza ya Madiwani, hata kama wataalamu watakaa na wapendekeze hatimaye Mabaraza ya Madiwani yatakaa yaweze kuidhinisha. Kwa hiyo, ni jambo linalowahusu watu wengi, si jambo ambalo anaweza akakaa katibu au mkurugenzi akaamua tu kwamba leo ada itozwe hivi.

Lakini swali lake ni zuri ni imani yangu kwamba katika harakati hizi za mageuzi ya Serikali za Mitaa, suala lake la kuwa na taalamu wa kutosha katika Halmashauri na katika sehemu nyengine ambazo mambo haya yanafanyika Serikali inaendelea kulifanyia kazi na ni matumaini yetu kwamba Halmashauri zetu tutazijengea uwezo wa kuweza kuwapatia wataalamu ambao watakuwa na sifa za kuweza kuzifanya kazi hizi. Ahsante sana.

**Nam. 39**

**Mbadala wa Jengo la Kusubiria Kutazama Wagonjwa**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Ali Salum Haji)** - Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, naomba Serikali itoe majibu ya suala hili ikizingatia wakati tuliokuwanao na hali ilivyo hivi sasa. Swali hili ni mmoja ya miongoni linaloniathiri na kuninyima usingizi ni mimi, nimelichangia tokea mwaka uliopita na wizara sijui imejipangaje kuhusu suala hili. Nasubiri majibu kutoka serikalini.

Kwa kuwa suala la ujenzi wa banda la kupumzikia watu wanaosubiri muda wa kutazama wagonjwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja limekuwa tatizo kwa muda mrefu na kuonekana kutopata ufumbuzi wa haraka.

Je, wizara haioni haja ya kujenga japo mahema kwa dharura ili kunusuru tatizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia tukiwa tumeamka wenye afya njema na uzima.

Pili, naomba nitoe pole kwa familia ya Mwenyekiti wetu wa Mbweni eneo hili ambalo tupo ambaye amefariki dunia jana na *Inshaallah* atazikwa leo saa saba mchana Kiembesamaki.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 39 ambalo limeulizwa kwa niaba yake na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa banda la kupumzikia jamaa wa wagonjwa pamoja na wale wanaowauguza wagonjwa ambao huwa wanawasubiri wagonjwa wao, ni tatizo la muda mrefu sasa ambalo limeshachukuliwa hatua mbali mbali ili kufanikisha ujenzi wake. Kwa hivi sasa taratibu zote za ujenzi wa banda ikiwa pamoja na ruhusa ya ujenzi huo kutoka Mamlaka ya Mji Mkongwe zimekamilika. Wizara hivi sasa inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kutoka vyanzo mbali mbali ikiwemo Serikali Kuu pamoja na kutoa matangazo kwa wafanyabiashara mbali mbali ambao hivi karibuni tunatarajia kukamilisha ili kupata kile ambacho kinatarajiwa kufanyika pale, lakini baada ya kupata kibali cha Serikali Kuu.

Aidha, ushauri wa kujenga mahema ya dharura tumeupokea na tayari tumeshaufanyia kazi tokea suala hili lilipofika ila haukukubalika na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe kwani eneo lote linalozunguka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Wizara ya Afya, *Victoria Garden*, Ikulu, Mahakama, Makumbusho ya Taifa ni maeneo makuu katika uhifadhi maendeleo na kuenzi Mji Mkongwe wa Zanzibar na wazo la mahema katika eneo hilo ambalo ni urithi wa *UNESCO* kwa hivi sasa ulimwenguni inakwenda kinyume kabisa na uhifadhi wa urithi huo, kwa kizazi chetu na kizazi kijacho.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kutokuwa na afya na hayako makini, huo ndio ukweli ulivyo. Mimi ni mdau wa suala hili kwa muda mrefu na nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikumshukuru Waziri dhamana wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa uungwana wake

aliyoonesha katika chombo hiki, alionesha ramani na vibali kutoka Mji Mkongwe huu tayari ni mwaka, nimshukuru tena Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kwa kuwajali wananchi. Lakini suala hili mimi naona wizara haiko *serious* kama Waziri wa Afya alivyokuwa akisema; *"are you serious*"? Wizara haiko *serious* kwa hili wala halina ubishi mimi niko tayari kwa suala hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wanaoumia ni wananchi wa nchi hii na Serikali haiko tayari kujenga pale. Je, kama wizara iko tayari kukabidhi vitu hivi kwa mtu akashughulikie kujenga kama ilivyofanyika katika bandari ya Malindi kutokana na banda lililojengwa pale na ubora wake na imekuwa bora kuliko yote, wako tayari kukabidhi kwa mtu kwenda kujitolea kwa ajili ya wananchi baada ya wizara kushindwa ikiwemo jukumu hili, siku zote kuja humu tukipigwa muziki tu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kusema kwamba Serikali iko *very serious*, wizara zote ziko *very serious* katika kutimiza majukumu yake na hili linaendelea kutekelezwa.

La pili, Serikali bado haikushindwa, ndio maana nikaeleza katika jibu la msingi kwamba tunasubiri kibali cha juu cha Serikali. Aidha, hili jambo litafanywa na Serikali yenyewe au litatangazwa kupitia vyombo vya habari ili lifanyike na wafanyabiashara kama huo mfano aliyotoa wa Sheikh Said Salum Bakhresa pale bandarini.

Bahati nzuri kwa kuwa Mhe. Mwakilishi, huyu ninakaa naye karibu nje ya utaratibu huu wa kujibu maswali nilishawahi pia kumuonesha tangazo la kwamba hili ndio tangazo lililochorwa pamoja na zile ramani ambazo zitatolewa kwenye gazeti, lakini tunasubiri kibali rasmi cha kutoa matangazo hayo. Kwa sababu lile eneo lenyewe lina *sensitivity nature* na ni eneo la Mji Mkongwe. Kwa hiyo, tukishapata kibali tu kama Serikali haitoshughulikia yenyewe basi naamini hayo matangazo yatamfika Mhe. Jaku Hashim, Ndugu Said Salum Bakhresa na wafanyabiashara wengine mbali mbali. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Utaratibu**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Kifungu 37 "Waziri au mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi, kwa ufupi, isipokuwa kwamba swali aliloulizwa waziri mmoja linaweza kujibiwa na waziri mwengine".

Suala hili tayari kibali Mji Mkongwe wameshatoa sasa sijui kibali kipi wanachotaka wizarani kwake, kutoka Ikulu, wananchi wanazidi kuumia na mvua hizi pale, pale wanakwenda kwa shida, baada ya kwenda kutibiwa maradhi yanawazidi na maradhi mengine na hivi sasa baadhi ya dawa hazipo hospitali. Ni lini watatoa kibali kwa sababu mmeshashindwa kutumikia wananchi, toeni kibali tukatafute watu waje wajenge, lini mko tayari kukabidhi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naona unachanganya mambo, sisi tunazungumza jengo, wewe umeingia kwenye madawa. Sasa Naibu Waziri anasema kwamba kila kitu kishakaribia kuwa tayari kama kuna mtu ana uwezo wa kujenga ajitokeze wizarani ajenge. Sasa uwezo unao nenda wizarani na matangazo yanayotangazwa mwenye uwezo atajitokeza. Kwa hiyo, tustahamili tufuate utaratibu wa wizara.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya msingi na mazuri ambayo Mhe. Naibu Waziri, amekwishakujibu hapa, lakini mimi nilikuwa nina swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri pamoja na kwamba tayari wana mipango ya kuweza kutengeneza eneo ambalo wananchi watakwenda kuhifadhiwa katika maeneo yetu ya Mnazi Mmoja.

Je, hawaoni kwamba kwa kipindi hiki ambacho ni cha masika wale wananchi hususan kinamama ambao kwa wingi wanakwenda kulala pale nje wakafanyiwa eneo mbadala pale ambapo zamani tunachukulia vyeti au mpaka sasa hivi kule ndani ni eneo ambalo ni zuri na limehifadhika vizuri, wale kinamama ambao wanalala pale nje wakenda wakahifadhiwa pale mpaka hapo watakapokuwa wamejikamilisha wakaweza kuendelea na huduma zao vizuri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa swali zuri sana kwa sababu nitapata kutoa kidogo ufafanuzi zaidi. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na yeye kwamba hiki ni kipindi cha masika na wale wauguzi wa wagonjwa wengi wanaokuja pale wanapata tabu na mimi mwenyewe nimeshabahatika pia kutembelea eneo lile zaidi ya mara tatu na watu wengi ni wanaotoka Kaskazini, Kati na Kusini; ambapo huwa

wanachelewa kukaa na wagonjwa wao mpaka muda wa kutoka wakati mwengine hata usafiri kuukosa kwa hiyo wao hubakia pale.

Naomba pia niseme wazi kwamba katika tatizo moja kubwa kabisa tulilokuwanalo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni uhaba wa maeneo, yaani tunahitaji nafasi kubwa zaidi kuliko ile nafasi iliyokuwepo, ndio maana mnakuta kila pahala tumejenga jenga, hata ile sehemu iliyokuwa inaanikiwa nguo sasa hivi kuna jengo lile la *Neurosurgery***.** Kwa sababu tunajaribu kutumia kila nafasi iliyokuwepo na tunamshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hivi karibuni ameturuhusu tuendelee mbele kwenye jimbo la Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa maeneo ya Kizingo kule ambapo ule Mradi wa *ORIO* unaendelea.

Pia, naomba nikiri kwamba hivi sasa tayari eneo lile la pale mbele linatumika kwa watu kulala usiku hata Waheshimiwa Wawakilishi, mkipita pale mtakuta watu wamelala usiku na sio hapo tu, ile *over floor* inakuja mpaka Wizara ya Afya kwenye ile baraza ya nje zamani palipokuwa panachanganyiwa madawa pia watu siku hizi wanatandika, ukienda pale *times* za usiku baada ya sala ya *Insha* unakuwa watu wamelala. Hiyo ni kutokana na tatizo hilo hilo la nafasi na ufinyu wa nafasi iliyokuwepo.

Baada ya kupatikana ruhusa hiyo tu, maana kuna ruhusa moja bado haijapatikana ya kutengeneza vyoo maeneo yale kwa sababu wale watu wote wanaolala huwa wanahitaji kutumia huduma zile. Hivi sasa huwa wanarudi ndani asubuhi kwenda kutumia huduma zile ambapo inaleta kero zile mlizokuwa mnazizungumza juzi hata mitaro kujaa haraka. Kwa sababu sasa hivi imekuwa *double usage;* wale waliolazwa kule ndani na wale wanaotoka nje wanatumia *sewerage system* ile ile, mitaro ile ile.

Kwa hiyo, ndio maana tatizo moja wapo ni hilo katika kuchunguza kwamba mbona inajaa haraka! Tumegundua kwamba hata hawa wa huku wanatumia kule. Kwa hivyo, *Inshaallah* kabla ya bajeti naamini kibali hiki kitakuwa kimeshatoka na Mwenyezi Mungu akitujaalia masika haya haya au baada ya masika tu, basi mambo yatakuwa mazuri *Inshaallah* tumuombe Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, ahsane sana.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na nimshukuru Mhe. Jaku Hashim, kwa kuniulizia swali langu. Swali langu ni dogo tu, wakati Mhe. Naibu Waziri, akijibu swali langu kwa sababu mimi nilitaka yajengwe mabanda ya dharura baada ya kwamba kibali kinachelewa na ukizingatia mazingira ya wananchi wetu.

Sasa alijibu kwamba taratibu za *UNESCO* katika kuhifadhi Mji Mkongwe ndio zinazotupelekea kushindwa kujengwa mabanda haya ya dharura, lakini sijui kama hilo eneo analifahamu au halifahamu. Kwa sababu eneo husika ninalolizungumza mimi na ambalo limeombewa kibali na tayari ramani zimeshatayarishwa na Mhe Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alisema mambo yote yameshakamilika, eneo hilo lina mabanda ya kuuza madawa, kuuza machungwa, urojo.

Je, hawa waliojenga wao hawaharibu mandhari ya Mji Mkongwe? Mhe. Naibu Waziri, haoni hii ndio ile hadithi niliyoizungumza kwamba ndani ya Serikali mna mchwa wanatutafuna ili ionekane Serikali hii haitendi haki.

**Mhe. Naibu Waziri wa AFya:** Mhe. Naibu Spika, naomba kwa sababu kuna Mjumbe hapa alikuwa anafanya zogo sana kwa kupiga meza na makelele humu ndani ya Baraza sikuweza kusikia kipande chote cha mwisho cha Mhe. Mjumbe. Kwa hiyo, kwa idhini yako naomba arudie tafadhali.

**Mhe. Naibu Spika:** Labda nisaidie kama nitakosea atamalizia mwenyewe. Mheshimiwa, anasema kwa kuwa Mji Mkongwe unatakiwa usiharibiwe kimazingira yake na kila anayetaka kujenga mule apate kibali kutoka Mji Mkongwe. Je, wale waliojenga mabanda pale ya kuuzia machungwa, dawa, maji na vitu vyengine, wale hawakuvunja taratibu hizo, mbona wamejenga na hili banda la kukalia wataizamani wagonjwa lisiwezekane? Hilo ndio swali lake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba niseme kwamba ile ramani ambayo imekubaliwa na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na kutolewa kibali cha Mhe. Waziri wa Ardhi, eneo hilo jengine la hayo maduka pamoja na mabanda ya machungwa, maduka ya madawa, pamoja na hii ofisi ambayo inashughulika na masuala ya *UKIMWI* halimo katika eneo ambalo sisi tumekabidhiwa ramani. Nafikiria wao wako

nje ya eneo lile na kama kuna vibali wamepewa, basi ni nje ya eneo lile halihusiani na lile eneo la *garden* lenyewe ambalo lipo katika uhifadhi huo.

La pili, kweli naomba nikiri kwamba Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, imeshakamilisha mambo yake yote kwa pale tunachosubiri ni kibali kutoka Serikali Kuu cha kuitisha *interest* kama *PPP* au njia yoyote nyengine ya wafanyabiashara waweze kuwekeza hapa. Sasa naomba niseme kwamba maeneo hayo aliyouliza Mheshimiwa basi yako nje ya eneo hilo na kwa upande wa Mamlaka ya Mji Mkongwe tumeshakamilisha yote ila wametutaka wakati tunataka kujenga vyoo pale katika eneo hilo akishapatikana huyo mtu basi tujue ile mitaro itaungana na mitaro ipi ama zile karo zitakwenda vipi. Hilo tu ndilo lililobakia moja.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

**Nam. 40**

**Kauli Chafu Zinazotolewa na Baadhi ya Wauguzi**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** - Aliuliza:-

Kwa kuwa kauli ni moja ya mambo yanayoweza kumfariji au kumkatisha tamaa mgonjwa awapo katika mazingira yoyote hasa hospitali.

a. Je, Serikali inafahamu kuwepo kwa baadhi ya wauguzi wenye lugha za udhalilishaji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

b. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kauli chafu za aina hiyo zinazotolewa na baadhi ya wauguzi katika hospitali zetu za Unguja na Pemba zinakomeshwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri na kuwa ni kweli kauli njema ni tabibu, wengine kusema kauli njema ni nusu ya matibabu. Wizara ya Afya inafahamu kuwepo kwa baadhi ya wauguzi wenye lugha zisizopendeza, wajeuri na wajuba kwa wanaofika kupata huduma hizo katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Hata juzi katika michango ya Kamati jambo hili lilielezwa kwa upana wake wote na kutolewa ufafanuzi pia na Mhe. Waziri. Hata hivyo, wizara imekuwa ikichukuwa hatua mbali mbali kukabiliana na hali hiyo pale inapotokea ikiwemo kuwaita na kuwaonya na hata baadhi ya wakati kutoa barua za maonyo au uhamisho katika utendaji wa suala hilo. Pia, wizara huhimiza sana kufuata maadili ya uuguzi (*nursing ethics*) ambayo yanasomeshwa katika Chuo cha Afya Mbweni na manesi wengi napenda kusema wanaomaliza pale au wanaofalu pale somo hili wanakuwa wamelifaulu. Lakini wanapofika sehemu zao za kazi hususan Hospitali ya Mnazi Mmoja hali wakati mwengine hubadilika, lakini bado hali hiyo inaendelea kusimamiwa na kuchukuliwa hatu mbali mbali.

(b)Ili kuhakikisha kuwa hali hiyo inakomeshwa hatua za kinidhamu za kuwaadabisha zinachukuliwa dhidi ya muhiska kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi Serikali. Hivyo, wizara inawaomba wananchi kutoa taarifa katika Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mnazi Mmoja pale watakapombaini mfanyakazi yeyote anatumia aidha lugha chafu au isiyofaa ili hatua za kinidhamu dhidi yake ziweze kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

**Mhe. Jaku Suleiman Ayoub:**

(a)Mhe. Naibu Spika, tatizo la lugha chafu zinazotolewa na wauguzi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja bado zinaendelea na kadhia hiyo hata mke wa Naibu Waziri wa Afya imemkuta kadhia hiyo na sijui wafanyakazi wangapi

mpaka sasa hivi mmeshawachukuliwa nidhamu, ikiwa kadhia kama hiyo imeshamkuta mke wa Naibu Waziri wa Afya.

(b)Askari wenu wa milangoni wamekuwa na lugha ambazo hazifahamiki hawamjui kiongozi nani, Mheshimiwa nani na Mkugenzi nani. Wajue pale pahali hapatolewi sadaka wala pesa, wanakwenda pale kwa shida. Lini kama Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi mtakaa kuwapa darasa lini mtafanya hatua hiyo kwa sababu maneno mazuri ni sadaka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kwanza naomba nikubaliane nae pia kwamba suala hili limejitokeza kwa wale walinzi wa mlangoni na tayari wameshaitwa mara moja wakuu wao wa ulinzi pale mlangoni kuambiwa kuwa pale ni Hospitali, si pahala ambapo wale wanaowaunguza wagonjwa wao wanakuja kuomba au kuja kutafuta jambo jengine lolote ila kuwatumikia na kuwahudumia wagongonjwa wao.

Kwa hiyo, tokea tumefanya kikao nao naweza kusema lugha ile kidogo imerekebishika wanakwenda vizuri. Lakini jitihada endelevu ambayo tutaendelea nao na wakati nazungumza hapa naamini wa wao kule watakuwa wananisikia hasa wale wakubwa wao ma-*supervisors,* nawaomba sana maana bado Wawakilishi wanaendelea kulalamika wajirekebishe laa, wasipofanya hivyo, yaani wasipojirekebisha basi tutamuamrisha na kumpa agizo Katibu Mkuu afute mkataba wao na kuwaajiri watu wengine ambao wataweza kuwatumikia wananchi vizuri hususan wale wanaoingia ndani.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa wauguzi mpaka sasa zimeshatolewa barua tano za onyo kwa wauguzi mbali mbali ambao wamegundulika kufanya makosa hayo na baada ya kugundulika kufanya makosa hayo, ushahidi ulikuwepo na uliwasilishwa kwa sababu mtu wakati mwengine unaweza kuwa na chuki zako tu binafsi au mke mwezako anafanyakazi pale ukataka wewe kumshitaki tu bila sababu. Ushahidi lazima upatikane, uasilishwe na pande zote mbili ziwepo za yule mtuhumiwa na yule ambaye anatoa ushahidi kusema kwamba huyu kanifanyia hivi hivi.

Mpaka sasa hivi uhamisho wa aina tatu umeshatokezea kutoa pale kwa wauguzi kutolewa pale kupelekwa eneo jengine. Naomba kuendelea kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

## HOJA ZA KAMATI

*(Majadiliano wanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba nitoe taarifa kwamba tuna nia ya kumaliza kiporo chetu tulichokianza Ijumaa na kumaliza kwake lazima *quorum* ndani ya Baraza. Sasa naona baadhi ya Waheshimiwa wanaanza kutoka, ningeomba wanaotaka kutoka aniage mimi ende na arudi ili tuweze kumaliza kazi hii na tuingie kazi nyingine na hivi sasa nimebaki na wachangiaji sita, tukimaliza hawa sita tutaanza kuwaita Mawaziri, Mwenyekiti akamalishe tutoe hoja tuingie kwenye sehemu nyengine.

Kwa hivyo, naomba sana tujali muda tutoke kwa utaratibu ili kazi yetu tuweze kuimaliza vizuri. Mchangiaji atakaenza sasa hivi ni Mhe. Mussa Ali Hassan, baadae Mhe. Abdallah Juma na Mhe. Panya Ali Abdallah ajiandae.

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsnate Mhe. Naibu Spika, kuweza kunipa nafasi hii ya kuchangia nikiwa mtu wa kwanza leo katika uchangiaji huu.

Sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuhakikishia kwamba tuko wazima katika Baraza hili na tumefika salama. Sina budi kwanza nichangie Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu hali ardhi ambayo tunaenda nayo. Ni kweli hali ya mazingira ni mbaya sana ya miundombinu ambayo imeharibika katika maeneo yetu ya ardhi ambayo hivi sasa kuna matatizo mengi katika sehemu nyingi za ardhi hasa katika sehemu za uchumbaji michanga.

Kwa kweli hivi sasa uchimbaji mchanga unakwenda ovyo na kwamba sehemu nyingi za wananchi zimeharibika hasa ukiangalia wakati huu mgumu wa masika ambao unaendelea. Hivyo, iko haja wenzetu ambao wanahusika na mazingira kuhakikisha kwamba hali hii inadhibitiwa na kuhakikisha kwamba uchimbaji ovyo unadhibitiwa kabisa ili kuhakikisha usalama wa nyumba pamoja na watoto wetu ambao wanaishi katika maeneo ambayo ni hatarishi hukusu kuzama katika sehemu hii.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu matatizo ya ukati miti hasa ya mikoko. Hivi sasa kuna matatizo mengi sana katika maeneo ya bahari. Ni kweli kwamba ukataji miti umezidi sehemu nyingi za ukataji miti hapa Zanzibar hivi sasa ni maeneo mengi ambayo yanatumika kwenye bahari, utakuta kwamba hivi sasa bahari inakuja juu kwa nguvu sana kwa vile sehemu nyingi za ukataji miti bado hazijaweza kudhibitiwa na hiyo inahatarisha usalama wa hali ya bahari kuja juu kwa nguvu sana na kuhatarisha mafuriko ambayo hivi sasa yanahatarisha sana.

Katika miji yetu ya Kusini hivi sasa eneo la Jambiani utakuja sehemu kubwa sana bahari iko katika majumba. Hii imesababishwa kwamba maeneo yale yote yalikuwa na mikoko mingi sana, lakini utaona mikoko hiyo imeshindwa kabisa kuhakikisha kudhibitiwa na wahusika na utakuta sasa bahari imeshafika katika ardhi na makaburi mengi ambayo yalikuwa katika maeneo yale sasa wameshachukuliwa na maji.

Sasa kwa kweli wahusika na hali ya ardhi wanatakiwa kuhakikisha kwamba mazingira yote yanahakikishwa kwamba wamo katika hali salama ili kuhakikisha usalama wa ardhi unapatikana na sio kuwa tunaishi kiholela na kuhatarisha maisha ya wananchi. Hivyo, naomba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ihakikishe mazingira yanahakikishwa kwamba ukataji miti ndio unaosababisha kuleta bahari juu na kuhatarisha makaburi na nyumba za ufukweni zinaendelea akuharibika.

Mhe. Naibu Spika, naendelea katika sehemu ya Madawa ya Kulevya, hivi sasa kwa kweli hali ya madawa ya kulevya yamezidi kuimarika na kusema kwamba Serikali labda itakuwa inashidwa kudhibiti madawa hayo. Sasa naomba ofisi inayohusika ziadi ituhakikishie kwamba udhibiti wa madawa ya kulevya unahakikishwa kwamba uko katika hali nzuri na watu wote wako salama, ili kuhakikisha watu wanaovuta madawa hayo kudhibitiwa katika sehemu ambazo zimewekwa kwa ajili ya kuhakikisha wagonjwa ambao wameshaathirika kwamba wanakaa salama katika maeneo hayo. Hayo yote ni kwamba ofisi inayohusika haijachukuwa hatua zinazotakiwa ama zinazohakikishwa kwamba usalama unapatikana.

Mhe. Naibu Spika, hayo yote yanathibitishwa kwamba ofisi inayohusika hivi sasa ni bado haijaweza kuhakikisha kwamba usalama unatapikana katika sehemu zote ambazo madawa ya kulevya wanadhibitiwa hasa katika sehemu ya Uwanja wa Ndege na sehemu za Bandari. Utakuta kwamba sehemu hizo tumeweka vifaa vingi vya kuweza kuhakikisha usalama, lakini bado utakuta usalama bado hajapatikana.

Mhe. Naibu Spika, sehemu nyengine ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ofisi hii hivi sasa mashukuru sana ofisi kwa miundombinu wa bahari imehakikishwa kwamba imefanikiwa vizuri pamoja na Anga, hasa kwa vile sehemu ya Anga hivi sasa tumepa vyombo vingi sana vinakuja katika nchi yetu tena kwa wakati na utulivu.Tunahakikisha tunajenga sehemu ya Bandari ya Mpigaduri hiyo itahakikisha kwamba uhakika wa usafiri unapatikana na uhakika wa kwamba vitu vyote ambavyo vinahitaji kupokewa vinapokewa kwa wakati na uhakika.

Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Uzalishaji hivi sasa sekta hii tumepata miundombinu mizuri ya kuweza kumwamgilia. Sekta hii sasa imehakikisha kwamba vitu vingi ambavyo vilikuwa tunaagiza kutoka nje hivi sasa ni mwiko kuagiza hasa tukiangalia katika masuala mengi ambayo yameimarika sasa hapa Zanzibar, mambo ya *tomatoes* na tukasema malaji mazuri yameendelea kama matikiti.

Hivi sasa tunahakikisha kwamba viti hivi hatuagizi kutoka nje, kwa kweli hayo yote yanatokana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuhakikisha miundombinu mingi inakuwa mizuri na inaimarika zaidi. Zaidi ya hapo nampongeza sana Mheshimiwa mwezangu hivi juzi alipomaliza kuchangia alichangia katika Ofisi ya Makamu wa

Pili wa Rais kwamba hivi sasa kwa kweli Serikali imezorota sana, akafika kusema kwamba kuhakikisha kuwa yeye mwenyewe muhisika mkubwa anaweza akajiuzulu.

Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba huyu mwezangu amesema vizuri sana.

Lakini sio kusema Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ijiuzulu, ni afadhali ingelikuwa kusema kwamba Serikali iliyokuwepo hivi sasa haifanyi vizuri, inafaa ijiuzulu yenyewe kwa sababu ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa na ndio inayoendesha Serikali ya Makamu wa Pili wa Rais.

Hivyo, iko haja ya kusema kwamba yeye mwenyewe ilikuwa anahakikisha kwamba ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa haiwajibiki na sio Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais na namsifu kwamba aliweza kusifu sana katika Serikali ya Kwanza iliyopita ilikuwa na Waziri Viongozi, akawasifu kwa majina kwamba Ofisi za Waziri wa Pili wa Rais ni Ofisi za Mawaziri Viongozi waliopita walikuwa wanawajibika sana.

Hivyo, iko haja ya kusema kwamba ni bora irejeshwe Serikali ile ile inayondeshwa na Waziri Kiongozi na sio Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo inaongozwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hivyo, nahakikisha kwamba, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iweze kujadiliwa na kuweza kuhakikisha kwamba kama kweli haiwajibiki na mawaziri hawawajiki basi ni bora kuhakikisha kwamba ofisi yetu ya Makamu wa Pili ambayo inaongoza Serikali ya Umoja wa Kitaifa ijiuzuli wenyewe sio Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, Hali ya utulivu tunashukuru kwamba hali hii inaimarika na hivi sasa katika hali ya nchi yetu tuko katika hali ya utulivu na kwa muda mrefu sana hatujahakikisha matokeo ambayo yalikuwa yanatokea hapo mwanzo. Hivi sasa tuko katika hali ya utulivu na kwamba hivi sasa tunazidisha hali ya utulivu, lakini kuna baadhi ya wananchi ambao hawaelewi nini maana ya utulivu na nini faida ya ulivu, ndio wanazidi kuharakisha kwamba kutatizo ili nchi yetu iingie kwenye hali ya machufuko na hii sio kwamba hali nzuri ambayo itaisaidia nchi yetu.

Tunaishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuhakikisha kwamba tunaenda vizuri katika hali ya utulivu wa nchi hii na ndio suala ambalo tunaliomba hasa katika uchaguzi wetu wa mwaka 2015 tuhakikishe kwamba hali ya utulivu inaimarika na inafaidisha katika nchi yetu.

Tukikumbuka nchi za wenzetu ilikuwa kama yetu chokochoko nyingi sana zilikuwa zinaendelezwa, lakini mpaka sasa zimesambaratika kutokana kwamba umetoweka utulivu katika nchi zao. Hivyo, tunaomba kwamba nchi yetu iendelee kuhakikisha kwamba ina hakika utaluvu wa nchi yetu unaimarika na unadhibitiwa kwa faida ya Taifa letu na Taifa la vijana wetu wa kesho ambao wanatarajia kuongeza nchi yetu kwa usalama zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa leo sitakuwa na mchango mkubwa sana isipokuwa nataka kuchangia tu kuhakikisha kwamba hali ya Makamu wa Kwanza wa Rais uendelee vipi na hali Ofisi ya Makamu wa Pili iendelee vipi. Ahsante kwa hayo.

**Mhe. Abdallah Juma Abdalhah:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu anaendelea kutupa neema yake ya uzima na uhai ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kama kawaida.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze na Ofisi ya Rais na katika Ofisi ya Rais kuna jambo kubwa sana. Ujengaji wa Ofisi ya Rais Pemba ni muda mrefu sana Ofisi yake ni mbovu na linavuja ni jengo la zamani sana halikaliki sana, keshasema sana mpaka kanyamaza. Sasa naomba Ofisi ya Rais iandae utaratibu wa kujenga Ofisi kule Pemba angalau na wale wafanyakazi walioko kule Pemba basi waweze kufanyakazi katika pahali pazuri.

Nikiondoka hilo Mhe. Naibu Spika, nije katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na katika Ofisi hii jambo ambalo linanigusa sana ni jambo la uchafuzi wa mazingira. Mpaka leo pamoja na makelele ambayo Kamati zetu zimekuwa zikisema sana na sisi Wajumbe wa Baraza hapa tukipiga makelele sana. Lakini uchafuzi wa mazingira bado unaendelea na changamoto kubwa sana katika Ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka hivi karibuni tulipitisha Sheria ya Mazingira. Ndani ya sheria ile imetajwa kuwa patatengenezwa Mamlaka ya Kusimamia Mazingira. Sasa labda niombe hasa basi utaratibu huo uharakishwe ili hii mamlaka iweze kuundwa na kukabidhiwa majukumu yake ili iweze kudhibiti hali. Kwa sababu mimi nasikitika sana Mhe. Naibu Spika, kwa mfano taasisi kama *ZIPA* ambao inajua athari ya mazingira, lakini sijui kwa sababu zipi inakiuka Sheria ya Mazingira na inatoa vibali kwa *investors* bila ya kuangalia tathmini ambayo *investment* hiyo inaweza ikasababisha katika masuala ya mazingira.

Sasa kwanza naomba sana hawa wakubwa wa *ZIPA*, huu mtindo wauache mara moja. Nchi hii ni yetu, ni kijinchi kidogo sana, athari yake ni kubwa kwa wananchi na Wazanzibari hatuna pa kwenda. Kwa hivyo, suala la mazingira lipewe kipaumbele, tusimuachie mtu hata dakika moja kutuchafulia mazingira.

Jambo jengine ambalo ni sugu katika Idara ya Mazingira Mhe. Naibu Spika, ni unyonge wa wananchi, wananchi ni maskini. Tulipokuwa wadogo tukisoma skuli kule kuna kitabu kimoja kinamueleza bata aliyekuwa akitaga yai moja la dhahabu. Sasa yule aliyekuwa anamiliki bata akasema aah! mimi mpaka lini kila siku anataga yai moja. Bora nimchinje huyu bata ili nipate ile dhahabu iliyokuwepo tumboni kwa pamoja niweze kufanyia shughuli zangu. Kumbe alipomchinja hakukuta yai hata moja.

Mhe. Naibu Spika, sasa wananchi wana dhiki ya maisha, wamegeuka yule mmiliki wa bata, tunakula raslimali zetu tena bila ya kuwa na utaratibu mzuri. Maana yake tukiwa na utaratibu mzuri, wapo wenzetu wanatumia raslimali hizi ambazo hazirejesheki. Lakini wana utaratibu ikiwa wanakata miti basi kuna utaratibu wa *replacement*, unakata mti, unapanda mti. Na kunakuwa na utaratibu maalum, wanapanda halafu wanavuna, wakimaliza kuvuna kuna shamba jengine linaendelea kukua.

Sasa utaratibu wa misitu unakuwa bado unabakia na wao wanavuna na hakuna athari ya kimazingira inayotokea kwa sababu ya ukatwaji wa misitu. Lakini kwetu sisi usimamizi huo na uratibu huo bado ni mdogo sana. Kwa hivyo, mwananchi anachukua tu lile msumeno wake anakwenda anakata hajali kama nikishaukata huu athari yake itakuwa kubwa na kuna miaka pengine hamsini ili mti kama huu tuweze kuupata tena, hivyo, tunamaliza misitu, tunakimbiza mvua, tunachafua hali ya hewa.

Mhe. Naibu Spika, wengine ni ajira zao wanakata matofali yale. Nafikiri Ofisi ya Makamu ya Kwanza wa Rais imefanya mazungumzo mara nyingi na wale wanaokata matofali, ili angalau kuwe na *replacement* kuwe na utaratibu maalum uliokuwa hauharibu yale mazingira, lakini bado hali haiendi vizuri sana. Kwa hivyo, nasisitiza kwamba hii Mamlaka ya Mazingira sasa iundwe na iweke mikakati itakayowafanya wananchi waweze kutumia raslimali zisizohamashika au kurejesheka lakini bia ya kupata athari katika mazingira yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa naomba niende Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuna Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali. Hii ni Idara kubwa sana kwa sababu kazi yake ni kuratibu Serikali nzima. Nimevutiwa sana na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati. Ukisoma ukurasa wa 10, Kamati imeshauri mambo matatu kwa Idara hii. Mimi naomba nilisome hil moja tu.

Mhe. Naibu Spika, hivyo, naomba ninukuu ili nipate kujenga hoja. Kamati inashauri; "Serikali ihakikishe utekelezaji wa Taarifa za Kamati za Kudumu na Kamati Teule za Baraza la Wawakilishi zinazofanyiwa kazi ili kupunguza kero katika jamii na kupelekea wananchi kuwa na imani na Serikali yao. Kwani maelezo yanayotolewa Barazani, mengi huwa yanatoka kwa wananchi na utekelezwaji wa maagizo hayo ni kuwatumia wao wananchi.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kuna ubadhirifu mwingi uliogundulika na Kamati zilizoundwa na Baraza la Wawakilishi, lakini hatuoni hatua za haraka kuchukuliwa. Hii ipelekea wale wakosaji kujiona wapo sawa na wengine kuweza kufanya kama hivyo, kwani watahisi kufanya ubadhirifu ni jambo la kawaida tu. Hivyo, hata malengo ya Serikali itakuwa ni ndoto tu ikiwa tutaendelea kuoneana muhali, huku wachache wakitafuna. Kamati inaamini ikiwa Serikali itakuwa makini basi bado kuna uwezekano mkubwa wa kujitegemea kwa bajeti ya matumizi ya kawaida kupitia mapato yetu ya ndani bila ya kutegemea wafadhili kutoka nje ya nchi".

Mhe. Naibu Spika, nimejaribu kupasoma hapa ili kujenga hoja na hoja ambayo ninakusudia kuijenga watendaji wanatafuna pesa za wananchi ovyo. Mimi nasikitika sana kwa sababu pale Rwanda, yule Mzee Kagame ukitafuna pesa za wananchi, anakupigia simu mwenyewe, bwana mkubwa umeiba, mimi ninakuja huko niachieni ufunguo wangu nikija nisikukute huko na nikikukuta nakupiga risasi. Hii ndiyo lugha ya Mzee Kagame.

Mhe. Naibu Spika, na tuangalieni kinchi kile kinatoka ndani ya matatizo makubwa hivi karibuni na leo uchumi wao upo mbali kuliko sisi. Sasa Mzee Kagame yupo *serious*. Hivi kwa nini bwana mkubwa naye hawi *serious*; mashaka tunampelekea kila siku, bwana huyu katafuna pesa, anashindwa kumchukulia mtu hatua mpaka leo.

Mhe. Naibu Spika, hili linanisikitisha sana mimi na ikiwa Mhe. Rais, ataendelea kuwa na muhali wa aina hii, wala tusitegemee kama nchi hii itafikia hatua ya maendeleo. Maana yake maendeleo ni hizi pesa zinazotafunwa. Ni Kamati ngapi Teule zimeundwa zikaleta ripoti zake hapa, kuna watu unawaona hivi hivi hawa siyo watu hata wa kubakia, alivyoyaona Tundu Lissu hata kwa dakika moja hafai kukaa ofisini. Leo, tunaendelea kuwaonea muhali mpaka lini.

Sasa mimi sielekezi lawama zangu kwa Makamu wa Pili wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais kaajiriwa, lakini tatizo huyu aliyemuajiri Makamu wa Pili wa Rais, ndiye yeye anaona muhali kuwachukulia watu hatua. Na hili na hii ndiyo moja kubwa sana ambayo Rais anaifanya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninamshauri sana rafiki yangu. Dkt. Ali Mohamed Shein ni rafiki yangu mimi. Namuomba sana aondoe muhali ili wananchi wajenge matumaini na Serikali yao. Wananchi wanapoteza matumaini.*(Makofi)*

Kuna tatizo la wafanyakazi hewa tunapigana nalo huu mwaka wa ngapi na kila siku, ukifanywa ukaguzi wafanyakazi hewa bado wapo wanaonekana na hawachukuliwi hatua. Hivi Rais ataogopa watu mpaka lini. Lazima tubadilike.

Kama kuwa na *trend* hata kama anayofanya Dkt. Mrisho Kikwete pale. Dkt. Kikwete huu mwaka wa uchaguzi, hata juzi kafukuza watu. Kwa nini na Dkt. Shein hafanyi.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa nafasi tunampa Mhe. Farida Amour Mohammed, baadae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na tunamalizia Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Mhe. Naibu Spika, ahsante nakushukuru.

Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia akatupa hazina yake ya uhai na uzima tukafika hapa leo katika Baraza hili. Pili, naomba niwapongeze kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuzisimamia Wizara hizi. Wizara ambazo zote tatu ndiyo roho ya nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, nataka nianze kwa kutoa mchango wangu katika Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Ripoti ya Kamati imeonesha uingizwaji, usafirishaji na utumiaji wa madawa ya kulevya bado unaendelea.

Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo na janga la kitaifa. Nasema hivyo kwa sababu hapa pamezungumzwa uingizwaji, usafirishaji na utumiaji. Sasa wanaoingiza na wanaosafirisha wanafanya hivyo kwa maslahi yao wenyewe, pengine utajiri hawajui mbele kuna nini. Lakini mimi nalizungumzia hapa zaidi linaloniuma na bila shaka kila mmoja wetu linamuuma hilo ni hawa watumiaji. Kwa sababu wanaotumia ni vijana wetu, ni nguvu kazi ya nchi hii, ni nguvu kazi za Taifa hili.

Sasa sijui mpaka lini hali hii itaendelea ya kufichwa au kuhifadhiwa hawa wanaosafirisha na wanaoleta hapa nchini haya madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, tatizo hili ni la muda mrefu. Wizara husika inafanya kila mbinu kuweka vyombo vya usalama, uwanja wa ndege na bandari, lakini pia kuna bandari bubu, lakini sasa sijui vitu hivi vinapita wapi kila siku mpaka vikafika wakati vikaja kwa mtumiaji na kuwaathiri vijana wetu ambao kuwa wote sasa hivi wameshakuwa na akili pungufu, juu ya kazi kubwa waliyonayo Wizara husika ya kutafuta pamoja na watu binafsi maeneo ya kuhifadhi walioathirika. Tutaendelea kuhifadhi wanaoathirika na madawa hawa mpaka lini wakati bado Serikali inalifumbia macho hili suala la waingizaji na wasafirishaji wa madawa haya.

Mhe. Naibu Spika, nije katika udhalilishaji. Ripoti ya Kamati imesema kuwa udhalilishaji mkubwa na hasa kwa walemavu.

Mhe. Naibu Spika, bado Serikali haijawa maskini katika kulisimamia hili. Ninasema hili kwa sababu. Hapa tatizo kubwa lililoopo inaonekana *DNA machine* tu. Jamani *DNA machine* kweli inachunguza baadhi ya mambo, lakini kuna ushahidi mwengine mtoto mlemavu, hana akili anaekewa watu zaidi thalathini, anaambiwa mseme, anasema ni huyu hapa lakini *still* panaambiwa patafutwe *DNA machine. DNA machine* ina maana gani jamani!

Kiukweli Serikali naiomba sana iwe makini katika hili, tunawadhalilisha watoto wetu na leo wangu, kesho wa mwenzangu. Hili ninaliomba sana Serikali ilisimamie kwa nguvu zote, kwa sababu watu wapo wenye akili, wenzetu wengine wamesema hapa walipochangia kuwa kuna watu wazima, wanene, wana kilo zaidi ya mia tatu wenye akili timamu. Kwa nini wakawatafute watoto wadogo wa kike na wa kiume ambao ni walemavu wawafanyie mambo kama haya na bado Serikali imekaa kimya.

Mhe. Naibu Spika, hili linauma na hili ni janga na naiomba Serikali ilichukulie kama kuwa ni janga hili na lichukuliwe hatua zinavyowezekana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nije katika Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini kabla sijaingia katika ofisi hii, naomba nipate ufafanuzi kutoka Waziri husika. Taarifa ya Kamati ya Ripoti hii ina kurasa kumi na moja. Maelezo ambayo hayahusiani na maagizo ya Kamati. Kuna majibu yanayohusu uzalishaji, mapato, matumizi na upatikanaji wa huduma mbali mbali.

Imani yangu ni kwamba maelezo haya yangekuwepo kwenye bajeti. Sasa sijui watendaji hawa wa Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, maelezo haya wameyatoa wapi na wakayaleta hapa na nina wasi wasi mkubwa hata huyo Makamu wa Pili wa Rais mwenyewe hawezi kulijua hili. Kwa sababu Makamu wa Pili wa Rais ana watendaji wake, wao ndiyo wakaangalia jambo lipi linafaa, halafu wampelee yale majibu yawe vipi. Sasa hili kwanza naomba nipate ufafanuzi wameyatoa wapi majibu haya, kurasa kumi na moja ambazo kuwa yameendana na mambo mengine tofauti na maagizo ya Kamati.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye agizo nambari ishirini na saba, "Matengenezo ya Baraza la Wawakilishi Pemba". Hichi ni kilio chetu cha muda mrefu, tokea siku wengine hatujaingia kwenye Baraza la Wawakilishi waliokuwepo nyuma na mpaka sasa. Tokea nimeingia kwenye Baraza la Wawakilishi, Baraza lile la Pemba ninachokiona matumizi yake ni ile siku ya mwanzo ya kuthibitisha ratiba, ndiyo tunaingia pale kama linaonekana jengo, lakini lile jengo bado Serikali haijaamua kulifanyia matengenezo likaonekana na hadhi ya Baraza la Wawakilishi.

Naiomba Serikali sana kwa unyenyekevu mkubwa ile Ofisi ya Pemba nayo, wale watu wa Pemba nao wanataka maendeleo na miongoni mwa maendeleo ya kile kisiwa cha Pemba angalau lile jengo kuonekana kama jengo la maana. Sasa haiwezekani kama vikao vyote miaka mitano, hakuna hata kikao kimoja, hata cha wiki mbili kilichokuwa kimefanyika pale Pemba kwa sababu ya mapungufu yaliopo katika Baraza lile.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Naibu Spika, Wizara inayohusika ilishughulikie hili kwa nia safi, kama kuna mtu Mwenyezi Mungu atamjaalia arudi tena na hata tusirudi tena, hawa watakaokuja angalau lile jengo lionekana linafanyiwa kazi kama ipasavyo.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka katika upungufu wa vifaa kwenye Kamati ya Maafa. Katika Idara ya Maafa ripoti ya Kamati imesema kuna upungufu wa vifaa na ucheleweshaji wa kupata taarifa za maafa.

Mhe. Naibu Spika, pia hili ni tatizo kwa sababu maafa yanatokezea wakati wowote na pahali popote. Kwa hivyo, wakati kuna Kamati hii Maalum ya Maafa, inatakiwa ijipange madhubuti kwa kujiandaa wakati wowote litakalotokea maafa ya aina yoyote lipate kusimamiwa kwa haraka. Si vizuri itokezee maafa iwe hata kutoka zile taarifa zake zinachukua muda mrefu, mpaka taarifa zikipatikana walio wengi tayari wameshapata athari kubwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba Wizara inayohusika ilisimamia hili kwa sababu maafa yanatokezea kila wakati, pahali popote na haya ni mambo ya Mwenyezi Mungu hatuwezi kuyazuia. Kwa hivyo, angalau tujipange katika kulisaidia hili.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Tume ya Uchaguzi. Ripoti ya Kamati imesema Tume za Uchaguzi zote ndivyo ilivyo zimo katika majengo ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya. Hili ni kweli na ingelikuwa Ofisi za Wakuu wa Wilaya zimejifanya ni marafiki wa wananchi wote, basi isingekuwa tatizo. Lakini Ofisi za Wakuu wa Wilaya zinatumika kisiasa zaidi kuliko jamii. Kwa hivyo, Tume za Uchaguzi kuwemo ndani ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya ni tatizo ambalo halitusaidii wananchi wote na linawanyima wananchi haki zao.(*Makofi*)

Hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri anayehusika na hili Serikali ilione hili na itafute maeneo mahususi ambayo kuwa wananchi wote watapata kwenda pale kutafuta haki zao, zisiwe Tume za Uchaguzi katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, nije katika agizo namba saba na namba nane. Majibu haya hayakuniridhisha hata kidogo. Naomba niulize swali. Katika hii Kamati ya Sherehe na Mapambo katika Sherehe za Mapinduzi, hivi Kamati hii vitendeakazi vilivyokusudiwa na Kamati hapa ni kununua shamiana tu. Ufahamu wangu mdogo nilionao na naamini kuwa katika Sherehe za Mapinduzi kuna vifaa vingi sana vinavyotakiwa, mbali ya vifaa hivyo, kunatakiwa fedha nyingi, vifaa viwe vya kisasa na muhimu kwa sababu Sherehe za Mapinduzi ni Sherehe za Kitaifa, ninavyofahamu mimi.

Lakini sasa Mhe. Naibu Spika, kuna jambo linanisikitisha sana. Karibu na jukwaa lile la viongozi wakuu na wageni mashuhuri, Serikali pale inaachia panakuja na makundi yasiyohusika au hata kama yanahusika yanakuja pale makundi yale kwa kudharau viongozi wa vyama vyengine, kwa kusikika na Ofisi ipo na Makamu wa Pili wa Rais yupo, wanadharau mpaka yule Makamu wa Kwanza wa Rais, wanajejea na wanakejeli.

Sasa katika hili naomba niulize, katika Sherehe hizi za Mapinduzi ni za CCM au ni za Serikali. Sasa kama ni za Serikali basi hii tabia ya kukaa pale watu wakawadhalilisha watu wa vyama vingine na kuwadharau haipendezi, wakati zinazotumika pale ni pesa za wananchi kwa lengo la kuimarisha Mapinduzi haya na kila siku wanazungumza hapa wenyewe Chama cha Mapinduzi Mapinduzi daima, lakini sasa Mapinduzi daima sio kwa ighlali, Mapinduzi haya wayaenzi itakiwavyo.

Mhe. Naibu Spika, katika hayo maagizo ya Kamati kwenye Ofisi ya *CAG*. Ripoti ya Kamati ilisema inaitaka Ofisi ya *CAG* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ilete ripoti hapa Barazani ya mishahara hewa, lakini kwa bahati mbaya sana hakuna dalili ya kuletwa na hili linaonesha dharau kwa sababu ya hizi Kamati zinazochaguliwa na Baraza la Wawakilishi hapa kufanyakazi katika maeneo tofauti zinadharauliwa, zinaonekana hazifanyikazi, kwa sababu kama zinakubalika Kamati hizi zinazofanyakazi na kutumia pesa za walipa kodi wa nchi hii, basi ingelikuwa zile Ripoti za Kamati zao zinatekelezwa na kuheshimiwa, lakini mpaka leo hii sijaona dalili na sifikirii kama italetwa hapa ripoti hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, naomba sana Serikali inapoteza pesa nyingi kwa Baraza la Wawakilishi kuunda Kamati zilizomondani ya Baraza kwa kufanya kazi kila baada ya wiki mbili katika maeneo tofauti, inapoteza nguvu na pesa, lakini baadaye hatuoni maslahi yake yaliopo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.*(Makofi)*

**Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia maagizo haya ya Kamati pamoja na utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi naanza na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa pili, agizo namba 1, linalosema kwamba; "Kamati inamtaka waziri anayeshughulikia masuala ya ardhi kutoa maelezo ya kina, ufafanuzi ndani ya Baraza hili juu ya mmiliki halali wa eneo linalotaraji kujengwa kituo cha kubadilishia tabia huko Tunguu".

Mhe. Naibu Spika, katika maelezo yake ya mwisho niseme kwamba utekelezaji ulisema kwamba kutokana na mazingira ya eneo ambalo ni kubwa zaidi kuweza kukidhi haja ya ujenzi unaokusudiwa na kuwa mbali na mji.

Lakini niseme Mhe. Naibu Spika, hawa ni binadamu kama binadamu wengine, tukisema kwamba watu hawa tunawajengea eneo lililo mbali na mji itakuwa tunawatia roho mbaya. Mimi nadhani katika maneno yake angesema kwamba;

> "Hapa tuanze kikubwa zaidi kuweza kukidhi haja ya ujenzi unaokusudiwa kujegwa basi na kukusudiwa", lakini isingetiwa "na kuwa mbali na mji".

Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu cha 2 kinachosema kwamba;

> "Serikali kuipatia Idara ya Mazingira na kuhakikisha kuwa miradi yote ya Serikali na ya watu binafsi binafsi inafanyiwa tathmini ya kimazingira".

Mhe. Naibu Spika, Hii pamoja na utekelezaji wake niseme kwamba hili ni suala muhimu sana, Serikali kuyafanyia tathmini ya mazingira, kiasi ambacho tunajua mazingira ya nchi kavu na ya baharini. Sasa katika mazingira ya baharini tukiangali ujenzi unaojengwa na mahoteli unakuwa ni tatizo, kwa sababu mule muna viumbe hai ambavyo vinaishi katika bahari na huwenda vikatoweka wakati wa ujenzi huo.

Vile vile. Mhe. Naibu Spika, nikija katika ukurasa wa 3 unaosema;

> "Kamati inataka Idara ya Mazingira ishirikiane na Bodi ya Viwango zaidi Zanzibar *ZBF*, ili bidhaa zinazoagizwa ziwe kwenye viwango vizuri kimatumizi na kiafya".

Mhe. Naibu Spika, hili niseme Serikali iwe makini sana kutokana na bidhaa za mitumba. Bidhaa hizi zinazoingizwa zinaleta madhara makubwa sana hasa kwa wananchi. Hii hutokana na madhara ambayo hutokezea katika kiwiliwili cha binadamu wanaponunua mitumba hii na kutokea madhara ya kiwasho au mapele katika mwili.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri, aliangalie sana suala hili kutokana na bidhaa hizi. Vile vile, Sheria ya Mazingira ihakikishe inaleta katika Baraza hili mianya yote ya uharibifu wa mazingira iwe inazibwa.

Mhe. Naibu Spika, hapa niseme kwamba pamoja na sheria hii kuletwa katika Baraza la Wawakilishi, lakini niseme kwamba katika kikao cha Baraza hili la Wawakilishi kilichopita, naiomba Serikali isimamie sheria hii kwa makini sana, kuliangalia hasa suala la mazingira ili kuona kwamba kuna visiwa ambavyo sasa hivi vinaanza kutoweka kama vile Kisiwa Panza.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa katika Kamati ya Viongozi Wakuu ambapo wakati huo nilikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, tulitembelea Kisiwa Panza. Ukiangalia ile sehemu ambayo ilikuwa ni makaburi wanazikwa watu na mpaka sasa hivi maji tayari yameshagawa sawa sawa na kupanda juu.

Kwa hivyo, naomba pamoja na sheria hii kuipitisha Barazani, lakini vile vile Mhe. Waziri, alione hili ambalo sasa hivi ni tatizo sugu na kuna visiwa vingi sasa hivi vinaanza kutoweka, kikiwemo Kisiwa Panza, Matumbini na visiwa vyengine na kadhalika. Mhe. Waziri nakuomba na wewe ulione suala hili.

Pia, Mhe. Naibu Spika, nije katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Nije katika sekta za uchumi, kama ilivyoeleza hapo nadhani na wenzangu wengine wanaiona. Lakini hii niseme inatokana na makusanyo ya walipa kodi. Je, sekta binafsi ambayo inatarajiwa kufaidika na ukuaji huu wa uchumi, Serikali imeweka mkakati gani ili kuwanufaisha na wao?

Mhe. Naibu Spika, nija katika ukurasa huo huo wa 5 ambao unasema pia Serikali inaendelea na mazungumzo na wawekezaji kwa ajili ya kufanya matengenezo ya uwanja wa ndege Pemba.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba wakati wa utanuzi wa uwanja wa ndege wa Unguja kulitokea stofahamu au mabishano kati ya ma-*engineers* wa Serikali. Hapa Mhe. Ismail Jussa, nadhani alilizungumzia sana suala hili. Kuliibua mjadala mkubwa katika Baraza la Wawakilishi, kiasi kwamba baadhi ya sehemu za uwanja huo kuvunjwa na kujengwa upya katika baadhi ya sehemu za *VIP*. Je, Serikali imejipanga vipi katika suala la ujenzi wa uwanja wa ndege utakaojengwa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, nija katika sehemu ya saba kwenye sekta za kijamii, Serikali inaendelea na juhudi zake za kuwapatia wananchi huduma bora za afya, elimu na maji safi. Kwa upande wa afya inaendelea na kupandisha hadhi baadhi ya vituo mbali mbali vya afya, pamoja na kujenga wodi hasa za akina mama na watoto. Aidha, kumeweza kuzipatia hospitali zetu vifaa vya kisasa pamoja na usambazaji.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia sekta za kijamii ni sekta moja wapo ambayo kila mmoja wetu inamgusa, hadi leo hii tunazungumzia viongozi wa kitaifa wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuhusu suala la bima za afya. Je, Serikali inaliangalia vipi suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 8 ambao unasema Hospitali ya Mnazi Mmoja imeimarishwa ili ifikie lengo la kuwa hospitali ya rufaa.

Mhe. Naibu Spika, nadhani sitoweza kuendelea hapo, lakini niseme pamoja na uimarishaji wa huduma za afya ili zifikie lengo, hospitali ya rufaa lakini bado tatizo katika hospitali hii ya Mnazi Mmoja *DNA machine* ni lini italetwa ili kuondoa mikwaruzano baina ya wananchi ambao wanatiliana shaka.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kuna *CT Scan* ambayo hii ni moja tu katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Je, Mhe. Naibu Spika, Serikali imejipanga vipi kuleta *CT Scan* nyengine itakapotokea kuharibika *CT Scan* hii ili watu wetu wasipate matatizo ya kusafiri kwenda Bara kufanya vipimo.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa 12 kwenye agizo namba 1 linalosema; "Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ichukuwe hatua ya kufanya *CCTV camera* katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kuimarisha usalama.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia usalama wa viongozi kuna viongozi wetu wengi tu hapa ambao na wao wanahitaji kupata *CCTV camera* katika ofisi zao. Tunaposema kwamba usalama wa viongozi, iwe ni kwa ajili ya viongozi husika, tunaposema tunataka kuweka *CCTV camera* tuweke kwa viongozi wote, sio kiongozi mmoja tu, akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais , Makamu wa Pili wa Rais na Rais mwenyewe, ili kuweka usalama kwa viongozi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile, narudia nilipokuwa kwenye Kamati ya Viongozi Wakuu, tulizitembelea sana ofisi mbali mbali ikiwemo Ikulu ya Mkoani na hapa niliwahi kuzungumzia suala hili, Ikulu ya Mkoani ni tatizo na hili linatokezea mmong'onyoko mkubwa sana ambao ni wa kuhatarisha hata hizo nyumba ziliopo Mkoani, pamoja na kuzungumzia yote hayo kwamba nyumba hizi zitajengwa pamoja na nyumba za viongozi, lakini tuangalie ile ni Ikulu, nyumba za viongozi ndivyo, lakini ile ni Ikulu.

Je, kiongozi wetu anapotoka hapa kwenda Kisiwani Pemba tutamuweka katika nyumba ya Ikulu iliopo Mkoani ambayo tayari nyumba ile ina mmong'onyoko na hadi hii leo tunapigia kelele suala hili hili, kwamba ni lini nyumba zile zitafanyiwa ukarabati au lini nyumba zile zitajengwa na nilitoa shauri kwamba nyumba zile kujengwa pale Ikulu hapafai. Ni afadhali ingetafutwa sehemu ambayo zitajengwa nyumba za viongozi wetu wakapata kuishi. Lakini hatuwezi kuwachukua viongozi wetu tukawaweka pale Kijiane na mmong'onyoko ule wa ardhi unaoelekea katika bandari hili ni tatizo kubwa sana.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kuhusu *fence* ya Ikulu Mkokotoni, hili nalo tulilizungumza, tuziangalie sana nyumba za viongozi ni tatizo, tusidharau kabisa nyumba za viongozi. Jamani kiongozi mzima hata ile *fence* ambayo anafikia pale Ikulu inakuwa ni tatizo, kwani mpaka hii leo *fence* ile haijajengwa. Nadhani bado hatujawa sawa.

Mhe. Naibu Spika, nija katika kuandaa miradi itakayoweza kushughulikiwa ukarabati pamoja na mmong'onyoko wa ardhi uliopo eneo la Ikulu ya Bwefumu. Suala hili nilipokuwa katika Kamati ya Ofisi za Viongozi Wakuu tuliitembelea Ikulu hii, lakini pia nikatoa ushauri kwamba nyumba ile ifanyiwe, sio ukarabati, ile nyumba iangaliwe kwa sababu kuna maji yanapita chini kwa chini ambayo yanaingia ndani ya nyumba, hilo ni tatizo, hatujui nyumba ile inaweza ikabomoka mara moja ikatumbukia ndani, kwa sababu maji yanapasua kwenye miamba, yanaingia ndani na yameshafanya njia hasa mpaka kwenye sehemu ya nyumba ile.

Nilisema Mhe. Naibu Spika, liangaliwe suala la nyumba ya Bwefumu ambayo sasa hivi ni tatizo na ile ni Ikulu ambayo anafikia kiongozi wetu, suala hili liangaliwe kwa kina, hii ni hata tena kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nilisema pale wapelekwe wachunguzi wakaangalie na uchunguzi ule ufanywe, maji haya yanafikia hatua gani yanafika mpaka kwenye nyumba au la, lakini hadi hii leo inarudishwa hapa bado nyumba hiyo inataka kufanywa matengenezo sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nikae kitako, ahsante nashukuru.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuweza kufika hapa leo, lakini tukaendelea na mambo yetu ambayo tunakawaida ya kujipangia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukrani hizo sasa niwashukuru Wawakilishi wenzangu, pamoja na mawaziri kwa ujumla wao, hususan hawa wanaosimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Serikali, kutokana na taarifa yao ambayo wameiwasilisha na baadae tukaweza kusomewa hapa kama ambavyo tumeisikia.

Vile vile, niwapongeze mawaziri kutokana na namna walivyojibu maagizo yale ambayo yalikuwa yametolewa katika wizara mbali mbali juu ya utekelezaji wa mambo ambayo Wawakilishi waliyaagiza katika maeneo mbali mbali ambayo walikuwa wamekwenda. Naishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imesimamia na kutekeleza yale ambayo yalikuwepo katika uwezo wao na kufanya kwa kadiri ambavyo ilikuwa imefanyika.

Baada ya hatua hiyo Mhe. Naibu Spika, na mimi nirejee pale ambapo mwenzangu amemalizia juu ya suala zima lile la ofisi ambayo imepambana na mmong'onyoko katika Ikulu ya Mkoani.

Mhe. Naibu Spika, eneo hili hata mimi niliwahi kulitembelea na kusema kweli hili eneo kutokana na hali ilivyo na Jiografia ya mazingira ya Pemba, eneo hili ni kweli liko katika hatari na linahitaji kufanyiwa kazi au kuonekana kwa juhudi za dharura, ili kunusuru athari ambayo inaweza kuja kujitokeza baadae.

Lakini nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Pale napo ilikuwa katika taarifa kule, kuna eneo ambalo linazungumzia suala la upande wa *ZIPA* katika kutekeleza na kusimamia sheria ipasavyo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wawekezaji hubahatika kupata vibali pasina kufuata zile taratibu za tathmini ya kimazingira, jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Sasa suala hili ningeliomba sana, wale watu ambao wapo katika sekta ya mazingira Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, suala hili walisimamie vizuri na kuhakikisha kwamba taratibu za kimazingira zinafuatwa kwa mustakabali wa kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri katika nchi yetu na watu hawaepuki sheria ambazo tumeziweka wenyewe katika nchi yetu.

Suala jengine ni lile ambalo Mwenyekiti alipokuja hapa alisemea juu ya suala zima linalohusiana na uingiaji wa maji chumvi katika maeneo zaidi ya 150, likiwemo hata eneo la mjini katika eneo langu hili ninaloishi la Kilimani, ambapo maji chumvi sasa yanaondoka katika bahari na yanakuja katika yale majumba ya maendeleo. Eneo hili ningependa sana hatua za dharura zifanyike, ili kunusuru hali ambayo itaweza kujitokeza ambayo inaweza kuleta athari kwa wakaazi katika maeneo haya, sio kwamba iwe ziara tu zinaendelea lakini utekelezaji wake ukawa hauridhishi. Ningeomba sana suala hili liweze kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nakuja katika suala linalohusiana na Ofisi ya Mkamu wa Pili wa Rais. Katika ofisi hii nina maeneo mengi kidogo ya kutembea; Moja ni suala zima linalohusiana na *escort* za gari ambazo wanatumia viongozi.

Mhe. Naibu Spika, kwa umakini kabisa nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa hatua ya kupata angalau gari mbili katika kusaidia *escort* ya viongozi wetu wakuu, lakini bado gari hizi hazitoshi na naomba sana juhudi za lazima zichukuliwe ili kuhakikisha kwamba viongozi wetu wanapatiwa gari za ziada ili waweze kwenda vizuri katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku, aidha ziwe za Serikali au masuala mengine ambayo yatakuwa yanawahusu wananchi kwa ujumla wao.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakuja katika jengo letu ambalo tunakaa. Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, nianze na jengo letu hili zuri, linavutia, lina rangi nzuri, lakini lina matatizo lukuki ndani yake. Naomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ifanye utaratibu wa kukaa na uongozi wa Baraza la Wawakilishi, ili kuweza kuchukua juhudi za haraka na za lazima kuhakikisha kwamba jengo hili ambalo limegharimu fedha nyingi sana liweze kufanyiwa marekebisho kwa yale maeneo yote ambayo yana matatizo ya hapa na pale, ili kunusuru hali isije ikawa mbaya na athari ikawa kubwa na fedha nyingi baadae zikaja zikatumika kwa ajili ya marekebisho ya jumba hili.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika kitabu chetu hichi ukurasa wa tisa juu ya suala zima linalohusiana na Idara ya uratibu kwa shughuli za Serikali Zanzibar. Mimi nasema naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa zaidi ya asilimia thamanini na tano (85%) ya mambo ambayo ilikuwa imejipangia.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio msimamizi mkuu wa shughuli zote za Serikali ndani ya Zanzibar hii, mambo na maendeleo na yote ambayo yamejitokeza yametokea haya chini ya usimamizi mahiri wa Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi. Na kwa namna fulani kama nilivyokwishasema mwanzo utekelezaji wetu wa ilani ya Chama cha Mapinduzi umefanikiwa kwa zaidi ya asilimia 65% katika mambo ambayo tulikuwa tumejipangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi sikubaliani na usemi kwamba Ofisi au iwe hata kiongozi mwenyewe Makamu wa Pili wa Rais kwamba ameshindwa kazi, hili nalikataa na nasema kwamba Makamu wa Pili wa Rais ametenda kazi ambayo ametumwa na Chama chake na ameitekeleza kwa ufanisi mkubwa kabisa, na hayo yote yanathibitika kutokana na mambo mbali mbali ambayo miaka hii mitano ambayo tunaimalizia mwaka huu Disemba 31 tayari yamekwisha kujitokeza.

Mhe. Naibu Spika, nataka tukubaliane kwamba awamu ya saba ya uongozi uliopo chini ya Jemedari imara Dkt. Ali Mohammed Shein, ilirithi nchi hii ikiwa na makusanyo ya shilingi bilioni si zaidi ya 13 kama nilivyosema kipindi cha juzi, leo narejea tena. Taasisi za Serikali zinazokusanya kodi zinafanya vizuri, *ZRB* inafanya viruzi, *TRA* inafanya vizuri na nawapongeza kwa hili kwa kazi ambayo wanaifanya *ZRB* na *TRA*. Lakini vile vile hata Wizara za Serikali zinazokusanya kodi kwa yale mambo ambayo yanapaswa kuwa yanaipatia kodi Serikali hii iliyopo madarakani nasema nazo pia zinafanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kama juzi nilivyozungumza lipo katika maeneo mawili kwa matatu, Kwanza *GBS* na pili misaada, lakini tatu ni mikopo. Mhe. Naibu Spika, kwa mfano Zanzibar tulikuwa tunategemea tuweze kupata mkopo kwa mfano nasema wa shilingi bilioni 40 za Kitanzania, lakini matokezeo yake msaada ule au mkopo ule kutoka shilingi bilioni 40 tukaweza kupata bilioni saba, kuna mambo ya msingi ambayo yanapaswa kufanyika ndani ya nchi yetu, na wale watu ambao walikuwa wametuahidi kutupatia ile misaada wakakatisha misaada yao na wakatoa katika utaratibu kama huo. Je, Serikali ilikuwa ifanye nini, ni lazima sasa Serikali iweze kukitumia kile kile chake ilichonacho kuweza kutimiza yale mambo ya msingi ambayo yana lazima kufanyika katika kipindi hichi tulichonacho ili shughuli za kiserikali na shughuli za wananchi wake ziweze kwenda. Sasa hapo ndipo ambapo ule ufinyu wa bajeti unapojitokeza.

Sasa suala hili halisababishi kuweza kuonekana kwamba kazi ya uratibu ambayo inafanywa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeshindikana au Makamu wa Pili wa Rais hawezi kufanya kazi, waswahili tuna msemo wetu tunasema kwamba kile kidogo kilichopo basi kitumike vizuri na tuweze kufaidika sote, sio kwamba tusubiri kingi tuanze kufanya fujo na batara ndani yake.

Hivyo kidogo tulichonacho na mimi naisifu sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kwamba tunategemea baadhi ya misaada kutoka kwa hao wenzetu, lakini hatubweteki tukasema kwamba kama misaada haikutokea basi na yetu hatuwezi kuyafanya, hapana, namsifu sana Dkt. Mohammed Shein, kwa kumtumia kiongozi wake wa shughuli za Serikali Balozi Seif Ali Iddi kutimiza yale ambayo tunayotaka na tukahakikisha kwamba yanakuwa kwa maslahi ya nchi yetu na wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, mambo ya Maendeleo ambayo yamefanyika katika awamu ya saba ni mengi na tukianza kuyazungumza hapa hatuwezi kuyamaliza, lakini mifano hai ipo na mfano mkubwa kwa sasa hivi hata meli ambayo keshokutwa tu inakuja kuwasili hapo ni katika jitihada hizo hizo za usimamizi mzuri wa Serikali yetu, chini ya mfumo huu huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hivyo kama tukitaka kulinganisha tusipeleke kasoro katika

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kama tunaamua kufanya mlinganisho basi mlinganisho huo mimi nahisi tuitathmini Serikali ya umoja wa kitaifa kwa ujumla wake.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ukiangalia mambo ambayo yaliweza kutekelezeka vizuri kabla ya kuwa na Serikali ya umoja wa kimataifa, ukiangalia katika *percentage* wakati ulipokuwa na yule anayeshinda anaunda Serikali tuliweza kufanya mambo vizuri zaidi, na kwa ufanisi mkubwa zaidi, na kutimiza yale ambayo yalikuwa yanatakikana Mhe. Naibu Spika, lakini sasa hivi ukiangalia katika utaratibu wetu tulionao wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuna mambo mengi sana yanakuwa na gati gati katika utekelezaji wake. Sisemi kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa haifai, sikuwa na maana hiyo, isipokuwa bado tunahitaji muda wa ziada Wazanzibari kuweza kuendelea kufahamu, kuelewa na kujua mantiki hasa ya nini Serikali ya umoja wa kitaifa ndani ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, miaka minne ya mwanzo katika Baraza lako hili hili Tukufu la Wawakilishi la Zanzibar ,ilikuwa huwezi kuona tofauti baina ya huyu Mjumbe ametokea chama gani na huyu ametokea chama gani, wakati ule Mhe. Naibu Spika, ilikuwa tunajenga nchi kwa umoja wetu na ilikuwa tunafanya maendeleo kwa umoja wetu, lakini sasa hivi wakati wa kipenga umetimia Mhe. Naibu Spika, ndio maana kila mtu sasa anataka mwenzake aonekane kwamba huyu hana maana na huyu ndio mwenye maana ili aweze kutimiza matakwa yake ambayo anayataka katika kwenda kuwaomba wananchi na kuweza kupata ridhaa ya kuweza kuongoza nchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba tu kwamba *mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni*, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya jemedari wetu Dk. Ali Mohammed Shein yametendeka mambo mengi, yamefanyika mambo mengi, na yataendelea kufanyika mambo mengi chini ya uongozi wa utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Nasikitishwa sana kuona kwamba miongoni mwetu tunafika pahala tunasema kwamba Serikali hii bora ikae pembeni, lakini ije Serikali nyengine ambayo itaongozwa na chama chengine ndio ambayo itaweza kufanya mambo ambayo yatakuwa na mustakbali mzuri kuliko Chama tawala ambacho kinaendelea na madaraka yake katika nchi yetu. Na wengine walifikia hadi kukejeli kusema kwamba Oktoba CCM itakaa chonjo na Chama cha Wananchi kiweze kuendelea na madaradaka. Nasema tena mbele ya chombo hichi bado hakijatokezea chama cha kuweza kuitetemesha CCM mpaka dakika hii, CCM itaendelea kuongoza na itaendelea kutoa ushindi katika uchaguzi unaokuja mwaka 2015 katika Mwezi wa Oktoba mwaka huu.

Lakini kama hiyo haitoshi, nasema haya si kwamba patatumika ubabe kama watu wengine wanavyofikiria hadi kuzungumza kwamba tutang'ang'anuana, CCM haina utaratibu huo, CCM inaomba ridhaa ya wananchi na inakubaliwa kupewa ridhaa na wananchi na mwisho wa habari inaongoza nchi kwa ajili ya kupewa ridhaa na wananchi hao. Kwa hivyo kama ambavyo wananchi hawa wamekwishafanya nyuma sidhani kama mara hii watafanya mabadiliko na wafanye mengineyo. Na hayo Waheshimiwa Wajumbe yatajidhihirisha pale ambapo wananchi watajitokeza kwa wingi tarehe 30 Oktoba kama ambavyo tumesikia tarehe 30 Aprili, kwanza kuipitisha Katiba iliyopendekezwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Katiba tuliyonayo sasa ina mambo mengi ambayo hayatoshelezi ndio maana tukasema kwamba Katiba iliyopendekezwa tumeongeza mambo mengi ambayo yataondoa kero, kadhia na mambo mengine ili kuleta mustakbali mzuri kwa Wazanzibari, kwa hivyo nachukua fursa hii kuwaomba Wazanzibari wenzangu hata wale waliokataliwa wajitokeze kwa wingi waende wakaipigie kura za ndio Katiba iliyopendekezwa. *(Makofi)*

La mwisho Mhe. Naibu Spika, kuna wenzetu hapa walikuwa wanazungumzia suala zima la uwajibikaji na kuheshimu madaraka. Mhe. Naibu Spika, nataka kusema kitu kidogo hapo tulishuhudia hapa katika Baraza hili hili Mhe. Naibu Spika, mwenzetu alivyokuja kujiuzulu katika nafasi ya Uwaziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa kipindi kile ambacho sasa hivi ni Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu. Katika *Speech* yake ambayo *Hansard* inazungumza juu alipotakiwa kujiuzulu anasema kwanza alizungumza na Katibu Mkuu wa Chama chake Maalim Seif Sharif Hamad, ambapo kwa wakati ule hakuwepo nchini.

Lakini kwa mujibu wa *hansard* mtu wa pili ambaye alizungumza naye alikuwa ni Mwenyekiti wake wa chama cha Wananchi Prof. Ibrahim Lipumba na mtu wa tatu ambaye alizungumza naye, ati alikwenda Ikulu kwa ajili ya kumfuata Rais lakini akaambiwa hayupo. Sasa hapa naona mtaangalia jinsi gani haya masuala ya uratibu, au masuala ya kuenziwa yule kiongozi ambaye alikuwa anaambiwa kwamba yeye ndio mwenye madaraka ya kuamua na kusimamia watu hawa lakini utaratibu wao ndio uko kama hivyo.

Naomba baada ya maneno hayo Mhe. Naibu Spika, niunge mkono taarifa ya ripoti hii kwa asilimia kwa mia, na nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji tumemaliza sasa nitamwita Waziri mmoja mmoja kuja kutoa maelezo na mwisho atamalizia Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa hivyo namwita Waziri wa Mwanzo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, Dkt. Mwinyihaji Makame.

**Mhe.Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata fursa hii kuja kufanya majumuisho ya michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe walioitoa kwa upande wa Wizara yetu hii ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kwa kuwasilisha maelekezo yale au utendaji ule wa maagizo kwa niaba yangu wakati nikiwa safarini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niishikuru sana Kamati yetu inayosimamia viongozi wakuu inayoongozwa na Mheshimiwa Hamza Hassan Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Wenyeviti, na Mwenyekiti wa kamati yetu kwa miongozo, maelekezo na mwisho kutupa maagizo ambayo tumeyafanyia kazi.

Vile vile, naomba niwashukuru Mjumbe mmoja mmoja kwa michango yao ambayo wamekuwa daima wanatupa katika kuendeleza Wizara yetu, lakini pia naomba nimshukuru Mheshimiwa Shadya Mohammed Suleiman kwa kusoma ripoti ile ya kamati kwa niaba ya Mhe. Hamza Hassan Juma, naomba nikushukuru sana Mhe. Shadya.

Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ripoti ni matokeo ya ziara walizofanya katika *sections* zetu mbali mbali za Wizara takriban kwa mwaka mzima au si chini ya miezi tisa. Na haya waliyokusanya tumebadilishana mawazo huko *field,* tukafanya majumuisho na mwisho wakaandika ripoti. Kwa hivyo kama yamejirudia mimi kwa kweli kwa mtizamo wangu na nitasema baadae sikuona kama imejirudia labda lile somo limejirudia, lakini maagizo yale ni tofauti kabisa na nitatoa mifano hapa kusema ipo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla waliochangia kwa upande wangu, *issues* ambazo zimenigusa kwa upande wangu kwa kweli walikuwa kumi na saba (17) na naomba kwa heshima niwatambue mmoja mmoja Mhe. Naibu Spika.

1.Mhe. Shadya Mohammed Suleiman kwa niaba ya Mwenyekiti
2.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3.Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Mji Mkongwe)
4.Mhe. Salim Abdalla Hamad (Mtambwe)
5.Mhe. Salma Mohammed Ali nafasi maalum za Wanawake,
6.Mhe. Mohammedraza Hassanali (Uzini)
7.Mhe. Ali Salum Haji (Kwahani)
8. Mhe. Hamad Masoud Hamad ( Ole)
9. Mhe. Abdalla Mohammed Ali (Mkoani)
10.Mhe. Hija Hassan Hija
11.Mhe. Marina Joel Thomas
12.Mhe. Mohammed Haji Khalid
13.Mhe. Mussa Hassan Mussa
14.Mhe. Abdalla Juma Abdalla
15.Mhe. Farida Amour Mohammed
16.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
17.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Mhe. Naibu Spika, wote hao tunasema ahsante sana kwa maoni yenu, michango yenu, ingawa kauli ile wengine hawaipendi, lakini ndio ukweli wenyewe kwamba sio yote waliyoyasema nitayajibu. Kwa hiyo mimi niseme tumeyachukua, tutayazingatia, na tutayafanyia kazi. Hakuna maneno mengine, Kiswahili tajiri lakini naona haya ni *very specific*. *Inshaallah* tukirudi mwakani Mwenyezi Mungu (*S.W*) na majaaliwa yake mwenyewe mtakuja kutuuliza sasa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba kwanza naomba nimshukuru yeye alikuwa ni mchangiaji wa mwanzo kabisa. Yeye hasa alizungumzia suala la miradi ya *PPP* pamoja na lile suala la Kitengo cha Mamlaka ya Kuzuia rushwa.

Tunamshukuru Mhe. Mshimba kwa maoni yake. Nataka kusema tu kwamba serikali ipo *serious* kwenye suala la *PPP*. Hii ni *concept* mpya imekuja kwetu, tumeipitisha juzi hapa na tumeona kwamba huko nyuma kwa utaratibu uliokuwepo tulikwama, sasa tufuate na wenzetu (*globally*) wenzetu wanafanya vipi. Hiyo ndio *the top of the town* kwa *World Bank* na wengineo. Si vibaya tumechelewa lakini lazima tujifunge kidete na sisi tuweze ku - *cope up*.

Serikali iwe *serious* na pia Mhe. Muhammedraza alizungumza kwamba wale wajanja wajanja nafikiri sheria ile tumeipitia na sote tumeiona, ile *room* ya ujanja ujanja kwa kweli haitokuwepo. Zote *private sectors,* wanafanya biashara na hakuna anayetaka kupata hasara. Kwa hiyo sifikirii kama kutakuwa na wazo tena la ujanja ujanja, lakini *Inshallah* na sisi sote tutakuwa macho na ile Kamati iliyoundwa ya wataalamu kufanya kazi kwa pamoja.

Mhe. Makame Mshimba, alipongeza suala zima la kupewa vitendea kazi. Hilo ndio lengo letu kwa Mamlaka ya Kuzuia rushwa. Kweli kama alivyosema gari wamepatiwa na Ofisi wamepatiwa, walinzi wapo wanafanya kazi vizuri, unajua yale mambo hayaji yote kwa mpigo, lakini mlivyotuagiza na yeye mwenyewe Mhe. Mshimba ni Mjumbe wa Kamati yetu basi hayo tumeyachukua.

Mhe. Naibu Spika, katika hoja zilizotolewa ni pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe kueleza kuhusu kujirudia kwa maelezo ya Kamati mara kwa mara, kwa hivyo kupelekea kudai kuwa serikali haifanyi kazi maagizo ya Kamati. Hili lilizungumzwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Hamad Masoud.

Mimi nataka nizungumze kama nilivyotaka kusema kwa ufupi tu. Hizi ni *issue* na kadiri unavyoishi *issue* huimalizi, suala hulimalizi au kama una-*deal* na watu, binadamu hulimalizi moja kwa moja. Wewe utatekeleza utakapofika, ukishakutekeleza na yeye anafikiri litakuja jengine utekeleze hilo ndio suala la msingi, wewe jitahidi utekeleze kwa sababu kila siku tunapokwenda *field* hawarudii Waheshimiwa maswali yale yale, wanaibua maswali mapya.

Nitatoa mfano kwenye utekelezaji wa Wizara yetu kabla haijagaiwa, wizara iliyokuwa ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Tawala za Mikoa. Kulikuwa na agizo mchango wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwa Zanzibar, sambamba na mpango mkakati wa kuendeleza uchumi wa Zanzibar. Leo Mhe. Abdalla Mohammed Ali wa Mkoani kaliuliza na kitabu kipo hichi hapa na imechapishwa na mimi naomba nikisome.

> "Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi wamesaidia ujenzi wa madarasa skuli ya Unguja Ukuu, thamani kwa Skuli za Kwale na Ziwani Kisiwani Pemba, na vifaa vya Afya kwa Hospitali ya Chake chake Pemba, *Diaspora* hao".

Aidha Benki ya Watu wa Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Al-ahli ya Oman, imefungua *account* ambayo itarahisisha utumiaji wa fedha na biashara. Sera ya *Diaspora* itatoa muongozo kwa upana zaidi wa kuwashirikisha Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, kuchangia maendeleo ya Zanzibar.

Sasa kama nilivyosema hiyo ni suala la *Diaspora* tushajibu hii bajeti tunayosema ya mwaka 2012 leo 2015 Mhe. Abdalla anazungumza suala hilo hilo tena yeye anasema halina maana tuikate kwenye bajeti. Jamani mimi naona kidogo Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa. Hivi tukimaliza hapa waende wakavipekure kidogo kabla ya kuchangia. Humu kuna mambo mazito tunaandika *for reference* ni muhimu sana.

Leo ukweli inauma sana Mhe. Abdalla anasema tufute *Diaspora*, maana yake ile *concept* yenyewe kama, mimi sisemi haijui, anaijua lakini hebu tizama kidogo. Watu wote mpaka inaundwa Idara wanaheshimiwa tumejenga maskuli na tumesharipoti humu, yeye anasema tuifute haina maana.

Mhe. Naibu Spika, kama ninavyosema hivi vitabu tuvipange kidogo, najua lazima tubadilishane uzoefu, wewe viweke mahala kila mara unakwenda unavuta tu, unafanya *reference* kabla hujachangia, mambo ndio haya. Labda ndio Mhe. Ismail Jussa anaposema tunauliza mambo hayo kwa hayo. Sasa hilo mimi nikulaumu wewe Mhe. Ismail Jussa, unayefanya *reference* halafu ukachangia. Mambo haya yako wazi, tumeshasema na mifano ipo. Mimi nasema tufute mradi huu hauna maana, *are you serious*?

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ismail Jussa, yeye pia alizungumza suala hilo hilo la kwamba yanajirejea rejea. Kama nilivyosema hayarejei maswali, inarudia *issue* na mfano wizara yetu *issue* ya *Diaspora* ni ya *Diaspora* ni suala kubwa sana, pana, leo unauliza huku, leo unauliza huku, lakini hayajirejei maswali. Kwa hiyo mimi nataka kama inaandikwa ile aliyosema *copy typist* imejirudia mpaka *typing* imepigwa hivyo hivyo, hilo swali jengine, hilo swali waulize wenyewe Kamati walioandika hilo usinitupie Wizara Mhe. Jussa.

Mhe. Naibu Spika, jengine Mhe. Ismail Jussa alichukua wasaa pamoja na Mhe. Hamad Masoud, kwa kweli kuichambua mimi niseme utendaji wa serikali yetu. Mimi ninachotaka kusema hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa na ina-*comprise* vyama viwili vikubwa na Mhe. Ismail Jussa *is inclusive.* Huwezi kutoka Mhe. Jussa na wewe umo.

Sasa unapokaa pembeni ukasema aah! Serikali hii hivi hivi, unajitukana mwenyewe, *yes*! na wewe *you are part and parcel*. Siku moja niliwahi kumtania Mhe. Ismail Jussa habari ya Mji Mkongwe kule nikamwambia e bwana wee, tukutane leo tupange habari ya kuzoa hizi taka. Akasema aah! mimi si kazi yangu hiyo. Mwakilishi wa Mji Mkongwe huyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi nasema tumejikita, tumekubaliana, tumelishana yamini kwamba tuendeshe nchi hii kwa *spirit* ya Umoja wa Kitaifa. Kwa hiyo sote ni ma- *core drivers,* mimi wa kulia wewe wa kushoto, lakini unaposema unakaa pembeni ungoje mpaka ukamate wewe usukani haitofika siku hiyo, *forget it!*

Kwa nini tunasema tushamsahau, kwa sababu sisi ni wengi na unasema umoja ni nguvu. Tulifanya makosa majimbo matatu kwa sababu watu wetu wenyewe walinuna. *Kutenda kosa si kosa kurejea kosa ndio kosa*, kwa hivyo tumejirekebisha, majimbo matatu yale. Rafiki zangu nawajua mawaziri wengine tena wajitayarishe kukabidhi majimbo yale. Huo ndio ukweli wenyewe, hatutorudia makosa.

Mhe. Naibu Spika mimi sishangai chochote atakachosema Mhe. Ismail Jussa kwa sababu mtu unamwangalia na *perspective* yake. Mhe. Ismail Jussa is *very intelligent* mimi namuheshimu sana kama *lawyer,* lakini sasa anapoamua kusahau maadili yake akazungumza kisiasa, basi tena hapo huwezi ukamlazimisha na hiyo ndio imani yake, *equally* Mhe. Hamad Masoud, Mhe. Hija Hassan hiyo ndio imani yao. Sasa kumbadili ni vigumu sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachotaka kusema *spirit* uliyonayo, tumelishana yamini tuendeshe nchi hii na vyama viwili hivi, Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein yeye katoka CCM, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais, yeye katoka Chama Cha *CUF*, Makamu wa Pili katoka CCM. Tena ajabu wanavyokaa pamoja wao *Alhamdulillah*, wanapanga wanakosoana, wanaelekezana, washauri wanashauriana. Na sisi tufuate hivyo hivyo, ukisema unakaa pembeni unawaachia wenyewe wanaovuruga ni wao sisi hatumo, utakuja kuhukumiwa huko mbele, kabisa kabisa!

Mhe. Naibu Spika, naomba univumilie kwa sababu mambo ni mengi sana yamezungumzwa na mimi ofisi yangu ni kubwa na muhimu lazima tuzijibu hizi *issues*.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni makini, ina dira, inapanga na kutekeleza kwa mujibu wa uwezo wake. Tatizo ni *resources* tu, inapotekeleza wajibu wake pia huwajali wananchi wake, suala la maslahi ya wananchi kwanza ndiyo *prime* hilo ndio kubwa tulitizame, wananchi wetu watafaidika vipi, lazima tu - *sacrifice* sisi lakini tutizame wananchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwajulisha kwamba kwa mwezi Juni, 2003 Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ilikuwa ina maagizo 78 na maagizo yote yalifanyiwa kazi ya kwenye kitabu.

Kwa mwaka 2013/2014 kuna maagizo 10 tu ya Kamati ambayo yamefanyiwa kazi kama ripoti yangu inavyoeleza. Mambo mengine yameelezwa katika ripoti ya Kamati yaliyokuwa sio maagizo, bali ni maoni na ushauri wa kamati ambayo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Mhe. Haji Omar Kheri, anawasilisha taarifa kwa niaba yangu, alieleza kwamba imepokelewa na imefanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, kuna uthibitisho wa kutosha kwamba serikali imepiga hatua kubwa. Namshukuru Mhe. Mahmoud Mussa katika kuwaletea maendeleo wananchi wake na inatekeleza wajibu wake vyema kwa mujibu wa

Ilani ya Chama Tawala cha CCM. Ile ndio muongozo wetu, dira yetu, muelekeo wetu, na tunafanya tathmini baada ya muda. Tumetekeleza vipi dira, hatwendi varange varange tu. *Alhamdulillah*, mimi nasema *intellectuals* wapo waliotengeneza ile, sio kama imekopiwa, imetengenezwa, na sasa hivi tunaandaa nyengine ya Chama Tawala kwa miaka kumi mengine inayokuja.

Mhe. Naibu Spika, jambo la msingi na la kusema tuelewane, majukwaa ya kisiasa yatumike kwa niaba ya siasa, tusiwatukane viongozi wetu au tusitukanane na sisi pia tudumishe hiyo amani na utulivu. Tuwe mstari wa mbele kabisa katika kudumisha amani na utulivu katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, maendeleo hayaletwi kwa kulumbana, maendeleo yataletwa kwa umoja, mshikamano na kuaminiana. Hilo ndio suala la msingi sana.

Mhe. Naibu Spika, suala la maendeleo ni pana sana na panahitajika juhudi za pamoja zikiwemo juhudi za kila mmoja wetu. Uthibitisho mwengine ni kuwepo kwa mazingira mazuri yanayowawezesha wananchi kufanya shughuli zao bila ya hofu wala woga. Kukua kwa uchumi wetu, kuimarika kwa sekta binafsi na kuongezeka kwa wawekezaji Unguja na Pemba. Hivi ni miongoni mwa vielelezo muhimu vinavyothibitisha kuwepo mafanikio katika utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa mafanikio machache yaliyopatikana katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu wa saba.

1) Kuimarika kwa huduma katika sekta mbali mbali za kijamii zikiwemo elimu, afya na upatikanaji wa maji safi na salama.

*2)* Ukusanyaji wa mapato unaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano fedha zilizokusanywa mwaka 2010/11 ni shilingi bilioni 181.4 na mwaka 2013/14 ni shilingi bilioni 330, sawa na ongezeko la asilimia isiyopungua 81.8%. Nashukuru hili Mhe. Jussa pia ka- *acknowledge.*

3) Pato la mtu binafsi limeongezeka kutoka shilingi laki saba, ishirini na sita elfu (726,000)mwaka 2010 kwenda shilingi milioni moja na elfu tatu (1,003,000)mwaka 2012 na hadi kufikia shilingi elfu moja na sabini na saba elfu (1,077,000)mwaka 2013.

4) Ukuaji wa uchumi, umekuwa kutoka asilimia 6.4 mwaka 2010 hadi asilimia 7.4 mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika, orodha ya mafanikio ni ndefu kama ilivyoelezwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba yake ya maadhimisho ya Sherehe za miaka 51 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 2015 pale *Amani Stadium* katika kilele cha sherehe za Mapinduzi.

Naomba sana Waheshimiwa tuisome hotuba ile. Ile hotuba Mhe. Rais kwa kweli kakaa ka-*chart out* mafanikio yetu, matatizo yetu na twende vipi. Kama mtu hajapata *copy* sisi tupo tayari Ofisi yetu kumpatia *copy*, lakini kwa kweli *speech* mojawapo Mhe. Rais ameifanyia kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine lililozungumzwa sana na Waheshimiwa kadhaa ni hatua za kuchukua katika kuzuia athari za mmong'onyoko katika nyumba za Ikulu. Nashukuru Waheshimiwa takriban wengi sana, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Farida Amour, Mhe. Mohammed Abdalla Ali, Mhe. Hamad Masoud, takriban wote wamezungumzia suala la mmong'onyoko.

Kwa kweli suala la mmong'onyoko sisi kama wizara niseme tunalichukua kwa nguvu zote. Lile suala sio jepesi kudhibiti mmong'onyoko. Wewe angalia tu kama wale waliofika Bwefumu walivyosema Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, anasema matokeo ya tabia nchi, yale madaraja ya kuteremka vile vigazi yamechukuliwa na maji. Hata Kibweni, hata zamani skuli ya Tumekuja pale, hayo ndio matatizo.

Sasa kulishughulikia suala lile mpaka kwa kweli utulie upange halafu tuone vipi tutafanikiwa. Na tumefanikiwa kwa sababu tizama pale *Starehe Club* sasa hivi ndio Hoteli ya *Hyatt* ile zege iliyotiwa pale wamedhibiti kabisa. Skuli ya Tumekuja, Hospitali ya Mnazi Mmoja, wamepajenga wamedhibiti kabisa na mmong'onyoko haujafanya kazi tokea miaka hiyo sisi wadogo hatujazaliwa.

Kwa hiyo, ni kiasi cha kukaa na kupanga. Ni mradi mkubwa tumeshauandikia, *Inshaallah* mwaka huu labda tutaangalia bajeti itakavyokwenda japo tuanze tuone, japo tuanze tu tuone japo kwa sehemu moja, lakini suala si jepesi, suala ni muhimu na wengine walidhihaki labda wamesema tunapanda bustani tu. Hatupandi bustani ile ni sehemu moja wapo, kupanda ile mihaliudi au yale majani mazito yale nayo yanasaidia kwa kiwango fulani kuzuia mmong'onyoko, lakini kwa kiwango cha muda mrefu kuna mbinu zake. Kwa hivyo sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Wizara ya Mazingira kuona kwamba suala hili tunalishughulikia ipasavyo. Tunawashukuru Waheshimiwa kwa kututanabahisha katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuendelea na michango ya Waheshimiwa. Mhe. Mshimba na yeye nimeshamzungumza sipendi kumrejea tena lakini Mhe. Jussa na yeye nimeshamgusia kidogo.

Mhe. Hamad Masoud Hamad, alizungumza kwamba maagizo 10 kati ya 41 na hii imezungumzwa pia na Mhe. Jussa. Naomba Mhe. Jussa na Mhe. Hamad Masoud warejee barua ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi aliyetoa maelekezo kwa Waheshimiwa mawaziri kuhusu ripoti ya kamati, barua inasema hii hapa. Uwasilishaji wa Hati Mezani, natoa mfano tu kuhusu ripoti za Wizara mbali mbali kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati za Kudumu.

Sasa utakuta bahati mbaya labda Waheshimiwa walitaka tuzungumze suala zima la maelekezo au ushauri lakini ukitizama kwenye hivi vitabu kama ukurasa wa 4 ukifungua wenyewe kamati nitatoa mfano kamati yetu, hili buku la mwaka huu ukurasa wa 4 maoni na ushauri wa kamati, wametafautisha halafu wamekuja kwenye maagizo ya kamati wametafautisha wenyewe, sasa kwenye maagizo ya kamati ndio wakatoa maagizo yao ambayo mwaka huu sisi tumeyaona kama 9 tuliwaripoti.

Kwa hivyo, lazima watafautishe vile tulivyoagizwa, na Waheshimiwa wanavyoona mambo kule *field* wengine wanashauri lakini wanasema unajua unaposhauri unashauri kwamba aidha unaweza kukubaliwa ushauri wako au kukataliwa lakini si aghalabu sisi kukataa. Tutalichukua lile shauri tutalitizama vipi tutalitekeleza. Lakini agizo moja kwa moja na inatokana kutokana na yale maoni ya ushauri wa Kamati walivyotushauri, basi walivyotushauri na maagizo wameandika wenyewe, haya ndio maagizo.

Kwa hivyo, nataka kusema Mhe. Naibu Spika, kwamba sifikirii kama sisi hatujayajibu, haya tunayajibu na tunafuata maelekezo ya kamati na kubwa zaidi unajua hakuna kitu kizuri kama kwenda *field*, unapokwenda *field* ndio unaona yale mambo moja kwa moja na *alhamdulillah* tunakwenda *field* pamoja nao tunakaa, tunatafakari, tunabuni mbinu pale, basi ndio unachukua tena kwa utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru sana Mhe. Salim Abdalla Hamad kwa ushauri wake kuhusu ujenzi wa nyumba ya Ikulu ndogo ya Micheweni, naomba kumhakikishia tena Mhe. Salim kwamba utata huo kwa upande wetu umemalizika na imethibitika kwamba mkandarasi hatudai na sisi hatumdai kutokana na vielelezo na majadiliano marefu kati ya Serikali na yeye, tumebadilishana *documents*, tumebadilishana fikra na mawazo mwisho tukafikia hapa. Hatua inayoendelea hivi sasa ni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, mkandarasi huyo naye anaweza akaomba zabuni kama anahitaji kufanya hivyo.

Kuhusu ushauri wake wa kutafuta njia mbadala ya kuzuia mmong'onyoko katika majengo ya Ikulu, tumeupokea na kama tulivyosema tutautekeleza. Tunamuahidi kwamba tutatumia njia mbadala kwa kupanda miti ya mihaliudi kwa kuanzia na mengineyo kama iliyopandwa katika barabara ya Gando na barabara ya Mtambwe, hiyo ni kuzuia ule mmong'onyoko.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa shukurani zangu kwa Mhe. Salma Mohammed Ali kwa mchango wake, naomba kumhakikishia kwamba Serikali hivi karibuni ilinunua gari mbili mpya kwa ajili ya matumizi ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na zimeshapelekwa Pemba kwa matumizi ya viongozi hao. Hakuna sasa hivi labda ku-*share* gari kwa viongozi wetu wakuu hao kila mmoja ana *VX* yake, na zile nathibitisha kwa sababu naziona zinalala Ikulu moja kwa moja chini ya utaratibu maalum.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumshukuru Mhe. Raza kwa mchango wake pia, aidha kuhusu utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais naomba kumhakikishia kwamba Mhe. Rais ana wasaidizi wake maalum wanaofuatilia ahadi zake zote anazozitoa. Kuhusu ahadi ya kuezeka ukumbi wa mitihani wa Skuli ya Pwani Mchangani nalo kupitia Wizara ya Elimu zitatekelezwa, tunamshukuru kwa kutukumbusha ahadi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Ali Salum kwa mchango wake mzuri na ushauri alioutoa na ninamuahidi kwamba tumeupokea. Kuhusu suala la kuzuia mmong'onyoko nalo hilo kama nilivyosema tumeshalijibu na tutalishughulikia.

Mchango wa Mhe. Hamad Masoud ulijielekeza zaidi katika utekelezaji wa maagizo ambao majibu yake nimeyaeleza wakati ninamjibu Mhe. Jussa. Aidha kuhusu maelezo yake juu ya uchaguzi wa mwaka 2015 mimi kama nilivyosema Mhe. Hamad kukubadili siwezi, lakini nataka kusema tuwe wastahmilivu, tumesubiri mwaka 2010 baada ya kumaliza, 2011, 2012, 2013, 2014 leo 2015 sasa wewe unapotoa kauli kwamba utashinda, na mimi nazidisha kauli yangu kwamba nitashinda. Kwa hivyo nataka kusema kwamba tusiandikie mate na wino upo, mimi nina imani kubwa kabisa kwamba CCM itaendeleza wimbi la ushindi wa kishindo kama kawaida yake. Kwa vile sababu moja tu kubwa kwamba Chama chetu Chama Tawala kinaungwa mkono na wananchi wengi, hiyo *fact* Mhe. Naibu Spika, huwezi kuikataa.

Kama unaishi nchi hii na takwimu unazo, takwimu ziko wazi kabisa idadi ya watu wote wa Mikoa miwili ya Kaskazini Pemba, wamezidiwa na watu wa Mkoa Mjini Magharibi. Sisemi kwamba wote wa Mkoa Mjini Magharibi ni CCM, lakini hiyo inakuonesha wazi kwamba juu ya *influx;* juu ya kuhama kwa watu kule, naomba nipeni nafasi hiyo kupiga Fatma Fereji haitosaidia hiyo, wewe tulia unisikilize. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wahenga wamesema *wa mbili ni wa mbili tu havai moja*. Tumesema tuna matatizo Zanzibar ya Muungano twendeni tukayetetee matatizo, tuchimbe mafuta yetu, tuondoe matatizo, Mhe. Jussa kanitoroka rafiki yangu hata hakuniaga. Sasa kwa Katiba ya Muungano iliyopo hivi sasa mafuta hatuyachimbi, sasa Katiba hii iliyopendekeza tunachimba mafuta yetu, wazanzibari tunataka nini tena Mhe. Naibu Spika, mikopo tutaweza kukopa, misaada kutoka nje tutaweza sasa hivi kuwasiliana wenyewe bila ya kupitia Wizara ya Fedha ya Muungano.

Maana yake umwambie *layman* anaweza kuyafahamu matatizo tuliyonayo. Mimi kabla sijaondoka kumwachia Wizara ya Fedha Mhe. Omar nilikuwa naona vipi tunavyoumia tunavyopata tabu, sasa leo yale tumeshayasuluhisha sasa tuungane jamani, uchumi tunao tunaukalia! *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba sana jamani, naomba sana Waheshimiwa nyinyi ndio wenye wananchi, naomba sana tuwashawishi wananchi wetu waisome Katiba wafahamu kiliomo wapige kura ya ndio tuondoke hapa tulipo, huo ndio ukweli wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla Mohamed Ali nimeshazungumza sitaki kumrejea tena naomba niseme kwa ufupi tu kwamba ripoti iliyotolewa na Umoja wa Mataifa hivi karibuni inasema kuwa *Diaspora* wapatao milioni mia mbili thalathini watatuma fedha katika nchi zinazoendelea, kiasi cha dola zipatazo bilioni mia tano kwa mwaka 2014 zimetumwa katika nchi hizo. Ni dhahiri kuwa Zanzibar nayo ni miongoni mwa nchi zinazohusika, ni dhahiri kuwa pia bila ya kuwa na Idara madhubuti ya kuwahamasisha wana *diaspora* faida hiyo haitapatikana.

Taarifa ya Benki Kuu Tawi la Zanzibar inaonesha kuwa mwaka 2013/2014 wastan wa dola zipatazo milioni moja zimetumwa kwa mwezi kutoka kwa wana *diaspora* mbali mbali. Aidha faida nyengine ni pamoja na uchangiaji katika sekta ya Elimu na Afya.

Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru Mhe. Hija kwa kutaka kujua maendeleo ya bandari ya mpiga duri. Naomba kumfahamisha kuwa majibu yanayohusika yatatolewa na sekta husika ninamuomba astahmili kidogo, hii haidhuru Mhe. Rais yeye ndio kila kitu lakini madhali sekta husika ipo itakuja kukuelezea tumefika wapi na tunakwenda vipi. Nasema tunakwenda vizuri tu.

Mhe. Marina tunakushukuru sana kwa jinsi ulivyotoa ufafanuzi, na naomba nielezee tu kwamba kuna baadhi ya Waheshimiwa wamekuwa kama hawafurahii waheshimiwa kuchangia *positive* kwa Serikali, aa jamani hiyo mtu ni uhuru wake na mbali ya uhuru wake yeye anaeleza *perspective* anatizama kwa mtizamo wake, yeye anatizama ule ukweli wa mambo ukoje. Kwa sababu wengine kama tunaficha ukweli au ukweli hatutaki tuuseme kwamba tunaipa *credit* Serikali hii mwengine mwache aseme.

Unajua jana tulikuwa na semina ya demokrasia, mwenyewe ulikuwa Mwenyekiti Mheshimiwa, hiyo ndio demokrasia, ni muhimu umsikilize mwenzio anaongea nini. Hata kama hutaki mwenzio kumsikiliza anaongea nini halafu wewe upate *point* hiyo sio nzuri Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, pia kutoa maelezo ya hoja Mhe. Mohammed Haji Khalid alishauri kuhusu ujenzi wa kuzuia mmong'onyoko pale nimeshamjibu Mkoani, aidha alitaka kujua kuhusu hati za Ikulu za Unguja, je zimeshapatikana? Hilo Mhe. Naibu Spika, hilo alisema Mhe. Mohammed Haji Khalid kwamba alikuwa Mjumbe wa Kamati hii na waliwahi kulisema naomba nisome humu. Maagizo ya mwaka juzi.

Hati za majengo ya Ikulu, tunajibu: Gharama za upimaji wa majengo zimelipwa kwa lengo la kuwatafutia hati miliki. Jengo la Ikulu ya Mnazi Mmoja limeshapatiwa hati miliki na majengo yaliyobakia hati zake zimeshafanyiwa uhakiki na imebakia hatua ya kutiwa saini na kukabidhiwa. Sasa tuko wapi, hivi sasa tuna ripoti zaidi hiyo ilikuwa miaka miwili iliyopita tumepewa agizo hilo.

Sasa tunaripoti kazi ambayo tumeshaifanya. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimkabidhi Mhe. Waziri wa Fedha ambaye ndiye msimamizi mkuu wa mali za Serikali katika sherehe za uzinduzi wa usajili wa ardhi uliofanyika *Victoria Garden* tarehe 28 Machi, 2013. Hati ya Ikulu Kubwa ya Mnazi Mmoja imekabidhiwa tarehe 29 Machi, 2013 je, Mhe. Mohammed Haji Khalid aliuliza, je, Ikulu za Pemba nazo zimetoka, je, za Unguja. Sasa naomba nisome *list* ndogo tu hii hapa.

Ikulu ndogo ya Fumba hati namba S176/2012 imetolewa tarehe 28, 2013. Pili Ikulu ndogo ya Migombani hati namba S180/2012 imetolewa tarehe 28 Januari, 2013. Ikulu ndogo ya Kibweni hati namba S177/2012 imetolewa tarehe 28 Januari, pia tarehe 4 Ikulu ndogo ya Migombani hati namba S179/2012 tarehe 28 Januari. Ikulu ndogo ya Maisara hati namba S178/2012 tarehe 28 Januari, 2013 na Ikulu ndogo ya Mazizini hati namba S183/2012 tarehe 28 Januari, 2013.

Mhe. Naibu Spika, agizo limeanza kule na leo tunamshukuru sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kukamilisha ngwe upande wake hizo hati tayari kabisa zimeshatolewa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa mara nyengine tena kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Viongozi Wakuu kwa ushirikiano na ushauri wao wakati wote tulipokuwa tukifanya kazi pamoja. Aidha naomba kutoa shukurani kwa Wajumbe wote waliochangia na kutoa ushauri wao ambao utasaidia katika kufanikisha kazi yetu.

Kulikuwa na wajumbe waliochangia leo Mhe. Naibu Spika, naomba haraka haraka niwaguse tu nao. Kwanza Mhe. Mussa Hassan Mussa tunamshukuru wa Jimbo la Koani kwa mchango wake lakini pia kulikuwa na Mhe. Abdalla Juma Abdalla wa Chonga, anasema ujenzi wa Ofisi ya Rais Pemba bado inapigwa dana dana tu.

Nataka kumwambia Mhe. Abdalla safari hii akienda Pemba ninampigia simu Ofisa Mdhamini uwasiliane nae akupeleke Tibirinzi ndani ya Ikulu uione Ofisi mpya ya Ofisa Mdhamini, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Pemba tayari imeshajengwa. Pale yalipokuwepo majengo mawili ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Ofisi yake, yale ndio yalikuwa mabovu basi moja tumeliangusha tumejenga upya kabisa na iko tayari. Kwa hivyo ninakuomba Mheshimiwa utapokwenda Pemba inafaa wewe una uzoefu wa ujenzi na *land scaping* kidogo ukatusaidie ili tuweze kuona ule ujenzi.

Halafu ulisema kwamba Rais awe mkali, Rais Kagame anapiga risasi anakwenda kijeshi, yule anaongoza kwa nidhamu ya kijeshi, lakini nataka kusema Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein yeye anakwenda kwa mujibu wa sheria na mgawanyo wa madaraka. *Institutions* zipo, sasa sisi ndio viongozi wa *institutions* tuzisimamie tusimwachie Rais, maana tunangoja mpaka Rais aseme atafanya mangapi Rais, lakini sisi tunaosimamia *including* sisi mawaziri pamoja na mimi tusimamie taasisi zetu pamoja na nyinyi Wawakilishi tusimamie maeneo yenu ndio utawala bora huo. Tunapozungumza utawala bora, uwajibikaji na uwazi Dkt. Shein ni muumini mkubwa wa utawala bora yeye ndio *alhamdulillahi* ndio aliyeanzisha chini ya Mhe. Rais mstaafu Aman Abeid Karume ile Wizara ya Utawala Bora.

Kwa hivyo, yeye ni muumini wa kila *institution* na kila mtu afanye kazi kwa upande wake, ile *discipline* ya woga ya Paul Kagame kijeshi tu, *yes sir,* kaza mguu hayupo aa. Lakini hebu tujiulize kweli Paul Kagame ana *democracy* kule nchini mwake? Ana uwazi? Ukihoji kitu wewe makorokoroni huonekani kabisa, *this typical* of Paul Kagame tumeshakwenda sote tunasoma tunasikia. Sasa Dkt. Shein hana *trend* hiyo. Yeye anawaamini mawaziri wake anaamini mihimili mitatu hii iende kila mmoja na mtizamo wake, Baraza la Wawakilishi liende upande wake, Mahkama iende upande wake na *Executive* iwe inaenda upande wake, lakini kila mmoja hawezi kufanya kazi peke

yake lazima tushirikiane mafya matatu haya hilo ndio suala la msingi sana. Kwa hivyo mimi kwa kwetu hapa Mhe. Abdalla kama hu-*perform* mimi nakuja na bastola yangu Chonga kule ninakupiga, tutakumalizeni!

Kwa hivyo, mimi nataka kusema Rais wetu makini na yeye anapenda sana kubadilishana mawazo kum-*consult* mpaka tunafikia, tunatumia vikao tunakesha mpaka saa nane kutafuta suluhisho ya matatizo, kuzungumza, unapozungumza ndio unapata suluhisho, usipozungumza tena hapo huoni muelekeo. Na uongo walioharibu labda si uzuri kusema waliokuwa wameharibu hawapo, tunawajua, tunawajua hawapo.

Mhe. Farida Amour Mohammed, nafasi maalum za wanawake tunakushukuru sana. Tunakushukuru sana, naomba niseme, nishasema mara nyingi sana suala hili la mishahara hewa. Mishahara hewa kazi ile aliyeagiza ni Mhe. Rais mwenyewe, kwa hiyo kazi imefanywa kapelekewa Mhe. Rais. Bahati mbaya sana Mheshimiwa lazima niliseme hili kuna baadhi ya Waheshimiwa wanakwenda kwa watendaji wetu wa *CAG* kuwa-*harass* wawape ripoti ile.

Tuna ushahidi kamili wanawa-*harass* wawape ripoti, kwa kweli tusiende hivyo, kwanza ile Ofisi ya *CAG* ni *independent* haitakiwi iingiliwe ingiliwe. Lakini leo Mwakilishi anapokwenda kutumia cheo chake kuwatisha wale haipendezi, haipendezi kabisa.

Ningeomba sana Mhe. Naibu Spika hili nakuripotia rasmi kwamba lazima tuwe na *discipline* ya utendaji kuwaendea watendaji wadogo wadogo ukawatisha wakupe ripoti, wakupe hiki, hiyo sivyo, sisi mawaziri tupo ndio tunaobeba dhima twambieni sisi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi nyumba ina mmong'onyoko mkubwa Mkoani tumesikia, lakini kama nilivyosema tunayafanya yote ya kwanza yale madogo madogo ambayo tunaweza kusaidia hivi sasa wenyewe. Lakini pili hilo la kuandika mradi na umetoa mfano ya Bwefumu kule, Mkokotoni kote huko tunashukuru tutajitahidi.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kwa kweli tunakushukuru sana, tunakushukuru sana kwa maelezo yako ya kina kabisa uliyoyaeleza na nataka kusema tu sisi wewe kama Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi na sisi kama wizara, sisi tuko pamoja kusikiliza maelekezo, mwelekeo ili tuone hatua ya nchi yetu inapiga hatua, tuko *very flexible* wakati wowote tushauriane, tuelekezane, tuone kwamba ile *spirit* ya Serikali ya Umoja wa Kimataifa irudi, iwepo tupate *the way forward.*

Mhe. Naibu Spika, kwa haya sasa niseme machache naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais):** Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kutoa ufafanuzi wa baadhi ya masuala ambayo yamejitokeza katika uwasilishaji wa utekelezaji wa maagizo ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama hivi ifuatavyo:

Napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kumi na sita (16) ambao wamepata nafasi ya kuweza kuchangia juu ya utekelezaji ambao tumeuwasilisha. Na naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia taarifa ya utekelezaji nao ni:

1. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman ambaye alisoma kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Salim Abdalla Hamad
5. Mhe. Salma Mohammed Ali
6. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
7. Mhe. Ali Salum Haji
8. Mhe. Hamad Masoud Hamad
9. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
10. Mhe. Mussa Ali Hassan
11. Mhe. Hija Hassan Hija
12. Mhe. Marina Joel Thomas
13. Mhe. Mohammed Haji Khalid

14. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
15. Mhe. Farida Amour Mohammed
16. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, na wa mwisho alikuwa ni
17. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Naibu Spika, michango mingi ambayo imetoka kwa Waheshimiwa mbali mbali juu ya utekelezaji wengine walikuwa wanakwenda kwenye ripoti ya kamati ya mwaka 2014/2015, lakini sisi tulijiandaa na maagizo na ushauri na maoni ambayo yalitoka kwenye ripoti ya mwaka 2013/2014. Na kwa sababu tunao muda kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Baraza wa kuwasilisha utekelezaji wa maagizo, maoni na ushauri uliotolewa na kamati kwenye ripoti hii ambayo Mwenyekiti ameiwasilisha mwaka huu, naomba yale yote tufuate utaratibu ambao tumejiwekea na mimi nijikite zaidi katika yale ambayo yanahusu ripoti ya mwaka uliopita.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, pale watakapoona mengine sikuyajibu wajue kwamba nimeyaacha kwa sababu utaratibu wetu tuliojiwekea ni kujibu yale yaliyotokana na ripoti ya mwaka 2013/2014 na sio mwaka 2014/2015. Nitaomba radhi sana utaratibu tumejiwekea wenyewe kama Baraza la Wawakilishi utaratibu huo tuufuate, na tujikumbushe katika kutoa maoni na michango hiyo.

Mhe. Naibu Spika, yako mengi ambayo yamezunguzwa na Wajumbe wengi kwa pamoja tutajaribu sana kutoa ufafanuzi wa masuala hayo na nitajikita katika hoja zaidi za kiutendaji kuliko maeneo mengine.

Tukianza na Ofisi ya Faragha kuhusiana na gari kwa ajili ya matumizi ya Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais. Hili jambo linaonekana baadhi ya Wajumbe wamelielewa na baadhi ya Wajumbe walikuwa hawakulielewa. Nataka niseme ofisi zote mbili, Ofisi ya Makamu wa Kwanza na Ofisi ya Makamu wa Pili kila moja imejibu na kutekeleza agizo ambalo ama ushauri waliopewa na kamati katika ripoti iliyopita.

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tumejibu suala linalohusu gari kwa ajili ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa maana gari la Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kule Kisiwani Pemba. Kwa hiyo, hatugongani lugha, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imezungumzia suala la gari ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tumezungumzia magari ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa maana ya Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais ndicho tulichokiripoti hapa. Na alichokiripoti mwenzangu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni gari inayohusu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kule Kisiwani Pemba. Kwa hiyo, napenda niseme kwamba serikali imeweza kutimiza kwa kutekeleza ushauri ama niite maoni, ama niite maagizo kuhusu eneo hili la kuwapatia viongozi wakuu wa Kitaifa magari mawili kule Kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, hoja ilikuwa inahusiana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia uliotokea huko Kizimkazi kama ulivyoelezwa na baadhi ya Waheshimiwa wengi.

Mhe. Naibu Spika, serikali itaendelea kulifuatilia suala hili kwa umakini kwa kushirikiana na taasisi husika ili kuhakikisha kuwa inashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa. Aidha, serikali itaendelea kuweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha kuwa vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia unadhibitiwa na unakomeshwa hapa Zanzibar.

Hoja kuhusiana na migogoro ya ardhi. Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaratibu na kufuatilia shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ushauri wa uundwaji wa kamati ya kumsaidia Makamu wa Pili wa Rais juu ya migogoro ya ardhi yeye mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameusikia, na endapo ataona ipo haja ya kufanya hivyo yeye mwenyewe atatoa maamuzi juu ya ushauri au maelekezo ambayo yametolewa.

Hoja kuhusiana na watendaji na wataalamu waliopelekwa kwenye masomo katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Serikali imepeleka vijana 30 kama tulivyosema kwenye ripoti yetu kwa mafunzo ya muda mrefu ya mafuta na gesi asilia chini ya udhamini wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Na kwa nini serikali imefanya hivyo? Imetoa *priority* kwa ajili ya kuwafunza vijana hawa kwa kuelewa kwamba sekta hii ni mpya na ni ngeni kwetu, kwa hiyo ni lazima tujiandae kuweza kuwafundisha vijana wetu ili wawe na utaalamu wa kuelewa sekta hii, lakini serikali imelifanya hili kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuwapeleka hao vijana 30.

Aidha, watendaji na wataalamu wa taasisi husika wamekuwa na utaratibu wa kufanya ziara ya mafunzo na kubadilisha uzoefu katika taasisi zinazohusiana na mafuta na gesi za ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuongeza ujuzi na uzoefu wa usimamizi wa masuala yanayohusiana na sekta hii.

Hoja nyengine ilikuwa ni kuhusiana na utendaji wa Mamlaka ya Maji (*ZAWA*). Ushauri juu ya serikali inalijua na tayari suala hili juu ya kadhia ambayo ipo. Serikali kwa ujumla inalijua suala hili na tayari imechukua hatua mbali mbali za kulipatia ufumbuzi kwa kushirikiana na wizara husika.

Miongoni mwa hatua ambazo zimechukuliwa hivi karibu wenzetu wa *ZECO* waliamua kuweka utaratibu wa kuweka mita za TUKUZA kwenye vianzio vyote au kwenye visima vyote vya maji. Sasa serikali imeamua mita hizo za TUKUZA zote ziondoshwe, na zimeshaondoshwa katika vituo vyote vya maji. Hili lilikuwa ni moja kati ya sababu iliyokuwa inasababisha baadhi ya maeneo kukosa maji, kwa sababu utaratibu wa TUKUZA ni kwamba unatakiwa ulipie ili kile kisima kiweze kufanya kazi. Serikali kwa kuelewa umuhimu na kuwajali wananchi wake imeamua kuondosha mita za TUKUZA na imeamua deni lote lilokuwa linadaiwa *ZAWA* la siku za nyuma basi serikali ilibebe na *ZAWA* waanze na malipo ya madeni mapya ambayo yatatumika. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba baada ya hatua hizo zilizochukuliwa na serikali basi tatizo hili linaweza likatatuka kwa asilimia kubwa sana.

Hoja kuhusiana na idadi ya skuli kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita ambalo limejitokeza kama kwamba si kweli. Serikali ilikusudia kuzitaja skuli hizi kwa namba ambayo imejitokeza. Unaposema sekondari maana yake ni kuanzia *form one* mpaka kidato cha sita, hatukukusudia kuzungumzia suala la kidato cha sita peke yake. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe waelewe ufahamu wa maelezo ambayo yametolewa na serikali kwamba tumesema hivyo. Na idadi hiyo ambayo tumeitaja ndio ilivyo kwamba kuanzia skuli zote za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha sita ilikuwa ina maana hiyo. Kwa hiyo, si kwamba tumedanganya au tumesema uongo, lakini skuli zenyewe zilizokusudiwa zilikuwa ni hizo.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa, hoja inayohusiana na ajali ya *MV. Spice Islander.*

Mhe. Naibu Spika, kama tulivyosema serikali iliwapatia fedha kwa utaratibu maalum uliowekwa wananchi wote waliofikiwa na maafa kufiwa na ndugu na jamaa zao katika ajali ya *MV. Spice Islander* ambazo walielezwa kuwa zitawasaidia katika huduma mbali mbali ikiwemo huduma za elimu kwa watoto waliofiwa na wazazi wao. Na kama nilivyosema bahati nzuri mimi nilibahatika kuwemo kwenye ile kamati iliyokuwa ikiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais kuzungumza na wahusika wote miongoni mwa mambo ambayo yalielezwa na serikali ni juu ya utaratibu mzima wa fedha zinavyotumiwa, zilizotolewa na matumizi yake na baadae wao wafanye nini kwa ajili ya kufuata utaratibu mwengine ambao tumeuzungumza kwenye ripoti yetu. Bado serikali inasisitiza kuhusu suala la ulipaji wa fidia, serikali inasisitiza kwamba suala hili ni la wahusika wenyewe kudai fidia hizo kwa wamiliki wa meli hiyo kwa mujibu wa sheria za nchi na sheria za kimataifa.

Hoja kuhusiana na serikali kuwa na vyombo vya kukabiliana na maafa na imejiandaa kiasi gani kukabiliana na majanga na maafa. Kwenye ripoti yetu tumeeleza vizuri ni kwa jinsi gani tumejiandaa kwa kushirikiana na mashirika ya ndani na nje, ya kitaifa na kimataifa na serikali yenyewe kupitia bajeti yake imejiandaa vipi, tumejieleza vizuri.

Serikali kupitia taasisi zinazohusiana na majanga na maafa zinaendelea kutoa huduma za kukabiliana na maafa kila yanapotokezea kwa kutumia vifaa na vyombo vilivyopo katika taasisi hizi. Hata hivyo, kuna changamoto kubwa ya upungufu wa vifaa vya kutosha na vya kisasa vya kukabiliana na maafa. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Fedha inaendelea kuomba miradi ya upatikanaji wa vifaa hivyo kwa lengo la kuijengea uwezo Idara ya Kukabiliana na Maafa baharini, angani na nchi kavu.

Kama nilivyosema kwamba katika eneo hili la majanga na maafa si Idara ya Kukabiliana na Maafa tu ndio yenye jukumu hili, lakini kuna taasisi mbali mbali kwa upande wake nazo zitakuwa zina jukumu la kuweza kutafuta zana na vitendea kazi kwa ajili ya kukabiliana na maafa kama vile tulivyosema. Kwa mfano, Idara ya *KMKM*, Idara ya Zimamoto na taasisi nyengine kadha wa kadha ambazo zimo ndani na ziko chini ya usimamizi wa serikali kwa kushirikiana na idara hii basi zimejiandaa vya kutosha kwa ajili ya kukabiliana na kadhia hii.

Hoja kuhusiana na suala la Mhe. Spika kuhamia kwenye nyumba. Hii ni hoja ambayo inajitokeza kila mara bahati nzuri hata mwaka jana nilikuwa mimi nakaimu kujibu hoja hii, na mwaka huu ime-*happen* kwamba ni mimi nakaimu najibu hoja hii.

Lakini serikali imeeleza kwamba suala hili limeulizwa sana na wajumbe tumeshatoa majibu yake kwamba ni lengo la kujengwa nyumba ile ni kwa makaazi ya Mhe. Spika na si vyenginevyo. Kama tulivyoeleza mwanzo kwenye majibu yetu kwamba eneo lile linakabiliwa na tatizo la upatikanaji wa maji, na Ofisi ya Baraza imechimba visima mara tatu lakini juhudi za kupata maji katika visima hivyo hazijafanikiwa. Ofisi ya Baraza imekubaliana na Mamlaka ya Maji *ZAWA* kuipatia maji nyumba hiyo kupitia mradi wa usambazaji maji ambao unatarajiwa kukamilika hivi karibuni katika eneo hilo. Na mara tu utakapokamilika mradi huo basi Mhe. Spika atahamia kwenye nyumba hiyo.

Hoja kuhusiana na matumizi ya milango ya kuingilia na kutokea kwenye jengo la Ofisi ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa kutumia mlango mmoja tu kwa kuingia na kutoka kwenye jengo la ofisi ni kwa ajili ya usalama. Madhumuni makubwa ni kuhakikisha wale wote wanaoingia wanapita kwenye *machine* ya ukaguzi kwa vile mashine iliyopo sasa ni moja. Utaratibu ni kupitia kwenye mlango ambapo mashine hiyo ipo. Tunawaomba Waheshimiwa watuvumilie kwani ofisi kupitia vyombo husika vya usalama ina mpango wa kuweka mashine nyengine mbili za ukaguzi ambazo zitawekwa kwenye milango mingine.

Hata hivyo, endapo dharura itatokea utaratibu umewekwa wa kuwawezesha kufungua milango mingine kwa haraka. Nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba funguo za milango hiyo wanazo ma-*sergeant at arms* wa Baraza hili ikitokezea dharura wao watakimbia kuweza kwenda kufungua milango hiyo, lakini Mwenyezi Mungu atupishie mbali.

Ni matumaini yetu pengine wakati wa kikao cha bajeti mashine hizi zitakuwa zimefika ili kuondosha usumbufu ambao umewakabili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza na watumishi wa Baraza kwa kipindi hiki.

Mhe. Naibu Spika, kwa jumla hayo ni mambo ambayo yalijitokeza kama nilivyosema, yale mengine tumeambiwa hapa kwamba pengine inaonekana maagizo tuliyoyajibu ni machache kuliko yale ambayo tumeagizwa, lakini tuelewe mfumo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, mfumo wa ripoti za kamati kuna maagizo, ushauri, maoni; sina haja ya kutoa tafsiri sasa hivi ya maagizo, maagizo maana yake utekeleze, ushauri maana yake na wewe lazima uende ukautafakari kuona kwamba ushauri uliopewa unafaa au haufai. Maoni vile vile unatakiwa uyazingatie ukiyaona yanafaa unapaswa kuja kuyatolea ufafanuzi.

Kwa hiyo, kuwa na ushauri, maagizo na maoni arubaini na zaidi kama alivyoyataja Mheshimiwa aliyetoa maoni ni kwamba tumejitahidi kujibu hayo thalathini na zaidi, kwa maana baadhi ya ushauri mwengine ambao tumeshauriwa ama unahitaji muda zaidi wa kuweza kuufanyia kazi, ama hautekelezeki, na katika kamati zetu mambo kama hayo tunapokwenda kukaa na wizara mbali mbali tunapata majibu pale tunapofanya majumuisho.

Sasa na utaratibu pia wa ripoti kama wa yale maagizo kujirejea rejea na sisi serikali tutaendelea kurejea rejea, ama kuanzia sasa labda tukimaliza mkutano huu tukubaliane kimsingi na kamati yepi ambayo mumekuja wizarani tukakwambieni kwamba haya yametekelezwa. Kwa hiyo na ripoti za kamati pia zilitakiwa zitambue ule utekelezaji ambao umeripotiwa kwamba umetekelezwa, *otherwise* ni kweli yatakuwa yayo kwa yayo; yanakuwa yayo kwa yao kwa sababu na ripoti za kamati nazo ni yayo kwa yayo. Kwa hiyo, tubadilishe mfumo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane kwa sababu kuna utata kidogo katika masuala haya, sioni kama kuna tatizo kati ya maoni yanayotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi na Serikali. Kwa sababu hakuna ugomvi wala hakuna kumtafuta mtu katika hili.

Waheshimiwa Wajumbe wanatoa ushauri, maoni na maagizo kwa faida ya serikali na wananchi kwa jumla na serikali hii ni ya wananchi imechaguliwa na wananchi inapaswa kuzingatia haya. Kwa hiyo, mimi nadhani hapa tunakosana pahala padogo sana, inawezekana pengine ama hatujaelewa namna tunavyotakiwa tujibu haya maagizo, ushauri na maoni tunatakiwa tufanye vipi. Kwa hiyo, nahisi iko haja ya kukaa pamoja kati ya serikali na Baraza kuona *modality* gani inafaa ya kuweza kujibu hizi hoja zinazokuja hapa mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kila mmoja ana uelewa wake, nataka niseme ndani ya Baraza hili wako Wajumbe wanatoa maoni yao vizuri sana na wanakwenda kwenye hoja, lakini wako Wajumbe ambao wanatoa maoni hujui wanachangia bajeti, hujui wanachangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Kwa hiyo, ni vizuri Waheshimiwa Wajumbe sote sisi tunajenga nyumba moja, tunajenga nyumba ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, kwa hiyo kama kuna mambo hatujaelewana ni vizuri sasa serikali na Baraza la Wawakilishi litafute *modality* ya kuweza kujibu hizi hoja na kuweza kamati kuandika zile ripoti zake, vyenginevyo kweli kila siku tukija hapa tutaambizana kwamba mambo yanajirejea, mambo yayo kwa yayo ni kwa sababu ya *modality* ya utaratibu uliopo.

Kwa hiyo, mimi naona hakuna tatizo kubwa wala hakuna haja ya kusema mpaka mishipa ya shingo ikatuna, ni jambo la kuweza sisi kuelewana, sote tunajenga nyumba moja, tuelezane kama kuna tatizo kwa upande wa serikali tuambiwe tatizo lenu hili, lakini na sisi ni vizuri tukabainisha matatizo ambayo tunayaona yanatukata sisi serikali katika kujibu baadhi ya mambo ambayo yanajitokeza kwenye ripoti za kamati.

Mhe. Naibu Spika, yako mengine ambayo yamechangiwa kwa mfano suala la kumfanya marehemu Mzee Abeid Amani Karume kama jemedari wa Mapinduzi kuwa baba wa Taifa. Sasa hili ni jambo ambalo linahitaji mazingatio maalum, lakini kimsingi ni jambo zuri na kwa kiasi fulani nahisi bado tunavyohisi kwamba tumejaribu kumuenzi na tukiweza kukamilisha yale ambayo tumekusudia katika kumuenzi serikali ikiweza kuyakamilisha yale nina hakika hilo jambo litakuwepo. Lakini katika lile wazo ambalo limetolewa linahitaji mashauriano mazuri zaidi hasa kulingana na mfumo wetu ulivyo. Baada ya kwisha kusema hayo nataka niwashukuru sana tena na tena.

Suala la Makamu wa Pili wa Rais kuwajibika au kujiuzulu. Nadhani yeye mwenyewe amesikia na Mhe. Rais amesikia, kwa hiyo niwaachie wenyewe hilo wanaweza wakalitoa ufafanuzi wao, mimi kwangu kulitolea ufafanuzi ni mdogo sana. Mhe. Rais kalisikia sana na mwenyewe alikuwepo kalisikia kwa hiyo naomba niishie hapo Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa vyote vilivyomo duniani na majini kwa kutujaalia kutuamsha tukiwa wazima katika siku hii ya leo, tukiendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi wa Zanzibar tukiwa katika hali ya uzima na afya.

Pili, naomba nikushukuru na wewe binafsi kwa kunipa tena nafasi hii ya kutoa ufafanuzi juu ya mawasilisho yangu juu ya utekelezaji wa maagizo na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kuipitia ripoti hiyo ya utekelezaji na kuweza kuuliza na kutaka ufafanuzi na wengine kutoa maoni yao mengine tena kutokana na ripoti hiyo. Niahidi kwamba ushauri na maoni yao tunayachukua kama Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na tutaendelea kuyazingatia na kuyafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwataje sasa wale ambao walipata fursa ya kuchangia katika ripoti hii na kuigusa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika michango hiyo.

1. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Salim Abdalla Hamad
5. Mhe. Salma Mohammed Ali
6. Mhe. Hamad Masoud Hamad
7. Mhe. Marina Joel Thomas
8. Mhe. Mohammed Haji Khalid
9. Mhe. Mussa Ali Hassan
10. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
11. Mhe. Farida Amour Mohammed
12. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, na

13. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Mhe. Naibu Spika, naomba Wajumbe wanivumilie kwamba nitajibu hoja zilizochangiwa kwa pamoja isipokuwa tu kama kutakuwa na hoja ambayo imechangiwa na Mjumbe peke yake nitafanya hivyo katika kujibu hoja hiyo.

La kwanza, naomba nianze kwa kuondoa sintofahamu iliyopo juu ya kwamba tulichotakiwa kukileta ndani ya Baraza la Wawakilishi hakikukamilika, hili lilichangiwa zaidi na Mhe. Ismail Jussa Ladhu lakini vile vile na Mhe. Hamad Masoud.

Mhe. Naibu Spika, barua tuliyopokea kutoka kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi ilitutaka maagizo ya kamati ambayo yamo katika kitabu kile cha ripoti za kamati cha mwaka 2013/14 na tulifanya hivyo mwaka uliopita kwa kujibu maagizo. Hicho ndicho ambacho tulichotakiwa kufanya na ni kwa sababu kama walivyoeleza mawaziri wenzangu waliotangulia ambao wanasimamiwa na kamati hii ya kudumu. Maoni na ushauri kikawaida huwa tunayamaliza wakati wanapokuwa na ziara zao siku ya majumuisho, yale huwa tunayamaliza siku hiyo. Kwa hiyo kile kinacholetwa kwetu kama maagizo ndicho ambacho Katibu wa Baraza la Wawakilishi ametutaka tuje tulete taarifa hiyo na ndicho tulichotekeleza.

Mhe. Naibu Spika, na mimi narudia kama kuna mapungufu katika hilo hatukulifanya kwa makusudi wala sio kwamba serikali haiko makini, hilo tumelifanya kwa maelekezo ambayo tumeyapokea na bado nafasi ipo ya kukaa pamoja Baraza na serikali ili tukaelekezana vyema hasa ripoti yenyewe inatakiwa iweje.

La pili katika hayo, hususan kwenye ripoti yangu mimi maagizo ambayo yalitolewa mwaka 2013 na mwaka 2014 yamejirudia maagizo hayo ya kamati katika ripoti ya mwaka 2014/2015. Mimi sishangai sana kwa sababu leo hii ndio unajibu maagizo ya kamati, ndio unaleta majibu kwa yale maagizo yaliyopita. Sasa inayumkini labda kamati haijapata majibu lakini utaratibu tuliopangiwa na Baraza ni kuja kujibu hii leo, yale yamejirudia tena vile vile likiongezeka agizo moja tu ambalo ni jipya.

Kwa hiyo, hapa pia kama Baraza na Serikali inabidi tukae vizuri tutafakari wakati gani majibu ya maagizo yataletwa ili kamati zisiwe zinarudia kuuliza maswali au maagizo ambayo sisi leo ndio tunaleta majibu yake tayari tumeshaandikiwa tena katika ripoti ya mwaka 2014/2015. Nahisi hapa tunahitaji kukaa vizuri ili suala letu liende vyema.

Mhe. Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huo katika ofisi yangu mambo makubwa yaliyoguswa ni matatu. La kwanza ni suala zima la Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (*ZIPA*) kuzingatia kufanya tathmini ya athari ya kimazingira kabla ya mradi wowote kupewa kibali cha kuweza kufanya uwekezaji wake ambao unahitaji kufanywa.

Hili Serikali tumeliona na katika sheria yetu mpya sasa hivi tuna chombo ambacho kitakuwa kinasimamia kuhakikisha kwamba wadau wote wanatekeleza masharti ya sheria hiyo, mojawapo ni kuhakikisha kwamba tathmini ya athari za kimazingira zinatekelezwa kabla ya mradi wowote kuweza kutekelezwa au kupewa kibali cha kuanza utekelezaji.

Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kipindi cha Baraza kilichopita tulipitisha sheria mpya ya usimamizi wa mazingira, ndani ya sheria hiyo kunatakiwa kuundwa chombo cha usimamizi wa mazingira Zanzibar ambacho ndicho kitakachokuwa na kazi ya kusimamia utekelezaji. Idara ya Mazingira nayo itabakia na shughuli zake za kusimamia sera na mambo ya kiuendeshaji yanayohusu suala zima la kimazingira. Ni imani yangu kwamba kuanzia sasa suala hili sio *ZIPA* tu, lakini mdau mwengine yoyote kuweza kutekeleza mradi bila ya kufanya tathmini ya athari za kimazingira litasita na usimamizi utakuwa bora zaidi. Naomba nilijibu hivyo.

Suala la pili lililoguswa ni kuhusiana na suala zima la uratibu juu ya shughuli za dawa za kulevya, na naomba nianze na Mhe. Marina Joel Thomas ambaye yeye alieleza kwamba haoni sababu kwa nini Serikali i-*invest* katika kujenga kituo cha kurekebisha tabia kwa vijana ambao wameamua kuacha dawa za kulevya badala ya kujikita katika kuzuia uingizwaji na usambazwaji wa dawa za kulevya ndani ya visiwa vyetu.

Naomba nitoe elimu kidogo kwa Mhe. Marina Joel lakini pia kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba, tunapozungumzia suala zima la udhibiti wa kuzuia uingizwaji wa dawa za kulevya tunazungumzia mambo

matatu; tunazungumzia kinga, tiba na marekebisho kwa walioathirika na madawa ya kulevya. Lakini pia linazungumziwa suala zima la kupambana na uingizwaji na usambazaji wa dawa za kulevya ndani ya visiwa vyetu.

Masuala haya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni mratibu Tume ya Udhibiti na Kuratibu suala la madawa. Mapambano dhidi ya dawa za kulevya kazi yake kubwa ni kuhakikisha kwamba masuala haya kila mdau anafanya wajibu wake ili suala zima la mapambano dhidi ya dawa za kulevya liweze kufanikiwa. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wasilitizame suala la dawa za kulevya upande mmoja.

Mhe. Naibu Spika, hata kama leo hii ikawa hakuna dawa ya kulevya hata moja ambayo itaingia ndani ya visiwa vyetu tayari tuna vijana wetu, watoto wetu, ndugu zetu ambao wameshaathirika na dawa za kulevya. Na wao kama wananchi wa Taifa hili wanapaswa kupewa huduma ya afya. Mtu yeyote ambaye ameathirika na madawa ya kulevya huyo anahesabiwa kuwa ni mgonjwa na anahitaji utibabu. Kwa hivyo, serikali ina wajibu vile vile wa kuwashughulikia sehemu hii ya jamii ya vijana wetu ambao tayari wameshaathirika na dawa za kulevya, na ndipo tukaona sasa tusitegemee moja kwa moja jitihada za taasisi ambazo zinajitegemea zilizoanzisha *Sober Houses,* lakini serikali yenyewe kwa kuwa ina jukumu la kutoa huduma kwa wananchi wake wote nayo iweze kuanzisha kituo cha *Sober House* chake wenyewe ambacho tutakiita Kituo cha Marekebisho ambacho kinategemewa kujengwa huko Kidimni ili kushughulikia vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa nijibu upande wa pili ambao nao uliguswa na Waheshimiwa wengi, suala la udhibiti. Mhe. Naibu Spika, suala la udhibiti wa usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya si suala ambalo linaweza kumalizwa kwa taasisi moja, yaani Tume ya Udhibiti na Uratibu wa Mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Hili ni suala la taasisi zote na jamii ya Wazanzibari kwa ujumla na ni suala gumu, suala ambalo linamuhusisha kila mmoja wetu na si kweli kwamba serikali inawalinda au inawaficha wasambazaji wa dawa.
Mhe. Naibu Spika, sheria tulipitisha hapa ndani ya Baraza lako Tukufu na tulizidi kuifanyia marekebisho ili kuipa nguvu kwa kuzungumza kwamba hivi sasa mtu yeyote atakayepatikana na akiwa na dawa za kulevya basi yeye ni mkosa chini ya sheria na atatiwa hatiani kwa mujibu wa sheria inavyozungumza.

Tulirekebisha kipengele kilichosema kwamba atakayekamatwa na dawa za kulevya ikathibitika kwamba anazisafirisha tukaona kwamba *loophole* kwamba wengine wanakamatwa na dawa lakini anasema hakuwa katika *process* ya kuzishafirisha ikawa anashitakiwa kwa kifungu chengine.

Kwa hiyo, serikali imejitajidi sana kuirekebisha sheria kuwabana wahalifu ambao wanahusika na usafirishaji wa dawa za kulevya. Na Waheshimiwa Wajumbe hichi mnachokisikia sasa mara kwa mara kikitangazwa kwenye vyombo vya habari kwamba kiasi fulani cha dawa kimekamatwa *Airport*, kiasi fulani cha dawa kimekamatwa Bandarini lakini pia kwa vijana wetu mmoja mmoja anayekamatwa na kete basi ndio jitihada zenyewe za serikali katika kupambana na dawa za kulevya.

Huko nyuma, usafirishaji ulikuwepo na usambazaji ulikuwepo, lakini hakukuwa na udhibiti wa kuweza kukamatwa kiasi ambacho hivi sasa kimefanyika. Kwa hiyo, yapo mafanikio lakini bado mapambano haya ni vita vikali, vita ambavyo vinahusisha ndani yake watu wenye fedha nyingi watu wanaohusika na dawa za kulevya ambao wako tayari kuhonga kwa mamilioni kuweza kukimbia sheria.

Kwa hiyo, wito wangu ni kwamba wadau wote ambao wanashughulika na suala zima la udhibiti wa dawa za kulevya ambao kama Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya mara kwa mara inawakutanisha ili kuona kwamba kila mmoja anatimiza wajibu wake kwa taasisi ambazo zinahusika na masuala ya Uwanja wa ndege, masuala ya Bandari, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Polisi, Mahkama, Muendesha Mashtaka, Taasisi ya *TRA*, *ZRB,* Mkemia Mkuu wote hao ni wadau katika suala hili la mapambano dhidi ya dawa la kulevya.

Tume ya uratibu inafanya kazi kubwa ya kuwakutanisha na kuweza kuona wana matatizo gani katika maeneo yao ili kusaidia kwa pamoja kuweza kuyatatua ili tuweze kupata mafanikio zaidi.

Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na wananchi kwa ujumla, hawa wadogo wadogo wanaosambaza na pengine wengine wanaosafirisha ni wenzetu tunaokaa nao katika mitaa na wengine tunawafahamu lakini inapobidi sasa kuja kumtaja na kutoa ushahidi kuna suala zima la muhali kwa wananchi wa visiwa vyetu, na suala lolote haliwezi kutekelezwa bila ya kufuata sheria na sheria inahitaji kuwepo kwa ushahidi. Kwa hivyo, wito wangu ni kwamba yanapojitokeza masuala haya kwa pamoja tuwe tayari kutoa ushahidi ili wahalifu waweze kutiwa hatiani.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililozungumzwa sana ni uharibifu wa mazingira. Kila mmoja alimeliongea kwa aina yake kama ambavyo sisi tunalieleza na changamoto zake wako waliozungumzia juu ya suala zima la ukataji wa mikoko ambalo pia na sisi tunalipigia mbio na kilipigia kelele kwamba wananchi waachane na utaratibu huo. Kubwa zaidi Waheshimuiwa Wawakilishi wale ambao tunaishi katika ukanda wa pwani tushirikiane na wananchi ambao tunao katika ukanda wa pwani tuwashajihishe katika kupanda mikoko hii na kuirejesha hali iwe njema.

Mhe. Naibu Spika, kidogo haifurahishi kwamba Wawakilishi wengi wanaokaa katika ukanda wa pwani hawashirikiani vyema na wananchi wao ili kuwapa *support* katika shughuli wanayofanya ya kupanda mikoko na kutoa elimu ya mazingira. Naomba sana tushirikiane na wananchi wetu katika kulitekeleza hilo, tuondokane na ukataji wa mikoko ambayo imo katika ukanda wa pwani ili kuepusha maji ya bahari kuvamia katika ardhi zetu za kilimo, mojawapo ya sababu ya maji ya bahari kuvamia maeneo yetu ni kuondoka kwa mikoko hiyo, uchimbaji ovyo wa mchanga ambao nao umekuwa ni tatizo kubwa na kuviacha visiwa vyetu vikiwa katika hali mbaya.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini sana baada ya kutunga sheria yetu hii mpya lakini hususan ikaunda ndani yake chombo hichi cha ushimamizi wa mazingira hali sasa itatengamaa kwa sababu kuna chombo maalum sasa cha usimamizi kuona kwamba kwa mujibu wa sheria umeambiwa eneo fulani ndilo linalohitajika kuchimba mchanga basi hakuna mwananchi mwengine atakayekwenda kufanya uharibifu katika maeneo mengine. Lakini hata wale walioruhusiwa kuchimba mchanga watauchimba kwa utaratibu ambao umewekwa na Idara ya Mazingira na Maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Naibu Spika, natumai hali itakuwa ni nzuri lakini pia naomba Washimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wote tushirikiane katika kuona kwamba tunashirikiana na wananchi wetu kukemea hali hii ya uharibifu wa mazingira. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine tunapata vikwazo wakati idara inapambana na uharibifu wa mazingira baadhi ya viongozi wanasema wananchi wetu ndio wanapopatia kipato chao. Kwa hiyo, tuwaachie waendelee hawana sehemu ya kupatia kipato.

Mhe. Naibu Spika, naomba pamoja na kutaka wananchi wetu wawe na kipato lakini turuhusu shughuli ambazo hazitaiharibu nchi yetu kwa ajili ya kukaliwa na vizazi vijavyo. Kwa hiyo, shughuli za kipato ziendelee lakini uhifadhi ya mazingira ni muhimu sana katika shughuli zetu zote tunazozifanya.

Mhe. Naibu Spika, suala la gari Mhe. Waziri wa Nchi Idara Maalum alimelizungumzia vyema kwamba hakuna Waziri alisema uongo mawaziri wote wawili wamezungumza maneno ya kweli, kwamba Mheshimiwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili suala lililokuwa linazungumzwa lilikuwa ni suala la kiongozi mwenyewe, gari ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, ninachozungumza mimi ni suala la gari ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliyopo Pemba, na hili suala limerejewa katika maagizo ya kamati. Nioneshe masikitiko yangu tu kwamba ni kweli suala hili limekuwepo toka mwaka jana, lakini kutokana na uhaba wa fedha tunazoingiziwa suala hili tumeshindwa kulitekeleza, lakini tumeahidiwa na Wizara ya Fedha kwamba katika robo ya mwaka huu wa fedha fedha hizi zitakamilishwa ili tuweze kununua gari hiyo.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Salma Mohammed Ali aondokane na mawazo aliyokuwa nayo kwamba mawaziri wanalidanganya Baraza, naomba wawe makini sana wakati mawaziri wanapotoa ufafanuzi kusikiliza. Kwa sababu saa nyengine neno moja tu ndilo linaloleta tafauti katika maelezo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwajuma Faki Mdachi yeye alieleza kwamba tumeeleza katika suala namba 7 katika kujibu agizo namba 7 kwamba tumesema agizo hilo tumeliwasilisha katika taasisi husika. Mhe. Naibu Spika, ni kweli na taasisi husika hapo tumeitia ndani ya *bracket* ni *ZIPA* au Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi, kwa sababu suala hilo ambalo kamati imetuletea sisi, si suala ambalo taasisi yangu inahusika nalo. Lakini walilizungumza kwetu na sisi agizo hilo tumelipeleka kwenye taasisi inayohusika kama utaratibu ulivyo kwamba serikali inafanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ambayo nimeyatoa kijumla, naamini kwamba nimeweka vyema hoja na masuala mbali mbali ambayo yalihitaji ufafanuzi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusiana na Ripoti ya Utekelezaji wa maagizo kwa mwaka 2013/14. Naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe msitoke tunataka kuipokea hii taarifa na umebakia muda mdogo tu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma: (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na hatimae kutujaalia uzima na afya njema na uwezo wa kuondoka majumbani kwetu hadi katika jengo hili bila kushikiliwa. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu, na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Vile vile, nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kwa niaba ya Kamati kama sikuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza na sisi kamati kuja hapa mbele kutoa majumuisho kidogo kuhusiana na wachangiaji wa taarifa yetu hii. Kwa hivyo, kwa niaba ya Mwenyekiti wangu wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma na Wajumbe wote wa kamati, kwa hivyo nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja katika taarifa yetu. Kwa niaba ya Mwenyekiti, kwanza nianze na Wajumbe wa Kamati ni wale wale ambao aliwataja juzi pale Mhe. Shadya Mohammed Suleiman ndio wale wale Wajumbe hawajabadilika na makatibu ni wale wale.

Sasa utambuzi wa waliochangia, Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati napenda niwatambue wachangiaji 16 pamoja mawaziri 3.

Kwa hivyo, napenda kwanza niwataje hawa wachangiaji 16 ambao ni:-

(1) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

(2) Mhe. Ismail Jussa Ladhu

(3) Mhe. Salim Abdalla Hamad

(4) Mhe. Salma Mohammed Ali

(5) Mhe. Mohammedraza Hassanali

(6) Mhe. Ali Salum Haji

(7) Mhe. Hamad Masoud Hamad

(8) Mhe. Abdallah Mohamed Ali

(9) Mhe. Hija Hassan Hija

(10) Mhe. Marina Joel Thomas

(11) Mhe. Mohammed Haji Khalid

(12) Mhe. Mussa Ali Hassan

(13) Mhe. Abdalla Juma Abdalla

(14) Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

(15) Mhe. Farida Amour Mohammed

(16) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mawaziri 3 kwanza ni Mhe. Haji Omar Kheri ambaye jana aliwasilisha pale kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora na leo katoa ufafanuzi, vile vile napenda nimtambue Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, vile vile nimtambue Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji ambaye anatokea Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze na niwashukuru Mawaziri wote kwa kuweza kuangalia michango ya Wajumbe na kuitafakari na kuahidi kwamba michango ya kamati wameipokea, na wataendelea kuifanyia kazi. Kwa hivyo kwa niaba ya kamati napenda kuwapongeza mawaziri wote.

Sasa Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe, jicho moja halioni mwezi, huu ni usemi wa Kiswahili, halikadhalika kidole kimoja hakibanji chawa. Sisi taarifa yetu tuliyoleta ni kama mlivyoiona hiyo, na sisi tunafarijika sana kwa michango yenu, ambayo tukichanganya na taarifa zetu basi tunaweza kuisaidia sana Serikali, na yale mapungufu ambayo yamejitokeza katika taarifa zetu za kamati muone tu ni hiyo dhana ya kwamba jicho moja halioni mwezi hiyo ni sababu ya kwanza.

Sababu ya pili ni vikwazo vidogo vidogo tulivyokuwa tukikumbana navyo katika kazi zetu za kamati. Katika kazi za kamati Waheshimiwa tulilazimika wakati mwengine kwenda Dar es Salaam, nashukru nimesafirishwa kwenda Dar es Salaam, tulilazimika wakati mwengine katika kazi zetu za kamati kwenda katika kisiwa ambacho wakati wowote kutokana na mabadiliko ya tabia nchi nacho kikaendelea na kukumbwa na tatizo hili yaani kisiwa cha Matumbini.

Mhe. Naibu Spika, hiki kisiwa kiko Wilaya ya Mkoani hatukufika sisi na mambo ya kamati ndio yanamalizika malizika kile kisiwa wakati wowote nacho kinaweza kikaenda kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi, vile vile ni *safeguard* ya Kisiwa Panza ambacho kinakaa watu. Hichi kisiwa cha Matumbini hakikai watu, lakini ni *safeguard* ya mawimbi na mkondo wa Nungwi ambao unazuiwa na Matumbini kabla hayajafika Kisiwa Panza kule, ambako ukiona hicho Kisiwa Panza chenyewe hivi sasa tayari kinaendelea kuchukuliwa na maji.

Sasa ikiwa Matumbini hatukienzi hiki ambacho hakikai watu lakini kinaathirika sana, sasa wamehamia watu kule wanavunja miamba, wanabanja kokoto sisi tukataka twende kwa kweli Kamati ilishindwa kufika kutokana na usafiri, kwa sababu ilikuwa mawimbi makali na Serikali ilishindwa kutupatia boti ya KMKM sisi tukashindwa kwa vile vimashua pale.

Kwa hivyo, huko hatukufika lakini naomba Waheshimiwa kamati zijazo zikaona hiyo hali katika kuinusuru Matumbini na kukinusuru Kisiwa Panza chenye wakazi wasiopungua karibu elfu mbili kule, kwa hivyo, hiyo ndio miongoni mwa changamoto ambazo tulipambana nazo katika safari zetu hizo.

Mhe. Naibu Spika, michango yetu imezungumzia sana kiujumla jumla, nitatoa kiujumla matengenezo ya Ikulu ya Mkoani, ujenzi wa uzio wa Ikulu Bwejuu kule na vile vile Micheweni.

Waheshimiwa, ninaiomba Serikali katika hapa ifanye kazi, isikilize kilio chetu. Maraisi wetu ni binadamu na kule Ikulu ya Micheweni ni muhimu sana. Sisi katika miaka ya thamanini hivi, tulikuwa na msafara wa kiongozi wetu akitaka kuosha mikono na tulikuwa tunakwenda Kusini huku, basi ikabidi maskini kiongozi naye tupate shida kumpitisha pitisha katika vichochoro.

Sasa ikiwa mutaendelea kudharau ile Ikulu ya Micheweni basi itakuwa munadharau viongozi wetu, kwa sababu itakuwa ni jambo la aibu sana kwa Rais, hatusemi pale ni Dkt. Ali Mohamed Shein sasa, ni Rais. Kama ni Dkt. Shein tu anaweza kwenda kwa ndugu zake na jamaa zake na rafiki zake lakini Rais kwenda kumuazimia kwa Mkuu wa Wilaya, sijui kwa Sheha, haya ni matatizo. Hii ifanyieni maarifa mumalize lile tatizo.

Ikulu ya Mkoani niipongeze Serikali kwamba imefanya kazi nzuri kwa ile *renovation*. Imefanya *renovation*, imefanya *construction* ya jengo nzuri lakini kuna *retaining wall* unahitajika. Mmomonyoko mkubwa sana huku chini wakati ambapo wakati wowote inaweza ikachukua sehemu ya lile jengo jengine. Mimi ninadhani kuna haja sasa ya kwenda mukaona kwamba kunahitajika *retaining wall* ili kunusuru yale matatizo pale kwenye Ikulu yetu ya Mkoani.

Mhe. Naibu Spika, kuna ule mmomonyoko wa Ikulu ya Bwefum. Katika miaka ya nyuma pale Rais alikuwa akilala hasa pale, enzi ya Mzee Aboud Jumbe, ilikuwa wakati mwengine anapenda upepo wa *country side* ya kisiwa hiki, anakaa kule anamalizia *week end* kule. Lakini hivi sasa ukiangalia lile jengo limeshachukuliwa sana na maji mpaka baadhi ya maeneo yake yameshaanza kusombwa maeneo.

Sasa mimi ninadhani Serikali katika hapa ione umuhimu wa kuangalia ile kwa matendo na siyo kuchapa chapa maneno humu ndani, unaona wafanye kwa matendo. Unajua kula uhondo kunataka matendo, asiye matendo hula uvundo. Mimi ninadhani haya siyo maneno *as such*, haya ni maneno ya mwana falsafa mmoja muhimu sana katika nchi hii.

Fanyeni mambo kwa matendo na siyo kwa maneno Waheshimiwa ili wazanzibari wapate kula uhondo, tukiendelea kusema maneno tu basi sidhani kama tutafanya vizuri. Kwa hivyo, ile Ikulu inatakiwa ishughulikiwe. Ninawapongeza kwa Ikulu ya Kibweni kuifanya vizuri ile, halikadhalika kwa ule uzio ambao mumeanza kaskazini.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi ni taasisi muhimu sana kwa nchi zetu hizi. Ni *peace-making institution* ni taasisi ambayo inayoweza kuleta amani na utulivu katika nchi. Ikiwa itatunzwa vizuri na kufanya kazi zake vizuri Tume ya Uchaguzi, basi kwa kiasi kikubwa amani ya nchi itakuwepo na haitoharibika.

Lakini inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, kwamba Tume yetu ya Uchaguzi haipewi kipaumbele katika kufanya kazi zake. Ofisi hii yaani Kikatiba hii Tume inatakiwa iwe *impartial*, isipate maelekezo. Leo Ofisi za Wilaya za Tume ya Uchaguzi zimo katika majengo ya Serikali, majengo ya Mkuu wa Wilaya na Mkoa.

Sasa mimi ninaomba sana Mhe. Naibu Spika, muwafanyie maarifa wapate majengo yao, tena *well equipped* yale majengo. Kwa mfano ukiangalia lile jengo la Tume ya Uchaguzi ya Wilaya ya Chake-Chake lipo katika barabara, kijijumba tu kidogo kidogo, kilango kimoja, wakitokewa na moto hawana pa kukimbilia wale na wanapata maelekezo pengine kutoka *DC*, jambo ambalo ni *impartiality* inakosekana mara zote. Sasa ninadhani katika hili mujitahidi sana.

Mhe. Naibu Spika, nikija ule ukurasa wa tisa mpaka wa kumi kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais sehemu ya Uratibu pale, yale ni maneno ya kamati yetu. Kamati yetu ambayo ina wajumbe watatu kutoka CUF na wajumbe wanne kutoka Chama cha Mapinduzi. Ile ndiyo kauli ya kamati yetu. Kwa hivyo asitafutwe mchawi ni nani. Yaani ile ni kauli yetu sisi na asikamatwe huyu kasema hivi na vile. Mimi ninadhani Serikali iyatumie maelezo yetu kama kioo. Taarifa yetu itumike kama kioo, waangalie, halafu wajirekebishe na pasiwe pa kukamatana kamatana mchawi hapa.

Mhe. Naibu Spika, nilisema nitakwenda kijumla mambo yaliyoguswa sana mambo ya mazingira. Miradi hii kutofanyiwa ile tathmini ya kimazingira ni tatizo. Na wakati mwengine Waheshimiwa sisi huwa kamati yetu iliwahi kuzuia mradi mmoja usifanywe pale Makangale, ujenzi wa hoteli, jina la hoteli limenitoka lakini hoteli moja ilizuiwa na kamati wakati mimi bado siyo mjumbe wakati huo lakini ni kamati hii hii, kwamba mradi haujafanyiwa tathmini ya kimazingira lakini ikenda likanyooshewa mkono la Serikali mradi ukaendelea kujengwa na hivi sasa hoteli ile imejengwa mpaka baharini huku. Ni tatizo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mbali na uharibifu wa mazingira, ni tatizo. Kuna viumbe hai pale mbali ya kuharibika mazingira, kuna viumbe ambavyo vinapoteza maisha yake kwa kuendelea kuwachukulia ufukwe. Kwa mfano kasa. Mhe. Naibu Spika, kasa ni *marine organism* lakini ana *spend motografy* kwenye *marine* lakini *part of life* anakuja zake juu

kutaga mayai na kuzaa. Sasa akija pale anakutia pameshajengwa kuta la hoteli, hapana tena ufukwe, hana pa kuzaa. Matokeo yake viumbe hivi kasa vinaendelea kupotea siku hadi siku.

Kwa hivyo,  mbali na kutuharibia mazingira hii miradi ilivyokuwa hamuifanyii tathmini ya mazingira yanatuharibia mazingira pamoja na kutupotezea baadhi ya viumbe vilivyopo baharini na hata hivi viliopo huku juu, kwa sababu wengine hupenda kwenda kufanya mazungumzo katika *beaches*, ukenda haupo tena ufukwe washajenga hoteli hawawezi kukaa. Sasa ninadhani hii Serikali iwe makini katika hilo na miradi yote iliyokuwa haijafanyiwa tathmini ya kimazingira ifanyiwe.

Mhe. Naibu Spika, kuna chumba kile cha hoteli kiliopo chini ya baharini kile, kule Makangale. Jina lake la ile hoteli nimeisahau lakini kuna chumba kipo chini ya baharini. Je, mradi ule umefanyiwa tathmini ya kimazingira. Kama haujafanyiwa basi uende ukafanyiwa *environmental assessment*, yaani athari za kimazingira zilizopatikana tangu kuanzishwa ule mradi hadi hii leo. Kama hawakufanya basi tunaomba sana muende, kwa sababu kinyume na hivyo mutaendelea kutuathiri sana pale.

Halafu Waheshimiwa nitoe tanbihi sasa, nitumie dakika hizi chache zilizobakia kutoa nitanbihi kwamba hili siyo jukwaa la kisiasa. Waheshimiwa hili siyo jukwaa la kisiasa, hapa ni pahala pa wananchi. Yeyote ambaye ana hotuba zake za kisiasa anataka kutoa, basi mikutano ya hadhara inapatikana huku nje na ikiwa itakuwa hana zile *speakers* mimi Wilaya pangu aje achukue afunge lakini hapa siyo pa kutolea mikutano ya kisiasa hapa.

Nimalizie Mhe. Naibu Spika, kuhusu rasimu ya Katiba. Kwanza mimi ni-*quote* Jaji Robert Makaramba. Huyu ni Jaji wa Mahakama Kuu, ninadhani kama hajastaafu sasa hivi. *(Makofi)*

Jaji Robert Makaramba nendeni kitabu chake cha *Constitution-Making Process*. Hiki alikitunga katika miaka tisini na nane au tisini na saba, nimesahau ule mwaka. Alizungumzia *constitution-making process* akasema kuna *process* nne za kutunga Katiba, ni Jaji Robert Makaramba, siyo Saleh Nassor Juma *botanist* aah! ninasema *lawyer* Jaji Robert Makaramba. Mtaalamu katika mambo ya Katiba. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, amesema kuna hatua nne za kutunga Katiba. Hatua ya kwanza Jaji Robert Makaramba alisema kuna kitu unatengeneza kitu kitaitwa Tume ya Kutunga Katiba, ambacho hapa iliundwa hiyo Tume ya Kutunga Katiba.

Jambo la pili unafanya kitu kinaitwa *National Conversation* yaani unafanya makongamano ya Katiba, *National Constitution Conversation*, yalifanywa hapa na watu wakatoa maoni yao. Ile Tume ya Kutunga Katiba ilikuwa inaongozwa na Jaji Warioba na akafanya *National Conversation* nyingi wakatoa mawazo.

Baada ya kutoa mawazo ikapatikana Rasimu ya Katiba, ikafuatia *Constituent Assembly* ni hatua ya tatu. Kwa mujibu wa Jaji Robert Makaramba hatua ya tatu ya kutunga Katiba ni *Constituent Assembly*, yaani Bunge la Katiba.

Bunge la Katiba lilikuja kujadili Rasimu, ikajadiliwa Rasimu lakini mambo mengi yaliyotoka kwa wananchi yakatolewa, yakaingizwa mengine na hayo Bunge la Katiba likagawika vipande viwili; nusu wakatoka na wengine wakabakia mule ndani. Kwa hivyo mawazo ya wananchi ...

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa Mwenyekiti yamo ndani ya taarifa yako hayo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Eeh! ni katika mchango wangu.

**Mhe. Naibu Spika:** Hebu malizia.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Sasa Mhe. Naibu Spika, katika hili nimalizie kwamba huu ni mchango wangu na mimi sikupata kuchangia.

Ni kwamba Katiba imeanza tatizo tangu katika suala la Bunge la Katiba na kwa hivyo *referendum* ambayo ni hatua ya mwisho, vile vile itakuwa na matata. Kwa hivyo naomba Waheshimiwa wananchi walio wengi wajue kwamba kunakuja hiyo kura ya maoni, lakini kura ya maoni ya wananchi hasa yametolewa mule ndani. Kwa hivyo siku ya kura ya maoni wasijitokeze hata kidogo kwenda kupiga kura ya maoni.

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa niaba tunakushukuru.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu wa hali sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana mheshimiwa. Sasa Waheshimiwa hoja imetolewa niwahoji wale waliokubali ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wanyooshe mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Sasa Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwashukuru kwa kazi nzuri tuliyofanya tangu asubuhi hadi sasa hivi pamoja na ushirikiano mulionipa. Baada ya kazi hii ilikuwa tuanze kazi nyengine mpya ya wizara mbili; Wizara ya kwanza kuwasilisha ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza ilitolewa na Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji, Habari kwa mwaka 2013/2014 na baadae ije Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo .

Kwa kuwa nimezungumza na Mawaziri kila mmoja anataka si chini ya nusu saa na muda tuliokuwa nao ni mdogo. Kwa hivyo naahirisha Baraza letu mpaka saa kumi na moja za jioni.

*(Saa 6:51mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

## TAARIFA ZA SERIKALI

### Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2013/2014

**Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Nashukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuja hapa kutoa taarifa ya utekelezaji wa maagizo yanayotokana na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, katika kufuatilia utendaji wa shughuli za serikali, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema na kujaalia nchi yetu kuwa na amani na mshikamano, tunawapa wananchi wetu nguvu za kushiriki na kujituma kikamilifu katika harakati za kuinua maisha yao, pamoja na kuchangia kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, napenda kuchukua fursa hii adhimu kukupongeza kwa dhati wewe na Kamati yako ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, kwa kuendelea kutushauri kikamilifu katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya kazi ya wizara yangu.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu ni miongoni mwa wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi. Kwa kawaida wizara na kamati kwa jumla huwa zinafanyakazi za ufuatiliaji wa shughuli zilizopangwa kila robo mwaka. Shughuli hii husaidia wizara, kamati pamoja na wadau wengine wa wizara hii kuona mafanikio yaliyopatikana kwenye utekelezaji.

Aidha, kwa zile changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji, ambazo zilipelekea baadhi ya malengo kutofanyika. Wizara hupokea ushauri kutoka kwa wajumbe wa kamati na kufanyakazi kadiri inavyowezekana.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia utendaji huo Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilifanyakazi zake na kutoa ripoti yake kama kawaida, ambapo pamoja na mambo mengine kamati ilitoa maagizo kwa wizara yatokanayo na

wizara hiyo. Wizara ilipokea maagizo ya kamati kwa njia ya maswali, na kufanyakazi kwa kuyatolea majawabu kwa mujibu wa utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima sasa naomba kuwasilisha taarifa rasmi ya wizara yangu juu ya maagizo yatokanayo na taarifa ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, mbele ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Tukianza na sekta ya mifugo. Agizo la kwanza ilikuwa ni wizara ifanye marekebisho sheria ya mifugo, ili iweze kuwadhibiti wafugaji wakaidi ambao wanakwepa kupeleka mifugo yao katika chanjo za kujikinga na maradhi ya wanyama.

Utekelezaji kwa upande wa wizara, sheria ya rasilimali ya mifugo namba 11 ya mwaka 1999, imo katika hatua za mwisho za kufanyiwa marekebisho, baada ya kupita kwa wadau na watendaji wa sekta ya mifugo. Hivi sasa sheria iko kwenye Tume ya Kurekebisha sheria na inafanyiwa marekebisho ya mwisho kabla ya kuwasilisha katika ngazi za juu za maamuzi na hatimaye Baraza la Wawakilishi.

**Agizo la pili**

Eneo la mradi wa kupandisha ng'ombe kwa sindano Maruhubi ni eneo la karantini ya mifugo, hivyo lisitumike kwa shughuli nyengine kinyume na masuala ya mifugo.

**Utekelezaji**

Tatizo hili limefikishwa kwa Makamu wa Pili wa Rais na hadi sasa halijapatiwa ufumbuzi wake. Mhe. Makamu wa Pili, aliagiza watu wanaolitumia eneo hilo kinyume na utaratibu, watafutiwe eneo jengine ili waende. Wametafutiwa eneo Chumbuni Redio lakini hawataki kwenda huko. Kwa mujibu wa kitaalamu, eneo lile halipaswi kufanywa shughuli za kibinadamu kama inavyotumika hivi sasa. Hali hii inaathiri afya ya madume ya mbegu na hayatoweza kutoa mbegu kama inavyotakiwa.

**Agizo la tatu**

Kamati inaiagiza wizara kuvipatia taaluma zaidi vikundi mbali mbali vya wafugaji kuhusiana na elimu ya ushirika, biashara na ufugaji.

**Utekelezaji**

Idara inaendelea na kuwaelimisha wafugaji kuhusu utaalamu kwa ufugaji wa kisasa. Vikundi 16 vya wafugaji na wafugaji binafsi 19,600 walipatiwa mafunzo ya ufugaji wa kisasa Unguja na Pemba. Katika kipindi kilichobakia cha mwaka wa fedha huu, inatarajiwa kuwafundisha wafugaji elimu ya ushirika na biashara, masuala haya yote yameingizwa katika bajeti ya mwaka huu.

**Agizo la nne**

Wizara iwahamasishe wafugaji ili wachukuwe tahadhari mapema ya kuwakinga wanyama wao na maradhi mbali mbali kwa kuwapeleka kwenye chanjo.

**Utekelezaji**

Tahadhari ya mapema ya magonjwa ya mifugo na kuwalinda wanyama kwa kutumia chanjo. Mfumo wa tahadhari ya magonjwa ya mifugo kwa magonjwa ya miripuko upo na unaendelea kutumika.

Kwanza kwa wafugaji wa ng'ombe kuna chanjo za aina tatu ambazo hutolewa kwa kuwakinga ng'ombe na maradhi ya mripuko, ambazo ni kimeta cha mbavu na maradhi ya ngozi. Chanjo hizi hutolewa kila mwaka mara moja.

Kwa mwaka 2013/2014 jumla ya wanyama 3,102 wamechanjwa dhidi ya maradhi ya kimeta cha mbavu na 5,064 wamechanjwa dhidi ya maradhi ya ngozi.

Pili, kwa ufugaji wa kuku kuna chanjo za aina tatu ambazo hutolewa kwa chanjo hizi ni kama zifuatazo.

Mahepe hutolewa kila baada ya miezi mitatu na kila vinapozaliwa vifaranga vipya. Kwa mwaka 2013/2014, jumla ya kuku 1,064,763 wamechanjwa. Gumboro maradhi mengine hutolewa kwa kuku wa kisasa, kuku wa mayai na wa nyama, ambayo hutolewa mara mbili katika mwezi wa kwanza toka vifaranga kuzaliwa.

Kwa mwaka 2013/2014 jumla ya kuku 63,007 wameshachanjwa gumboro na 8,683 wamechanjwa dhidi ya maradhi ya ndui. Maradhi ya mahepe na gumboro hayanatiba, njia ya kuyadhibitini kwa chanjo tu.

**Agizo la tano**

Wizara imfikirie mfugaji Amir Khamis wa Kandwi kwa kusaidiwa kufikisha umeme katika sehemu yake ya mifugo.

**Utekelezaji**

Wizara imelipokea suala hili, hata hivyo kutokana na bajeti finyu ya mwaka huu wa fedha, wizara haikuweza kumfikishia umeme mfugaji huyo, yaani bwana Ameir Khamis wa Kandwi. Hata hivyo, suala hili litazingatiwa katika bajeti ya mwaka 2015/2016.

**Agizo la sita**

Wizara iharakishe ujenzi wa kituo cha uzalishaji na utibabu wa mifugo Unguja Ukuu, ili ujenzi huo ukamilike kama ulivyopangwa.

**Utekelezaji**

Ujenzi umeanza, jengo limejengwa kwa matofali na limeshaezekwa, kazi ya ukamilishaji wa ujenzi inaendelea kwa kutafuta mzabuni wa kumalizia ujenzi huu. Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika katika mwaka ujao wa fedha.

**Agizo la saba**

Kamati inaishauri wizara kuandaa mpango maalum utakaowezesha kujikinga na ugonjwa wa ndui unaoshambulia mifugo hasa kuku, njiwa na hata mabati mzinga baada ya mifugo hiyo kupatiwa chanjo ya mahepe.

**Utekelezaji**

Wizara kupitia idara ya huduma za utibabu wa mifugo, imetengeneza mpango wa kutoa chanjo kwa mifugo, inatoa elimu kwa wafugaji wa kuku jinsi ya kujikinga na maradhi ya ndui na kushajihisha wafugaji kukaa pamoja ili iwe rahisi kutumia chanjo ya ndui. Chanjo hii hutolewa mara moja kwa mwaka wa kuku wenye umri wa kuanzia wiki sita hadi wiki nane.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kupitia Idara Huduma za Utabibu za Mifugo, imeweka utaratibu wa kila wiki mara mbili, yaani Jumatatu na Ijumaa kutoa chanjo, ushauri na maelekezo, juu ya chanjo zote za kuku katika hospitali ya mifugo Maruhubi. Vile vile idara hutoa wataalamu wake kumfuata mfugaji yeyote yule anayetaka kuchanjiwa kuku wake.

Kwa kawaida ugonjwa wa ndui hauna tiba ya moja kwa moja, isipokuwa tunaweza kupunguza ukali wa virusi kwa kutumia dawa za kusafishia mabanda, kwa kuviuwa virusi vya ndui. Kwa kuku mmoja mmoja mfugaji anaweza kutibu ndui kwa kutumia *iodine*, *acriflavine* au *gentian violet,* kwa kuzipaka ndui kila siku hadi zipone.

**Agizo la nane**

Kwa kuwa wizara haina hati miliki katika shamba la mifugo la Pangeni, ingawa linalimiliki kwa muda mrefu sasa. Kamati inaiagiza wizara kupatiwa hati hiyo haraka ili kuepusha uvamizi wa eneo hilo unaoendelea.

**Utekelezaji**

Shamba la Pangeni lilishapimwa tokea miaka ya 50, watu wasiokuwa waaminifu wameng'oa alama za mipaka yaani *becones*. Watu waliokuwa wamechukuliwa sehemu zao, pia walishalipwa tokea mwaka 1959, wizara ilishapeleka ombi la kutengenezewa hati miliki wizara ya ardhi, lakini bado wizara ya ardhi haijatupatia hati miliki.

**Sekta ya Uvuvi**

**Agizo la kwanza**

Wizara iharakishe kutengeneza *business plan* itakayoongoza katika ununuzi wa boti za uvuvi kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, ambazo wizara na wavuvi wetu wanaweza kuzimudu kulingana na mahitaji ya mazingira ya Zanzibar.

**Utekelezaji**

Wizara imeandaa mpango wa kuendeleza uvuvi wa bahari kuu hivi sasa. Moja ya shughuli za mpango huu ni kutengeneza *business plan*. Hivi karibuni kamati imeteuliwa na serikali kutengeneza *business plan* hiyo. Wizara imefanya mazungumzo na Kampuni ya Hairo kuwekeza katika ujenzi wa maboti ya bahari kuu, kampuni hii itashughulikiana na serikali uvuvi wa bahari kuu.

**Agizo la pili**

Wizara ihakikishe kwamba inawapatia hati miliki ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya madiko wanayotumia wavuvi wetu.

**Utekelezaji**

Kuna baadhi ya madiko tayari yameshapatiwa hati miliki, nayo ni Nungwi, Tazari/Kilimani, Matemwe Kigomani, Pwani Mchangani na Kendwa na bado wizara itaendelea kutengeneza hati miliki za maeneo mengine.

**Agizo la tatu**

Wizara iwaandikie viongozi mbali mbali wakiwemo wale wa Baraza la Wawakilishi, kufuata taratibu zinazokubalika katika utekelezaji wa sheria za uvuvi.

**Utekelezaji**

Wizara tayari imeshaandaa muongozo na umeshapatiwa Baraza la Mapinduzi, tuko katika maandalizi ya kuchapisha vitabu vya muongozo huo na baadaye kuvisambaza kwa wanaohusika, wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi.

**Agizo la nne**

Kamati inataka kuongeza muda zaidi wa doria za baharini na angani, kwani inasaidia kuwashajihisha wenye meli na uvuvi wa bahari kuu, kukata leseni na hatimaye kuongeza mapato ya mamlaka na taifa kwa jumla.

**Utekelezaji**

Kutokana na bajeti ya hivi sasa, wizara imejitahidi kuongeza doria za baharini, ambapo doria 150 zilifanywa kwa mwaka 2013/2014. Kwa upande wa doria za angani kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2013/2014, jumla ya saa 912 za doria za majini zimefanyika na kuanzia mwaka 2009/2010 hadi Februari 2015 jumla ya masaa 914 za doria za anga zilifanyika. Doria hizi zimepunguza uvunaji haramu katika bahari kuu na kuongeza mapato ya serikali. Kutokana na kuimarika kwa ulinzi, haijakamatwa meli inayovua uvuvi haramu kwenye bahari kuu ya Tanzania kwa jumla.

Aidha, idadi ya leseni za uvuvi wa bahari kuu zilizokatwa zimeongezeka kutoka leseni 23 mwaka 2009/2010 hadi leseni 77 mwaka 2013/2014 na hadi kufikia mwezi Januari 2015 leseni 62 zimekatwa. Mapato ya serikali

yameongezaka kutoka bilioni 1,123,200,000 mwaka 2009/2010 hadi shilingi bilioni 3,030,578,100 mwaka 2013/2014.

**Agizo la tano**

Wizara ihamasishwe uwepo wa ufugaji wa samaki wa maji baridi, pamoja na kuwapa kipaumbele na mashirikiano kwa wale wote wanaoanzisha ujasiriamali huu kwa kuwapa misaada na chakula cha samaki.

**Utekelezaji**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeshahamasisha wananchi kuhusu ufugaji wa samaki wa maji baridi. Pia imetoa huduma ya utaalamu wa ujenzi bora wa mabwawa ya kufugia samaki na kusaidia kusambaza vifaranga vya samaki hawa wa maji baridi. Hadi sasa kuna jumla ya mabwawa sita ya kufugia samaki ya maji baridi katika maeneo ya Mangapwani, Mwera, Mgeni Haji, Unguja Ukukuu na mmoja katika wajumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Mshimba Mbarouk, ni mmoja katika mfano na yeye ametengeneza mabwawa kule na tumeshatembelea na kwa kweli wako katika hatua nzuri sana, ni mfano wa kuigwa kwa kweli, hongera sana. Dimani na Kizimkazi vile vile.

Aidha, utaalamu wa utengenezaji wa chakula cha samaki umetolewa, pamoja na kufanya mawasiliano na mwenye kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki, kwa ajili ya kueneza huduma za chakula kwa wafugaji wa samaki.

*Formula* ya kutengeneza chakula cha samaki ni kama mnavyoona Waheshimiwa Wajumbe hapo, nafikiri mtajisomea. Lakini nikiendelea tu kwamba vyakula hivyo vinakauswa na kuchanganywa pamoja baada ya kusagwa na kufanywa vidonge yaani *pellets,* ambavyo hukauswa vizuri ili kuongeza muda wa kukaa bila ya kuharibika kabla ya kulishwa samaki.

**Hitimisho**

Mhe. Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, waipokee, waijadili, waitolee maoni, ushauri na mapendekezo na hatimaye waikubali kwa lengo la kuendeleza sekta ya mifugo kwa manufaa ya wananchi wetu. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, kwa kuniwezesha kuwasilisha utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa kwa Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2013/2014.

Aidha, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kusimamia na kutekeleza shughuli mbali mbali za wananchi iliyotokana na ripoti hiyo. Namuomba Mwenyezi Mungu atuongoze hekima, busara na uwezo wa kuwatumikia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Mlinde Mabrouk Juma Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako tukufu, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo, kwa maoni, mapendekezo na mashirikiano makubwa wanayoipa wizara yangu, ambayo imesaidia sana katika utekelezaji wa mipango ya wizara yangu. Napenda kuwahakikishia kwamba daima ushauri, mawazo na maelekezo yao tunapokea na kuyafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ilipewa maagizo 26 katika taasisi mbali mbali. Uchambuzi wa maagizo ulikuwa kama ufuatavyo.

Shirika la Utangazaji la Zanzibar maagizo 7, Idara ya Habari Maelezo maagizo 2, Shirika la Magazeti ya Serikali maagizo 2, Tume ya Utangazaji Zanzibar maagizo 2, Chuo cha Uandishi wa Habari agizo moja, Kampuni ya Uunganishaji Maudhui agizo moja, Kamisheni ya Utalii maagizo 2, Chuo cha Maendeleo ya Utalii maagizo 2, Hoteli ya Bwawani maagizo 4, Chama cha Mpira wa Miguu maagizo 3 na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale agizo moja.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa maagizo hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli lifuatalo. Katika Shirika la Utangazaji, agizo la kwanza serikali ihakikishe inaweka majenereta ya uhakika katika studio za *ZBC* pamoja na kujipanga katika gharama za uendeshaji wa majenereta hayo wakati wa dharura.

**Utekelezaji**

Katika kipindi kinachoendelea Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia Shirika la Utangazaji, imeweza kuweka majenereta katika vituo vyake mbali mbali, vikiwemo Rahaleo studio ya redio, Karume House studio ya televisheni Masingini na kituo cha kurushia matangazo ya televisheni na redio Dole na kituo cha kurushia matangazo na Bungi katika mnara wa kurushia matangazo. Jenereta limefanyiwa matengenezo na linafanyakazi vizuri, isipokuwa shirika linatafuta waya maalum kutoka kwenye jenereta hadi kwenye mitambo ya studio.

**Agizo la pili**

Kamati inaitaka serikali iharakishe upatikanaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi wa Soni kwa lengo la kuimarisha vifaa vyake, ikiwemo ununuzi wa *microwave* kwa upande wa televisheni, pamoja na *link* kwa upande wa redio ili kuwezesha *ZBC* kuweza kurusha moja kwa moja matangazo yake na kuwacha kutegemea vituo vyengine wakati wa kurusha matukio makubwa ya kitaifa.

**Utekelezaji**

Mradi wa Soni tayari umekamilika kwa Wizara ya Fedha kuilipa Kampuni ya Soni iliyofunga vifaa vya studio kwa Unguja na Pemba. Aidha, *ZBC* imenunua *microwave* pamoja na *link* kutoka katika bajeti yake, na kwenye vifungu vya matumizi mengine *other charges* zinazotoka Wizara ya Fedha.

**Agizo la tatu**

*ZBC TV* ifikirie kuanzisha *channel* nyengine.

**Utekelezaji**

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hiki *ZBC* imeanza kufanya majaribio ya channel namba 2 ambayo inaitwa *ZBC* 2.

**Agizo la nne**

*ZBC* iwe makini na baadhi ya watangazaji wake ambao mara nyingi wanakosea kosea majina ya watu na sehemu maarufu.

**Utekelezaji**

Mhe. Naibu Spika, kufuatia Deutsche Welle kutoa mafunzo mbali mbali ya kitaalamu, kutokana na mabadiliko ya teknolojia. Wafanyakazi wa *ZBC* wameweza kupatiwa mafunzo ya kujiimarisha na kwenda na wakati, kwa lengo la kukidhi ushindani wa tathnia ya habari.

Jumla ya idadi ya mafunzo waliotoa Shirika la Utangazaji la Ujerumani yaani Deutsche Welle ni saba, kwa mafunzo mbali mbali ambayo ni fani ya utayarishaji wa vipindi vya redio na televisheni na fani ya uongozi wa shirika. Mafunzo hayo yamesaidia sana kuondoa tatizo lililokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niongeze hapa kwamba mimi mwenyewe nimeonana na Mkurugenzi wa mafunzo wa Deutsche Welle, na kwa kweli ameahidi kwamba ataendelea kuwasaidia na kuwanoa wafanyakazi wetu.

**Agizo la tano**

*ZBC* iwe makini na ihakikishe kwamba taarifa zake za habari zinakwenda na wakati. Pia wahakikishe kwamba hawapitwi na habari muhimu, hasa za kitaifa na kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, Utekelezaji wake ni kwamba ni kweli hapo nyuma kulikuwa na tatizo la uchelewaji wa taarifa ya habari, kwa sasa tatizo hilo limepungua hasa baada ya kupata vifaa vya kisasa, vilivyonunuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mradi wa Soni.

Aidha, kwa sasa *ZBC* inakwenda sambamba na Mashirika mengine ya kihabari ulimwenguni kufuatia kukamilika kwa mradi wa Soni.

**Agizo La Sita:**

Ili kukuza mapato ya shirika ZBC ihakikishe kwamba taasisi zote za Serikali na watu binafsi zinalipa matangazo yao yanayorushwa na shirika hilo.

**Utekelezaji:**

Shirika la Utangazaji limeendelea kuchukua hatua ya kuelimisha taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi zinazopatiwa huduma na ZBC kwa ajili ya malipo kabla ya kupatiwa huduma, au baada ya kufanyiwa shughuli za matangazo yao. Aidha, kwa taasisi binafsi nazo zinaendelea kuwapa elimu juu ya umuhimu wa kulipa kabla ya huduma na baada ya kupatiwa huduma kwa ajili ya kujiengezea mapato.

**Agizo Saba**

Kamati inaitaka Wizara kukaa pamoja na Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Katibu Mkuu wa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, kulipatia ufumbuzi wa kuduma suala la kulipia matangazo ya mikutano ya Baraza la Wawakilishi kwa ZBC, kwani kamati inaamini kwamba ZBC inaweza kujiimarisha endapo Baraza la Wawakilishi litalipia matangazo haya.

**Utekelezaji**

Agizo hili linaendelea kufanyiwa kazi ambapo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inawasiliana na inaendelea kuwasiliana na Mhe. Waziri wa Fedha Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa ajili ya kufanya mazungumzo, mazungumzo mengine yamepangwa kufanyika katika kipindi hichi cha mwaka 2015/16 ili kuanzia mwaka mpya wa fedha ZBC ianze kulipwa.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Habari Maelezo kulikuwa na maagizo mawili, la kwanza Wizara ipewe kipaumbele kwa ununuzi wa vifaa vya kazi hasa vipaza sauti kutokana na umuhimu wa Idara hiyo, ukizingatia kwamba hivi sasa huduma za idara zinahitajika kwa kiwango kikubwa.

**Utekelezaji**

Idara imeweza kununua vifaa vya vipaza sauti kama vile spika mbili, stendi moja, waya wa *microphone roll* mbili, mabomba mawili na nyaya za umeme mita 50.

**Agizo la Pili**

Idara ijitangaze zaidi hasa katika mauzo ya picha na mabango mbali mbali yanayotengenezwa na Idara hiyo kwani idara inaweza kujiongezea mapato makubwa katika mauzo hayo.

**Utekelezaji**

Idara imeendelea kujitangaza kupitia Redio na Televisheni na magazeti katia mauzo ya picha na mabango ya Baraza la Mawaziri hasa yakitokea Mbadiliko ya Baraza la Mawaziri na viongozi wapya, kwa siku za kawaida mauzo ya picha na mabango ya Baraza la Mawaziri yanaendelea.

Katika Shirika la Magazeti kulikuwa na maagizo mawili, la kwanza mradi wa ujenzi wa Ofisi na kiwanda cha kuchapisha magazeti ya rangi hapa Zanzibar uingizwe katika miradi ya maendeleo katika bajeti ya maendeleo ya Serikali.

**Utekelezaji**

Wizara imelipokea agizo hilo la kamati na kulifanyia kazi kwa kuwasilishwa mradi huo Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango ili liingizwe katika miradi ya maendeleo ya Serikali katika bajeti ya mwaka 2014/15, lakini kutokana na uhaba wa fedha katika bajeti hiyo mradi huo haukufanikiwa kuingizwa katika miradi ya mwaka huu wa fedha, ambao pia utawasilishwa tena katika bajeti ijayo ya mwaka 2015/16 kwa kuombewa kuingizwa katika bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali. Wakati hatua hizi zikiendelea pia Wizara imechukua hatua mbali mbali za kulitafutia shirika mtambo wa kuchapisha magazeti yake kwa kuandika maombi ya miradi nchi mbali mbali ikiwemo nchi ya Saudi Arabia, China na Oman tayari mazungumzo ya awali yamefanyika baina ya Wizara ya habari ya Zanzibar na Wizara ya habari ya Oman juu ya utekelezaji wa agizo hili.

**Agizo la Pili**

Shirika liangalie uwezekano wa kutoa angalau ukurasa mmoja ndani ya gazeti la Zanzibar leo chapisho la kiingereza ili kuwasaidia wageni ili nao wafaidike na magazeti yetu.

**Utekelezaji**

Wizara imelipokea pendekezo hili kwa uzito mkubwa na kukubaliana umuhimu wa kuwepo Gazeti la Kiingereza katika Shirika la Magazeti ya Serikali, ambapo tayari shirika kupitia bodi yake limeagizwa kutekeleza suala hilo. Hata hivyo uwekaji wa ukurasa mmoja wa lugha ya kiingereza katika magazeti ya sasa ya kiswahili si utaratibu sahihina haupo katika tasnia ya magazeti ya ulimwenguni hivi sasa, jambo kama hilo huonekana katika majarida tu. Shirika linalifanyia kazi agizo hilo kama walivyolifanyia kazi agizo la kuwa na gazeti la Michezo ambalo sasa zinachapishwa na Shirika la Magazeti.

Katika Tume ya Utangazaji kulikuwa na maagizo mawili, la kwanza kamati inaishauri Serikali kuandaa mfumo wa king'amuzi kimoja kwa watoa huduma wote ili kiuwaondoshea mrundikano wa ving'amuzi watumiaji.

**Utekelezaji**

Utaratibu wa matumizi ya ving'amuzi uliopo sasa unaruhusu king'amuzi kimoja kupokea matangazo kutoka kwa mtoa huduma kuna tangazo la televisheni bila ya malipo iwapo matangazo hayo yatarushwa yaani *Freat Air,* katika mfumo huu seti za Televisheni zilizo katika mfumo wa DVD 2 utaweza kupokea matangazo hayo kwa antena na na bila hata kutumia king'amuzi kwa matangazo ya aina hiyo yasiyolipiwa. Utaratibu huu unabadilika kwa matangazo ya kulipia ambapo mteja unatakiwa kuwa na mkataba na mtoa huduma na kukubali kuunganishwa na huduma za kituo cha Televisheni kwa kulipia ada, mfumo huu ni wa kibiashara na ili kuweza kufanikiwa kunatakiwa kuwepo na mfumo wa kudhibiti wateja.

Utaratibu unaoweza kutumiwa king'amuzi kimoja kwa matangazo ya vituo vyote kwamba lazima kiwepo king'amuzi kisichoweka kizibiti, katika utaratibu huu mtoa huduma wa Televisheni za kulipia anaweza kuwatambua wateja wake kwa kuingiza kifaa cha kudhibiti wateja ndani ya king'amuzi kinachoitwa *CAM* yaani *Conditional Axes Maul*, utaratibu huo unaweza kutumika kwetu lakini utaongeza bei ya king'amuzi kwa asilimia sitini.

Aidha, king'amuzi cha aina hii kinaweza kupunguza mrundikano wa ving'amuzi kwa watumiji lakini kikawapa watumiaji usumbufu wa kubadili kila wanapotaka kubadili kupokea huduma kituo chengine. Wizara inapendekeza utaratibu uliopo sasa uendelee kwa sababu ya kuwajali wanyonge bila ya kuruhusu kupokea matangazo huria, ambapo mtumiaji anashindwa kulipa ada ya kila mwezi.

**Agizo la Pili**

Kamati imeiagiza Wizara kuangalia uwezekano wa kulegeza masharti ili kuwavutia zaidi wawekezaji kwa upande wa Televisheni.

**Utekelezaji**

Katika sera ya utangazaji wa mwaka 2008 Sheria ya utangazaji ya mwaka 1997 na kanuni za utangazaji za mwaka 2010 hakuna masharti magumu yaliyomo ndani yake na kukwaza uwekezaji wa vituo vya Televisheni. Aidha mabadiliko ya *Technologies* ya utangazaji kutoka mfumo wa *Analogies* kwenda *Digital* pia yamelegeza masharti ya wawekezaji kwa hivi sasa, ntoa huduma ya matangazo ya Televisheni halazimiki kuweka mitambo ya kurushia matangazo, huduma ya kurushia matangazo inayofanywa na usambazaji wa ishara *multiply operator* kama vile *Z. mixer* wengine.

Katika utaraibu huu gharama gharama huwa ndogo kwani ada inayolipwa ni makubaliano baina ya mtoa huduma maudhui na mrushaji wa matangazo kulingana na masafa ambayo Mwenyekiti wetu wa maudhui anapenda kufikishiwa huduma zake.

Katika chuo cha uandishi wa habari kulikuwa na agizo moja Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo izungumze na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili ofisi zinazotumiwa na FAWE zitumiwe na Chuo ikiwa kinakabiliwa na uhaba wa tatizo la nafasi. Utekelezaji wake suala hili umewsilishwa Serikalini na maelekezo ni kwamba Chuo cha Habari kimeanzimwa na Fawe hivyo itakuwa vigumu Fawe kuhamishwa.

Katika jitihada za kukipatia chuo eneo lao ili kiwe na nafasi ya kutosha Chuo kimepatiwa eneo jengine la iliyokuwa Kilimani Bar ili kihamie huko, Serikali imetoa fedha na ujenzi wa Chuo huko Kilimani unaendelea ambapo Chuo kitahamia baada ya awamu ya kwanza ya ujenzi kukamilika.

**Agizo la Sita**

Kampuni ya *Zanzibar Multiplex (ZMUX)* wawekezaji wa AGAPE wameshindwa kazi na wameitia hasara Serikali hivyo kamati inaitaka Serikali kupitia upya mikataba ya ujenzi wa miundombinu na uendekeshaji wa *Digital* kati ya Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo na Kampuni ya AGAPE.

**Utekelezaji**

Suala hili tayari limeshashughulikiwa na Serikali na taratibu zimekamilika za kuondokana na mkataba ulioipa Mamlaka kampuni ya *AGAPE* kazi ya kuwa mwendeshaji wa shughuli za *Digital* na sasa shughuli hizo zinaendeshwa na wafanyakazi wenyewe wa Zanzibar Multi Place.

Katika Kamisheni ya Utalii kuna maagizo mawili, la kwanza kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii wawekezaji na mali zao.

**Utekelezaji**

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa ulinzi na usalama unaimarishwa Serikali imechukua juhudi za kuanzishwa kikosi cha ulinzi wa utalii ambapo kipo chini ya Mamlaka ya Jeshi la kujenga Uchumi, uanzishwaji wa kikosi hichi kisheria tayari umeshapitishwa na Baraza lako tukufu Mheshimiwa Naibu Spika.

Aidha, Kamisheni ya Utalii kupitia miradi ya maendeleo imendelea na utayarishaji wa *Software* itakayotumika kutolea taarifa za hali ya usalama pale tukio litakapotokea au linapoonekana linaweza kutokea kwa tukio la uvunjifu wa amani katika maeneo ya utalii. *Software* hii itawekwa katika Ofisi za Kamisheni ya Utali na katika Ofisi ya Vikosi vya Ulinzi ili kurahisisha upatikanaji wa uchukuaji wa hatua za ulinzi na kiusalama kutokana na hali husika.

**Agizo la Pili**

Katika Kamisheni ya Utalii ni kuongeza bajeti ya utangazaji na uendeshaji wa shughuli za utalii, utekelezaji jitihada za kuhangaika bajeti ya utangazaji na uendeshaji wa shughuli za utalii zimeanza kwa kupitia maabara ya utalii Serikali imetenga fungu maalum la kutangaza utalii, na ndio maana hivi karibuni tumetiliana sahihi juhudi ya kuanzisha Ofisi ya kutangaza utalii nchini India. Katika maandalizi ya bajeti inayoendelea mwaka 2015/16 kasma ya kuutangaza utalii itaongezwa.

Katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii kuna maagizo mawili, la kwanza Kamati inashauri kujenga kwa hosteli za wanafunzi.

**Utekelezaji**

Bodi ya Chuo cha Utalii imeanza kuomba kiwanja kutoka Idara ya Ardhi Majengo na Mipango Miji kwa amatayarisho ya awali ya kujenga Hosteli, kwa sababu hivi sasa chuo hakina kiwanja kwa ajili ya shughuli hiyo.

**Agizo laPili**

Wizara ikuze mashirikiano kati ya Chuo na Wawekezaji wa Mahoteli ili kuondosha usumbufu na manyanyaso kwa wanafunzi wanaokwenda *field* .

Utekelezaji agizo hili limetekelezwa kwa kufanywa mazungumzo na wamiliki wa mahoteli kuanzia mwaka 2013/14 mtazamo wa mahoteli mengi imebadilika, takriban mahoteli mengi yamekuwa na mkabala mzuri wa Chuo cha Utalii hat zile hoteli ambazo zilikuwa hazipati kuchukua wanafunzi wetu kuanzia mwaka 2014 wameanza kuchukua na wengine wanawapa ajira. Pia wamebainika kuwa hoteli ambazo wanafunzi wetu wanapata ajira kutoka ngazi za uongozi zinachukua wanafunzi wengi wa chuo, mfano hoteli ya Lamagru Grada iliyoko Makunduchi ilikuwa haitaki kabisa kuchukua wanafunzi wa Chuo chetu, lakini tokea tubadilishe uongozi na kuwekwa PO ambae alikuwa mwanafunzi wetu mkabala wa hoteli hiyo na Chuo umekuwa mzuri zaidi.

Katika hoteli ya Bwawani kulikuwa na maagizo manne, la kwanza Wizara iendelee kulifanyia matengenezo sehemu zote chakavu za hoteli hiyo.

**Utekelezaji**

Uongozi wa Hoteli ya Bwawani umeendelea kufanya matengenezo ya sehemu chakavu za hoteli ya Bwawani kadiri uwezo wa fedha unavyoruhusu, sehemu ambayo hadi sasa uongozi wa hoteli umefanikiwa kutengeneza na kurejesha hadhi yake ya matumizi ni mkutano wa mkutano wa *roof top* ambao kwa sasa unatumika na vile vile kuzifanyia kumbi nyengine marekebisho madogo madogo katika ukumbi wa salama na marekebisho madogo madogo katika vyumba vya kulala. Vyumba ita vimekwishafanyiwa matengenezo na vyumba vyengine sita vinaendelea na mtengenezo.

**Agizo la Pili**

Katika hoteli ya Bwawani Wizara izidi kuziandikia na kuzikumbusha zaidi taasisi za Serikali ili kuitumia ipasavyo hoteli hiyo, uongozi wa hoteli katika utekelezaji wake unaendelea kujitangaza na kuomba Serikali kutumia hoteli yetu.

**Agizo la tatu**

Wizara izidi kutuatilia madeni yote ya hoteli hiyo, Wizara kupitia Uongozi wa Hoteli ya Bwawani umeendelea kufuatilia na kuziandikia taasisi za Serikali na za binafsi kuweza na kuzitaka kulipa madeni yao ambayo yanadaiwa na hoteli. Katika jitihada hiyo jumla ya shilingi milioni 170,412,848/= zimelipwa na deni lililobakia ni shilingi 85, 188,910/=.

**Agizo la Nne**

Wizara ifuatilie na ilimalize suala la mgogoro wa Pemba Bar, utekelezaji suala hilo limefuatiliwa na tayari sasa mgogoro wa Pemba Bar umeshamalizika na sehemu hiyo wameshakabidhiwa uongozi wa hoteli.

Katika Chama cha Mpira wa Miguu kulikuwa na maagizo mawili, kwanza ZFA ifanye kazi kwa mashirikiano ya hali ya juu kati ya viongozi wa Chama hicho na wadau wote wa michezo hapa nchini, kwani endapo uongozi wa chama hicho utayumba pia maendeleo ya chama hicho yatarudi nyuma.

**Utekelezaji**

Uongozi wa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar umeendelea kufanya kazi pamoja na wadau wake wote ambao ni ZFA Wilaya, pamoja na kamati zote za mpira kama vile kamati za waamuzi, kamati ufundi na kamati za mpira za wanawake pamoja na uongozi wa vilabu vya mpira.

Agizo jengine uongozi wa sasa wa *ZFA* uwe karibu zaidi na uongozi wa *TFF* na kuhakikisha kwamba mgao wa Zanzibar unapatikana.

**Utekelezaji**

juhudi mbali mbali zimechukuliwa na uongozi wa sasa wa *ZFA* kwa kufanya vikao mbali mbali kwa nia ya kuendeleza mchezo huo nchini.

Agizo jengine Serikali ipunguze au iondoshe ushuru katika vifaa vya michezo vinavyoingizwa nchini kwa shughuli za michezo sio biashara, Wizara imekuwa ikiomba msamaha, utekelezaji wake Wizara imekuwa ikiomba msamaha wa kodi kwa vifaa vya michezo vinavyoingizwa nchini kwa shughuli za michezo bila ya tatizo lolote lile kutoka katika taasisi zinazoshughulika na kutozwa ushuru na itaendelea kufanya hivyo, kila muda unapohitajika kufanya hivyo.

Katika Idara ya Makumbusho mambo ya kale kuna agizo kamati imeagiza Wizara kuendeleza zaidi maeneo hayo na kuyatangaza pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu ya kufikia sehemu hizo.

**Utekelezaji**

Wizara imeendelea kuyaendeleza maeneo kihistoria kwa kuyafanyia matengenezo ili kuyaweka katika hali ya uimara ili kuweza kudumu kwa miaka mingi zaidi katika fedha, miradi ya maendeleo pia Idara ya makumbusho ya mambo ya kale imeyatangaza maeneo yake ya kihistoria kwa kuyatangaza katika vyombo vya habari kwenye Televisheni na Redio, pamoja na kuendesha mikutano kwa wananchi kuwaeeleza umuhimu wa maeneo hayo kuwa ni hazina yao na inafaa wao kuyalinda ili yaweze kudumu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hayo ndio maagizo niliyopewa na Kamati ya Baraza lako tukufu na huo ndio utekelezaji wake tumejitahidi kadiri inavyowezekana, kulingana na hali ilivyoruhusu upatikanaji wa fedha na kwa heshima Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Mlinde Mabrouk Juma (Mwenyekiti Kamati ya Mifugo, Utalii na Uwezeshaji na Habari)** Mhe. Naibu Spika, Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (Subhana Wataala) kwa kutujaalia neema zake na kutuwezesha kuendelea kua hai tukiwa wazima wa afya njema.

Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imepewa majukumu ya kusimamia Wizara zifuatazo:-

1. Wizara ya Habari, Utamaduni , Utalii na Michezo
2. Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Mhe. Naibu Spika , Naomba sasa kwa heshima niwasilishe mbele ya Baraza lako Tukufu, muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015 kama ifuatavyo;-

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO**

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari , Utamaduni, Utalii na Michezo ina dhamana ya kusimamia sekta kuu nne (4) ambazo ni Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

**Sekta ya Habari**

Katika Sekta ya Habari, Kamati inaendelea kusikitishwa na mazingira magumu ya kazi licha ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na watendaji waliomo katika sekta hii.

Mhe.Naibu Spika, Kamati imegundua kwamba, kuna Changamoto kubwa ya kihabari Kisiwani Pemba, suala hili limejengeka kwa Utamaduni wa woga na usiri mkubwa miongoni mwa viongozi wa serikali hasa Maofisa wadhamini katika utowaji wa habari au taarifa mbali mbali zenye maslahi kwa jamii. Hali hii inaleta mvutano mkubwa kati ya wanahabari na baadhi ya Maafisa Wadhamini huko Pemba. Mhe. Naibu Spika**,** Kamati inaiagiza wizara na serikali kwa ujumla kulipatia ufumbuzi tatiza hili, likiachiwa ni kwenda kinyume na haki za Binadamu na Utawala bora.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu ilitembelea vyama vya waandishi wa Habari ikiwemo Pemba Press Club iliyopo Chake chake , Baraza la Habari Tanzania (*MCT*) Ofisi ya Zanzibar iliyopo Mlandege na Jumuiya ya Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*) Ofisi ya Zanzibar iliyoko Mombasa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imegundua kwamba vilabu na Vyama hivyo zimeanzishwa kwa lengo la kukuza viwango vya taaluma ya uandishi wa Habari kwa wanachama wake na kuraghibisha mashirikiano miongoni mwa waandishi wa habari, vyanzo vya habari na jumuiya za kitaaluma.

Aidha, Vilabu hivyo viko mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba Uhuru na haki ya kupata habari unalindwa, waandishi wa habari wanatekeleza vyema Wajibu wao (maadili). Kutokana na juhudi na mchango mkubwa wa Vilabu vya waandishi wa Habari hapa nchini kwa wanachama wake , Kamati inaitaka Wizara kuongeza mashirikiano na vilabu hivyo.

Mhe.Naibu Spika, vile vile Kamati inaiomba Wizara Kukaa na wadau wengine ili kuzipitia upya sheria kandamizi dhidi ya uhuru wa habari, ikiwemo Sheria ya Magazeti Namba 6 ya mwaka 1976 na Sheria ya Usalama wa taifa ya mwaka 1970 na nyenginezo.

**Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*)**

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaamini kwamba Serikali ilikua na nia njema ya kuanzisha *ZBC* kwa kuziuunganisha iiyokuwa Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar ( *STZ*) na Televisheni Zanzibar (*TVZ*), lengo likiwa ni kuwa na chombo kimoja chenye nguvu katika kuwahamasisha wananchi, kuwaelimisha na kuwapatia habari zilizofanyiwa utafiti, uhariri makini na zenye kuelezea sera na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuhakikisha kwamba umoja wa wananchi wa Zanzibar unaendelea kudumu nchini.

Hata hivyo utendaji wa Shirika hili hivi sasa unapigiwa kilele, na wananchi hawaonyeshi kuridhika na utendaji huo. Kamati yangu imebaini kwamba ucheleweshaji wa Ruzuku kutoka Wizara ya Fedha, unachangia kutokutekelezwa kikamilifu na kwa wakati Mipango ya Shirika hilo. Hapa Kamati inakubaliana kabisa na ile nukuu isemayo

> "Kama tunataka kupata maziwa bora, lazima tuhakikishe kuwa ng'ombe wetu tunampa malisho ya kutosha na kwa wakati."

Mhe. Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa Shirika la ZBC lilianzishwa bila ya kuwa na msingi wa kutosha wa kujiendesha lenyewe, halikadhalika Shirika limerithi mzigo mkubwa wa madeni jambo ambalo linarudisha nyuma utendaji kazi wa Shirika.

Kamati inaendelea kusikitika kuona kwamba bado taasisi nyingi za serikali, ikiwemo Baraza la Wawakilishi hazilipii matangazo yao, suala hili linarejesha nyuma ukusanyi wa mapato na hivyo kushindwa kujiendesha kama Shirika.

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena Kamati inaitaka Wizara kukaa pamoja na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Fedha kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala la kulipia matangazo ya Mikutano ya Baraza la Wawakilishi, kwani kamati inaamini kua *ZBC* inaweza kujiimarisha sana endapo BLW litalipia matangazo hayo.

**Kampuni ya Zanzibar *Multiplex* (*ZMUX*)**

Mhe. Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa lengo la kuanzishwa kwa Kampuni ya *Zanzibar Multiplex (ZMUX)* halijafikiwa, ikizingatiwa kwamba *ZMUX* imeanzishwa kama Kampuni ambayo ipo ndani ya Wizara ya Habari,

lakini bado haijakuwa na vyanzo vya kukusanya mapato na kujiendesha yenyewe, hivyo kuibebesha mzigo sana Serikali.

Kamati inaiagiza Wizara kwamba, Kamati iliyoundwa kwa ajili ya kutafiti kuendelea kuwepo kwa *ZMUX* au la ikamilishe kazi yake haraka na itowe majibu ya matokeo ya utafiti wao kwa wakati uliopangwa.

**Shirika la Magazeti ya Serikali**

Mhe. Naibu Spika, Kamati imegundua kwamba Shirika la Magazeti Zanzibar limeweza kuchapisha magazeti kama ilivyopangwa na kuyasambaza katika maeneo mbali mbali ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara huku likiendelea kufaidika na ufadhili wa Mfuko wa vyombo vya Habari Tanzania (*TMF*) ambapo Ofisi ya Pemba inaonekana kufaidika na ufadhili huo.

Hata hivyo, Mazingira ya kazi katika Ofisi za Shirika hilo sio rafiki kwa utendaji wa kazi na kuna madai ya wafanyakazi kuathirika kwa ugonjwa wa presha na macho kutokana na hali ya joto na giza katika sehemu hizo.

Mhe. Naibu Spika, wakati taasisi zilizo nnje ya Serikali zikiendelea kupunguza madeni yake, bado taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinadaiwa karibu shilingi milioni 400 kati ya shilingi 686,439,474/= zilizokuwa zikidaiwa kwa taasisi mbali mbali hadi kufikia Disemba 31,2014. Kamati inaishauri Wizara iwasiliane na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba wadaiwa wote walio chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakakatwa moja kwa moja kupitia katika vifungu vyao na kulipwa Shirika.

**Kituo cha Redio Jamii-Tumbatu *FM***

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaendelea kuipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Shirika la *UNESCO* kwa kuendelea kuwahamasisha wanajamii kuazisha vituo vya Redio jamii.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mwamko huo redio jamii nyengine mbili zimezinduliwa ikiwemo Redio Tumbatu na Redio Jamii Mkoani. Wakati wa kazi za Kamati, Kamati yetu ilivuka Maji hadi Tumbatu kuangalia maendeleo ya redio jamii iliyopo katika sehemu hiyo ambapo ofisi za redio hiyo zipo ndani ya jengo la Ofisi ya Wilaya Ndogo ya Tumbatu, Kamati inaamini kwamba jambo hili linaweza kuifanya redio hii kufanya kazi kwa kufuata maelekezo ya mtu fulani au kikundi fulani suala ambalo ni kinyume na uanzishwaji wa radio hiyo.

**Ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari**

Mhe. Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na harakati za ujenzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar hapo Kilimani. Shughuli hizo ambazo zimeanza Mwezi Desemba 2014 zinaonekana kutia matumaini na Kamati inaamini kwamba ujenzi huu utakapokamilika utasaidia sana katika kupunguza tatizo la uhaba wa madarasa ya kufundishia katika chuo hiki. Hata hivyo Kamati inaiagiza Wizara kutafuta Hatimiliki ya eneo hilo ili liendelee kuwepo kwenye usalama zaidi na kujiepusha na khitilafu zozote zinazoweza kujitokeza katika suala la umiliki, pia Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuwapatia fedha za ujenzi kwa wakati ili ujenzi huo umalizike kwa haraka.

**Sekta ya Utalii**

**Vituo vya Kukusanya Habari Na Takwimu Za Utalii**

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea vituo vya kukusanya Habari na takwimu za watalii Uwanja wa Ndege Kisauni, na Bandanirini Malindi Mjini Zanzibar. Kamati inapongeza kuazishwa kwa vituo hivi kwani inaamini kwamba Takwimu zinazokusanywa zinasaidia katika kuweka kumbukumbuku nzuri ya uingiaji wa Watalii Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilipofanya ziara katika vituo hivyo imebaini kwamba wanaokusanya taarifa hizi ni maafisa kutoka idara ya Uhamiaji na baadae wanazipeleka katika vituo hivyo kwa ajili ya kujaza taarifa hizo, vituo hivyo vimejumuisha wafanyakazi kutoka katika Afisi ya Mtakwimu mkuu wa Serikali na Kamesheni ya Utalii.

Kwa kuwa Utalii ni moja ya vyanzo vikuu vinavyoingiza mapato hapa Zanzibar, Kamati inaendelea kusisitiza juu ya kuimarishwa kwa vituo hivyo.

**Chumba cha Chini kwa Chini - Makangale**

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilifika huko Makangale Mkoa wa Kaskazini Pemba katika Mradi wa Hoteli ya Kitalii Manta Resort. Kamati ilitembelea mradi maarufu wa chumba Cha chini kwa chini kiliopo chini ya bahari katika hoteli hiyo ambacho kimekua ni kivutio kikubwa cha watalii.

**Changamoto Yenye Kuleta Matumaini**

Mhe. Naibu Spika, Meneja wa hoteli hiyo ameijulisha Kamati kwamba wageni wengi wanaotembelea chumba hicho wamekuwa wakilalamika kwamba wamekuwa wakilipia chumba hicho siku nzima kwa furaha, lakini huwa wanashindwa kupata usingizi kutokana na vituko mbali mbali ikiwemo samaki, matumbawe na mazao mengine ya baharini hasa wakati wa usiku.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaitaka serikali iimarishe miundombinu ya barabara na maji katika hoteli hizo ili eneo hilo lifikiwe kwa urahisi.

**Hoteli ya Bwawani**

Mhe. Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa bado kuna tatizo la baadhi ya Taasisi zilzokodi ndani ya Hoteli ya Bwawani kutokulipa kodi zao. Licha ya hatua iliyochukuliwa na Uongozi wa Hoteli ya kuzifungia Taasisi ambazo hazijalipa, lakini bado Kamati inaendelea kusisitiza kuwa wadaiwa hawa wafunguliwe kesi Mahkamani haraka iwezekanavyo, na kuchekelewa kufanya hivyo tunaweza kupoteza haki za hoteli kwani , kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo " Limitation Act" madai yote yana muda wake maalum, na muda huo ukipita hutaweza tena kufungua dai hilo mbele ya Mahkamani.

**Sekta ya Utamaduni na Michezo**

**Mgogoro Ndani ya Chama Cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*)**

Mhe. Naibu Spika, Kamati inasikitishwa sana kuwa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) kimepoteza kabisa mwelekeo wake na kimeshindwa kutekeleza majukumu yake, hii inatokana na migogoro iliyopo kwa viongozi wao wenyewe kutokufahamiana, jambo ambalo limepelekea kutokufanya kazi zao kwa mashirikiano na kugawika makundi mengine ndani ya *ZFA* ambayo yanapingana na kundi jengine miongoni mwao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaendelea kusikitishwa kutokana na kukua kwa mgogoro huo hadi kufikia hatua ya kusimama kwa ligi kuu ya Zanzibar jambo ambalo linapelekea kuondosha heshima ya Soka ya Zanzibar. Aidha pande zinazovutana zimeendelea kuukuza mgogoro huo hadi kuburuzana Mahakamani, na hadi Kamati inataayarisha Ripoti hii bado shauri hili liko Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, Kamati isingependa kulizungumzia sana suala hili isipokuwa ni kuishauri wizara kutumia hekima na busara kuzikutanisha pande zinazovutana ili walimalize suala hili nnje ya Mahakama.

**b. Wizara ya Migufo na Uvuvi**

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni miongoni mwa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo Kamati inatambua kwamba Wizara hiyo inalenga kuongeza ajira, Pato la Taifa, lishe bora na kupunguza umasikini kwa wananchi na kuwepo uhakika wa chakula kwa kila kaya hapa nchini.

**Sekta ya Uvuvi**

**Soko la Tumbe**

Mhe. Naibu Spika, wakati wa kazi zetu, Kamati ilitembelea soko la Tumbe lililojengwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia chini ya mradi wa MACEMP ambapo tayari limefunguliwa wakati wa sherehe za Mapinduzi zilizopita.

Mhe. Naibu Spika, Mkandarasi tayari ameshamaliza kazi yake na ameshakabidhi soko hilo bila ya kutimiza masharti ya mkataba wa ujenzi ambao pia ulijumuisha kuunganishwa kwa umeme katika soko hilo. Taarifa zilizogunduliwa na Kamati wakati inatayarisha ripoti hii ni kwamba, serikali imeamua kubeba gharama za kuunganisha umeme katika soko hilo ili litumike huku ikiangalia uwezekano wa kumchukulia hatua za kisheria mkandarasi huyo ambaye ameshindwa kutimiza masharti ya mkataba wa ujenzi huo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa mkataba huo wa ujenzi wa Soko la Tumbe uliingiwa kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Kampuni ya Ujenzi ya *Ngogo Engineering Ltd* katika mwaka 2011 kwa shilingi za Kitanzania 1,074,808,177/- na kwa mujibu wa maelezo ya Wizara kazi hii ilitakiwa kukamilika baada ya miezi 7.

Kamati ilielezwa kuwa baada ya kuzama kwa meli ya Mv. *Spice Islander* tarehe 10/09/ 2011 ambayo ilibeba vifaa vingi vya Kampuni hiyo kwa ajili ya ujenzi huo, makubaliano ya awali juu ya muda wa ujenzi na gharama ilibidi yabadilike na Banki ya Dunia ilikubali kazi hiyo ifanywe kwa gharama ya shilingi 712,500,000/- badala ya makubaliano ya awali ya Shilingi 1,074,808,177/-.

Hata hivyo kwa kuwa mkataba wa awali uliosainiwa haukubadilishwa, Kamati kupitia barua yenye nambari ya kumbukumbu BLW/K.10/17 *VOL*.1/100 iliomba ipatiwe maandishi ya kubadilishwa kwa makubaliano hayo ya awali. Kwa masikitiko makubwa sana, Kamati ilipokea barua kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya tarehe 25/02/2011 yenye nambari ya kumbukumbu WMU/20/3/21/VOLT ambayo ni tofauti na kielelezo kilichoombwa na Kamati. Kielelezo kilicholetwa ni barua iliyokuwa na kichwa cha habari:-

*"RE : PROVISSION CONSULTANCES FOR DESIGN AND SUPERVISSION OF THE CONSTRUCTION WORKS OF FISHLANDING SITES AT TUMBE IN PEMBA*".

Kamati iliona kuwa barua hii haihusiani kabisa na suala la kuzama kwa Meli ya *MV. Spice Islander* na kupunguzwa kwa makubaliano ya mwanzo kutoka shilingi 1,074,808,177/- hadi 712,500,000/=.

Mhe. Naibu Spika, meli ya MV. *Spice Islander* ilizama mnamo tarehe 10/9/2011 lakini barua hii ilitoka tarehe 30 Mei, 2011. Kwa hiyo ni wazi kwamba barua hii ilitoka kabla ya kuzama kwa meli.

Kamati bado inajiuliza jee kupungua kwa gharama za awali sababu ilikuwa ni kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islander* au "KULIKONI"?

**Ujenzi wa Soko Malindi**

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa Soko la Samaki la Malindi ambao ukimalizika utakuwa umegharimu kiasi cha Shilingi za Kitanzani 14,866.500,000/-, kwa sasa umesimama. Sababu kubwa ya kusimama ujenzi huo ni UNESCO kushindwa kutoa kibali cha ujenzi wa soko hilo kwa madai kwamba mchoro wa jengo hilo hauendani na majengo ya Mji Mkongwe.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa sababu kuwa khasa ni paa la mchoro huo pamoja na madirisha. Vile vile mchoro huo ulikuwa unafanana na majengo ya Kiarabu lakini *UNESCO* wametaka ufanane na majengo ya Kiengereza.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaitaka Wizara kwa kushirikiana na Serikali kuu iangalie uwezekano kwa hali yoyote ile wa kuonana au kuwasiliana na moja kwa moja na *UNESCO* ili wapewe taarifa za uhakika ni kwanini mpaka sasa hawajatoa kibali cha kuendelea na ujenzi wa soko hilo.

**Vikundi vya Ufugaji wa Samaki na Mazao ya Baharini**

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu pia ilibahatika kuwatembelea wafugaji mbali mbali wa samaki na mazao ya Baharini ikiwemo; Wambaa , Ufugaji wa Kasa Nungwi na Ufugaji wa Chaza Dimani.

Kamati iliridhika na juhudi zinazochukuliwa na kikundi hivyo vya wafugaji katika juhudi zao za uzalishaji wa mifugo na kupambana na hali ngumu ya maisha.

Mhe. Naibu Spika, vikundi hivyo vya ufugaji wa samaki, kasa na chaza Vinahitaji msukumo mkubwa kutoka serikalini na wafadhili mbali mbali ili kifikie malengo waliyojiwekea. Vikundi Vinahitaji utaalamu zaidi wa uzalishaji pamoja na malisho ya mifugo yao.

**Kilimo cha Mwani**

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilifika huko Uroa, Wilaya ya Kati pamoja na Dimani Wilaya ya Magharibi na kuonana na wakulima wa mwani wa shehia hizo pamoja na kupokea taarifa ya utekelezaji wa kilimo cha mwani katika maeneo yao ambapo wameripoti kwamba wanaendelea vizuri na kilimo hicho licha ya changamoto kadhaa zinazohitaji kufanyiwa kazi ikiwemo Bei ya Shilingi 500 kwa kilo moja ya mwani ni ambayo ni ndogo ukilinganisha na kupanda kwa hali ya maisha huku ikizingatiwa kwamba wakulima hao wanajitegemea wenyewe kwa vifaa.

Kamati inaitaka wizara ifuatilie bei ya mwani duniani kama vile inavyofanya kwa upande wa zao la karafuu ili wakulima wetu waweze kupata bei inayoridhisha na hatimai wapate mpato mazuri ya kazi zao.

**Sekta ya Mifugo**

**Shamba La Mifugo Pangeni**

Mhe. Naibu Spika, eneo la shamba hili la Pangeni ni la serikali na linatumika kwa ajili ya ufugaji wa ng'ombe, eneo hili kwa sasa lina ng'ombe hamsini (50). Kamati ilipotembelea shamba hilo ilibaini uvamizi wa shamba unaofanywa na baadhi ya wakulima wanaolima karibu ya maeneo na shamba hilo.

Kamati inaiomba wizara ianze kufatilia maeneo yote yaliyovamiwa na yarudishwe katika mikono ya shamba hilo.

**Majosho ya Konde, Mjimbini na Kituo cha Mifugo Chamanang'we**

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilitembelea vituo vya Mifugo vya Konde, Mjimbini na Chamanag'we ambavyo kwa sasa vinakabiliwa na Changamoto kadhaa zinazozoretesha utendaji wa vituo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaishauri Wizara kuwa, wakati inasuburi kupata hati miliki ya maeneo hayo ni nyema ikachukua hatua za dharura za kuyahami ili kuepusha vitendo vya uvamizi vinavyowea kutokea.

**Wafugaji Maarufu wa Wilaya ya Mkoani Pemba**

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilimtembelea mfugaji wa ng'ombe wa maziwa (Bw. Mohammed Jidawi) alianza na ngombe mmoja na hivi sasa anamiliki ng'ombe sita wanaotoa maziwa lita 15 kwa siku kwa kila mmoja huko Mjimbini. Mfugaji huyu ambae licha ya ufugaji huo anajishughulisha na kilimo cha aina mbali mbali na ameweza kupiga hatua kubwa za uzalishaji wa Mazao ya mifugo na kilimo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilifika Makhuduthu, kukagua mradi wa mtambo wa Biogas wa Bw. Hafidh Nassor ambae ameanza shughuli za ufugaji akiwa na ngombe wa maziwa mmoja (1) na hivi sasa anamiliki ng'ombe sita (6).

Mhe. Naibu Spika, changamoto iliyopo ni kwamba, baadhi ya wakati mbegu za Kupandishia zinapowafikia wafugaji hawa huwa tayari zimeharibika kutokana na ukosefu wa sehemu za kuhifadhia na wakati mwengine huhifadhiwa katika chupa za chai. Hapa Kamati inaiagiza Wizara ione umuhimu wa kuwa na mitungi ya *Liquid Nitrogen* ambayo ni portable, ili kuwa na urahisi wa kuwafikia wafugaji walioko vijijini zaidi badala ya kutumia chupa za chai.

**Uvuvi wa Bahari Kuu**

Mhe. Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba, Wizara ipo katika maandalizi ya kuanza uvuvi wa Bahari Kuu, miongoni mwa maandalizi hayo ni kuwapeleka vijana wetu huko Tanzania Bara kwa ajili ya kujifunza suala zima la uvuvi huo. Pia Kamati imegundua kwamba wizara iko katika hatua za mwisho katika ununuzi wa meli na vifaa vyengine kwa ajili ya Uvuvi huo. Kutokana na umuhimu wa suala hili, Kamati ilikwenda Bagamoyo Tanzania Bara

katika Chuo cha Uvuvi cha Mbegani. Kamati inaiagiza Wizara, iendelee kuwapeleka vijana wetu kujifunza zaidi kwani suala hili linahitaji utaalamu ukilinganisha na uvuvi wa kawaida.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamaliza muhtasari wa ripoti yetu, Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Utalii na Habari inawashukuru sana Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati hii, kwa kuweza kutoa mashirikiano makubwa ya kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa mwaku huu. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.

Hata hivyo, kasoro kubwa iliyogunduliwa na Kamati yetu ni upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini, kwamba umekwamisha kwa kiasi kikubwa malengo na shabaha za Wizara zote mbili zinazosimamiwa na Kamati hii hasa katika Miradi ya Maendeleo. Vile vile upatikanaji wa fedha za OC pamoja na vitendea kazi, usafiri na malipo ya muda wa ziada wa kazi *(over time)* navyo vimekuwa vinarejesha nyuma mwamko na ufanisi wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka 2014/2015 Kamati yetu imetekeleza jukumu lake la kuishauri na kuisimamia serikali kwa Wizarazake hizo, Taasisi na Idara tunazozisimamia kwa niaba ya Baraza lako.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru Mhe. Spika wa Baraza letu la Wawakilishi kwa kutuwezesha kutuongoza vyema katika utendaji wetu wa kazi. Mhe. Naibu Spika pamoja na wewe na Wenyeviti wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kutusaidia vizuri katika kufanikisha shughuli za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa Ushirikiano mzuri katika kufanikisha majukumu tuliyojipangia. Michango, mawazo na ushauri wao kwa kiasi kikubwa yamefanikisha majukumu ya Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Utalii na Habari.

Naomba sasa kuwatambua wajumbe hao kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Mwenyekiti. |
| 2. | Mhe. Abdalla Mohammed Ali | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Asha Bakari Makame | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mussa Ali Hassan | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Amina Idd Mabrouk | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Asaa Othman Hamad | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Kazija Khamis Kona | Mjumbe |

Aidha, kwa kipekee kwa niaba ya Kamati ninawashukuru Ndugu Himid Haji Choko na Ndugu Salum Khamis Mbarouk ambao ni Makatibu wa Kamati yetu kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati kwa kipindi chote hadi taarifa hii inapotolewa mbele ya Baraza lako Tukufu.

Napenda pia kutoa shukurani za dhati, kwa usikilizaji mzuri wa Waheshimiwa Wajumbe wakati wote wa Uwasilishwaji wa hotuba hii na tunatoa wito kwa Serikali kuyatekeleza kwa vitendo yale yote yaliyoagizwa na kushauriwa na Kamati ili kuongeza ufanisi wa Wizara hizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Naibu Spika, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia mpaka sasa hivi bado dakika zinayoyoma na ningali hai. Nikushukuru na wewe Mheshimiwa wangu Mwenyezi akujaalie kila la kheri na wewe kwenye kiti hicho upate uishi muda mrefu wenye heri na wewe na salama na wewe.

Mheshimiwa kwa kuwa hizi ripoti zinaandikwa tofauti tofauti, mimi nianze na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Tunaambiwa tujibu hoja au tuchangie hoja zilizokuwemo katika taarifa za kamati, mimi hilo sina tatizo nalo hata kidogo na ndio ilivyo. Lakini Mheshimiwa kuna hoja *same* na hiyo zilizokuwemo humu kwa mujibu wa taarifa tunayo haki ya kuchangia na tukazieleza na ndio sheria ilivyo. Hawa ni binaadamu wanapokwenda kule yanakuwa mengine wanayasahau, sisi *back bencher* tunatakiwa tuwakumbushe na tuwaelekeze, Mheshimiwa hiyo ni haki yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianzie na *ZBC*, kwanza niwashukuru sana juu leo kumejaa watendaji wote wapo niwapongeze sana na hiyo ni moja katika kuonesha umahiri na uongozi wao wako chini ya himaya ya waziri wao hilo moja niwashukuru sana Mungu awabariki na wao, ili watusikie wapi tulikosea wapi wanatakiwa msisitizo.

Mheshimiwa *ZBC* kwanza nimefurahika sana kusikia kifungu hiki hapa kinachosema Kamati iliita Wizara kukaa pamoja. *ZBC* ni sehemu ya biashara hii mimi nikubaliane nalo. Tusipokaa nao hao, tusipowalipa Baraza la Wawakilishi hatuwatendei haki na ndio maana wanaweza wakafanya vile wanavyotaka wao, kwa sababu juzi tu *camera* zilitolewa wakenda *part time* wakenda sehemu nyengine kufanya biashara yao, sisi ikwa *camera* hamna ikaja *camera* moja ikawa watu wakuoneshwa jinsi gani tunavyochangia vizuri kwa wananchi wetu, walituuliza jamani Baraza lilizimwa kumbe uhalisia tuseme ukweli, hawa watu biashara huu ukweli tukubaliane tatizo liko wapi.

Baraza lina fungu lake la fedha na wao tunawawekea kwenye bajeti, kwa nini tusiwape kwa nini tusiwaite. Mimi ninafikiria Mheshimiwa hatuwi wakali wajumbe lakini kuna mambo lazima tuisisitize Serikali na kusisitiza kwetu kuna mambo hapa inatumika jamii, vijana hawa wanakaa muda mrefu, sisi wenyewe kukaa kitako humu ndani kwa masaa tu hatuvumilia mara tunatoka tunakwenda nje. Je hawa wanakaa kama wanalinda, Mheshimiwa hili suala tulifikirie.

Mhe. Naibu Spika, labda mimi ninafikiria twende na *model* ya kisasa, kwa kuwa Baraza la Wawakilishi hatutaki kuwalipa *ZBC*, tufunge mitambo ya kisasa. Kwa sababu tunakwenda nini hapa na tutafanya nini kwa sababu ni *expensive* sana mitambo ya kisasa, jana mimi niliona mkonga ule nilishtuka, nilisema ule mkonga wa *TV* utanigonga kumbe ni televisheni.

Sasa televisheni kama zile tunazipata humu Baraza la Wawakilishi tunawangaisha nini hawa, tuna-*settle* mle katika sehemu zinazohusika vitu vinakwenda, leo tunawahangaisha, tunakaa pengine leo vikao vya ngapi hawajalipwa pesa ninafikiri sijui kikao cha nne hawajalipwa pesa maskini za Mungu hawa hawajalipwa.

Sasa mimi naomba sana tunasisitiza kwa msisitizo wa hali juu sisi watu wa *back bencher* kuisisitiza Serikali lazima hiki kikao kikaliwe na wafanyakazi wa *ZBC* waanze kulipwa, wakilipwa hawa watakwenda vizuri, hawazitoi ng'o televisheni hapa hata apate kazi gani huko hawazitoi. *Wallahi* juzi Mhe. Naibu Spika, ilikuwa aibu kubwa sana lakini si aibu kwa sababu wao wamekwenda ku-*part time* kazi nyengine nyie hamuwalipi, hiyo ni sawa sawa Mheshimiwa mimi sikupigii kelele sana.

Mheshimiwa nirejee katika mambo ya televisheni sehemu ya utangazaji, pamoja na hayo kabla sijaingia kuna kitu kimoja nisije nikakisahau, niende katika hii Kamisheni ya Utalii. Sasa niseme inaendana na ile ule umuhimu wa kuonesha ile Kamisheni. Juzi nimeenda Kamisheni katika shughuli zangu za hapa na pale lakini nusura nianguke chini kwa *tiles* zilivyokuwa nzuri, ile ndio inavyotakiwa wale lazima tuwawezeshe, tunaita Kamisheni tu lakini mazingira yake hayaoneshi kama haya ni mazingira ya utalii.

Kwa kweli niseme nimefurahi sana nimeona sasa nimedhamiria kweli pamoja na bajeti finyu hii sipendi tena kuitaja lakini inanibidi niseme pamoja na jitihada za bajeti finyu wamejitahidi kujifinya. Sasa hivi lile jengo zuri sana, wakati mimi nilipokuwa Mwenyekiti sikukuta hali ile lakini sasa hivi *alhamdu lillahi* nimshukuru sana Mwenyekiti wa sasa hivi anayeongoza hili suala nimpe pongezi kubwa anaitengeneza vizuri, sasa ile ndivyo inavyotakiwa Mheshimiwa.

Mheshimiwa hapa wanatakiwa wawe wanaendeleza katika matangazo na ni kweli kwa sababu tofauti wenzetu wanapokaa Bara, wanavyotangaza na sisi kwa sababu kutokana na ile bajeti yenyewe. Mimi ninafikiria kuna mambo yaliyokuwa ni muhimu kwa sababu hii ni moja katika kianzilishi cha kupatia fedha kitengo hiki, cha kuitangazia Zanzibar jinsi gani kina sifa za utalii na tuna mambo gani na gani ya kuweza kuja.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana pamoja na ufinyu wake wa bajeti, hebu tujitahidi sana Mheshimiwa kuwatafutia fedha kwa hali na mali ili waweze kufikisha pale ambapo panapotakiwa na matangazo yetu watu wakaja kututembelea, wakaja kutufanyia mambo ambayo ya kuweza kututilia fedha za kigeni.

Mhe. Naibu Spika, hapa pana masikitiko walikuwepo vijana walinzi wa KVZ kwa kweli hawa ndio walianzisha kulinda sehemu zilizokuwa za utalii, lakini kwa bahati mbaya Mheshimiwa kwa kuwa leo si pahali pake ninangojea kwenye bajeti, hawa watu nasikia wameondoshwa bila kupewa taarifa nzuri, wamerejeshwa kwenye vikosi wamepelekwa wengine.

Sasa mimi ningeomba kidogo uje uni-*brief* tu sababu gani iliyopelekea kufanyika *exchange* ya haraka na hawa watu ambao tayari kama ni *contract* na nyinyi, kidogo mimi naomba nisaidiwe maarifa ili tuweze kujua kabla huko kwenye bajeti kwa sababu huko ndio kunako maelezo zaidi kufika kuliko hivi sasa. Hapa sasa hivi mimi natilia mkazo masuala.

Mhe. Naibu Spika*, ZBC* ilishauriwa iwe makini baadhi ya watangazaji wake ambao mara nyingi sana huwa wanakosea kosea na kutamka na nini sio hao tu. Nina masikitiko makubwa sana na jilo mimi siku zote huwa bahari sipendi kuficha bahari. Lakini nimshukuru sana Mkurugenzi inaonesha mna wafanyakazi wengine hata zile kauli za Wakurugenzi wao wakubwa wao hawazithamini, hili jambo Mheshimiwa linasikitisha sana. Leo wewe unaagiziwa na Mkurugenzi wako kuna jambo la Mheshimiwa *wallahi* mimi sijapata kuona nchi hii. Sijui sheria zetu maana siku nyingi sana ninasema, na sisi unajua tunajishusha hadhi wenyewe watu wa *back bencher,* nataka nikwambieni. Kwa sababu tunakuwa ule ukali wetu tuna-*withdraw sometimes* tunapunguza makali mpaka wanafika hawa wafanyakazi wadogo wadogo, wanatudharau hawatufahamu kama sisi ni nani.

Kwa kweli hili suala linasikitisha sana. Mimi ningeomba Mheshimiwa hebu toweni taaluma sasa hivi itabidi sasa mkatoe taaluma, kwa sababu kuna wakubwa wengine utawapigia simu sisi hatupigi virungu bwana hata siku moja. Hatuwapigii simu wakubwa kwa kuwa labda tunataka kukupigeni virungu, tuna jambo tunataka kukupa indhari. Lakini waheshimiwa wakubwa mnakataa simu zetu hamzipokei nalo kosa hilo, ukija mripua hapa anasikitika anakuona mbaya sana, kumbe anasahau kama wewe ulimpigia simu.

Kwa kweli Mheshimiwa hili suala linasikitisha sana na kamati wameona hapa dharau wacha kutamka maneno. Lakini ndio maana nikasema kuna mambo mengine yanalingana na hii *statement* hapa kuwa wanadharau hata amri, wanadharau ujio wa kuja mkubwa, lakini hatuji kama ukubwa wa kutisha jamani, tunakuja kutokana na sheria zilivyo. Wao wakitaka wasitake mimi mkubwa, mkubwa tu tofauti na wewe. Lakini wewe weka sheria tukiweko mitaani tutasongamana lakini ninapokuja *field* au ninakuja na tatizo pale basi niwekee heshima kwa mujibu ya ile sehemu yenyewe inayohusika.

Mheshimiwa, hilo nimeona nilieleze kwa masikitiko makubwa sana kuwa kitendo hakiridhishi hata kidogo. Nikimalizia kwa hii ya habari nirudie hapa suala la Hoteli ya Bwawani, Hoteli ya Bwawani kwa kweli kuna Ofisi ninakubaliana na wewe hazilipi, kwa nini sasa kuwa hiki ni chombo cha Serikali lakini kina sehemu yake.

Hoteli ya Bwawani ya Serikali lakini hii sasa mimi jamani hebu tuondokane na ile Ofisi kuzitia kwenye hoteli si vizuri, mazingira mengine hayawi mazuri. Ndio juzi nikasema choo kinakwenda kufanywa Ofisi ni sawa sawa na hii, ile hoteli ni hoteli lakini huwezi ukaifanya kama ni Ofisi, jamani haya mambo mengine jamani Mhe. Waziri naomba uwaelimishe watu twende na wakati, hoteli ziwe hoteli tu, Ofisi ziwe Ofisi, choo kiwe choo kisiwe Ofisi ndio watu wanavyokwenda hivyo.

Sasa mimi ninafikiria hili suala tusiwape ulimwengu watu wakatucheka kwa sababu ile sijui niite *5 Star* au niite *4 Star* sasa nitaita *0 Star* haina hata hadhi ya *6 Star* ile haifiki. Kwa sababu leo mna maofisi mule ya aina mbali mbali, maji hamna mule hayapatikani, enzi za Bwawani jamani mlikuwepo wapi Bwawani Hotel.

Hoteli ya Bwawani si mchezo wakati ule si masihara. Nimewahi kuona mimi katika kula chumvi yangu nimewahi kuona ile Bwawani, wakati ule Bwawani sio leo, hatari tupu. Mbu wake ninafikiri anakupiga kikumbo unaanguka chini.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoteli ile ya Pemba *Bar*, ile hoteli ilikuwa ikiingiza ikikusaidia yale mapato lakini mpaka leo kimya kulikoni nini Mheshimiwa, tatizo ni nini naomba uje kunambia hata mpaka leo haieleweki haijafunguliwa, hakuna nani kama kuna mtu kaiba hujamfunga sijui kuna nini Mheshimiwa, hebu tujaribu kutueleweshsha.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina wazo ninamuomba sana Mhe. Rais anisikilize.

Mhe. Naibu Spika, kuna jambo ambalo kwa mujibu wa sheria, ni sheria tuseme lakini sheria unakuwa unaiunda iwe sheria. Mhe. Naibu Spika, wizara hii ndio inayo-*deal* na mahoteli, lakini kuna kitu kinakosekana ndani ya sheria hii, kinakosekana chombo ambacho kitaweza kwenda na wakati.

Mhe. Naibu Spika, ningependelea sana hii Kamisheni ya Kazi ingepelekwa kwenye utalii, kwa sababu hawa wana majengo lakini sheria iko wizara nyengine sijui niende wapi. Hawa wana-*control* wale watalii kwenye majengo yao, utendaji wa sheria uko katika *department* nyengine. Sasa hapa kidogo inanisikitisha sana, Mwanasheria hebu na hili tuliangalie umbali huu wa sheria wa chombo hiki, mimi nitoke hapa kwa kufuata Idara ya Kazi hukoo wakati ningekwenda hapa mimi ningefika na ningewakuta nikawaambia wananchi wangu nimefukuzwa kwenye mahoteli. Ni jambo ambalo linasikitisha sana mwambieni Rais hana tatizo, tatizo lenyewe Rais wangu kila akikua na akili zinakuwa vizuri, kwa sababu anaona jinsi ambavyo tunavyochangia watu wake.

Hili kwa kweli linasikitisha sana, naomba sana Mhe. Waziri unapokwenda kwenye bango kitita mwambie Mhe. Rais na mshauri Mhe. Rais hakatai ushauri, watu wanadhalilika, watu wanafukuzwa kwenye mahoteli, kwenye ardhi yao masikini za Mungu wanatimuliwa.

Kwa hiyo, mimi naomba sana hii sheria iwaangalie kwa mfano mimi naweza kusema hilo suala la viwanda nitakuja kulingojea kwenye Wizara ya Fedha huko, lakini na wewe utalii wako huo uulinde utakosa *market* kwa sababu tayari huku watu wanadhalilishwa mwisho watu wataondoka, watu watakataa kufanya kazi au watakuwa wale watalii hawawapati au kuandaliwa vizuri. Kwa hiyo, mimi niondoke huko ili kwa kufika pahala hatimu naingia kwenye mifugo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mifugo mimi mara nyingi sana na hasa hasa nimshukuru sana Mhe. Waziri mpya au waziri aliyewachia mifugo hii na *Hansard* zangu nilikuwa nikieleza, kwa sababu mara nyingi sana sipigi maneno pumba nazungumzia kitu kilichokuwa nimekiona na kitaweza kuwasaidia wananchi. Nilitoa rai jinsi gani ya ufugaji wa samaki wa juu, nilitoa rai sana na nilikuwa msimamizi mkubwa nikipiga kelele, mheshimiwa wangu akaniambia tulia nikamtafutia kijana mmoja akampeleka China ili akajifunze jinsi gani watu wanavyofuga samaki. Kwa bahati mbaya mwananchi yule sikuonana nae mimi kuweza kunifahamisha, lakini kwa kuwa hili jambo nina hamu nalo na mimi nina hamu kwa sababu uvuvi wa juu Mhe. Naibu Spika *wallahi* unaondoa umasikini.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema kuna bwawa la samaki Unguja ukuu amenitaja mimi njooni, nikufundesheni utaalamu nimefuga samaki mimi elfu na mia tano kabila ya tilapia kwa sababu angeniambia nijiandae ningekuonesheni samaki wazuri, samaki watamu.

Mhe. Naibu Spika, leo hii mimi nikikusa kura hapo aaah nakwenda kuvua uvuvi tu basi, nachukua nauza samaki bila ya wasi wasi. Na ukiambiwa samaki hao ni wa maji baridi utakataa kwanza *design* yao kama changu tena ni wazito na ni watamu, huwezi amini.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakusudia kumwambia Mhe. Waziri baada ya mimi kuona lile bwawa moja Mhe. Waziri sasa hivi nina bwawa jengine linaingia samaki elfu mbili tayari nimeshatengeza twende ukalione kwa ile hamu na jazba ilivyonijia hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, naiomba sana serikali yangu kupitia wizara hii ituwekeze watu tuliojitolea wanipeleke China basi na mimi nikasome, nikaone jinsi gani watu wanaendelea na uvuvi wa aina nyengine. Kwa hivyo, hilo suala sio dhambi kabisa kwa sababu niliishawishi wizara ikashawishika sasa jamadari mwenyewe Jihadi anakwenda mbio na Naibu wake, wanakwenda *field* kabisa kabisa wanaona ule ukweli na hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, mimi nawashukuru sana na niwapongeze sana kwa jitihada zao kabisa pamoja na wataalamu wao.

Mhe. Naibu Spika, hili suala ni zuri sana hasa kwa jamii kwa sababu leo bahari ni bahari inaweza ikachafuka na hasa kwa vile hatuna vile vyombo kwa sababu juzi hao walikwenda kuangalia Chuo cha Uvuvi. Wenzetu kule boti

moja ya uvuvi bilioni sisi ndio kwanza tuna milioni mia tano na ziko wapi milioni mia tano? Hebu njoo Mhe. Waziri uniambie hii milioni mia tano ziko wapi za boti ya uvuvi ya Zanzibar, unazo njoo uniambie Mhe. Waziri ziko wapi? Na kama zipo twambieni tuongeze ngapi panapobakia, harambee watapiga harambee tutakata bajeti kidogo kidogo kuna mambo mengine kwenye bajeti si muhimu. Tunazitoa tuziweke vile lakini tupate boti inayokwenda katika mkondo wa bahari kuu. Mimi naomba sana mheshimiwa hilo liweze kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, jamaa ananiulizia hapa ananiambia *DNA* basi, namwambia aah, iko pale pale *DNA* nishaambiwa zilipo nitakuja kulisema huko mbele zilipo *DNA* nishazijua.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna jambo la masikitiko hapa nataka niiombe serikali, nimuombe Mhe. Waziri, nimuombe Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili. Mhe. Naibu Spika, kuna shamba ambalo walieleza shamba la Pangeni ni kwamba Mhe. Waziri alieleza na hasa kwenye *package* yake kwa kuwa hili shamba lilikuwa halina miliki, lakini ameeleza historia ya huko nyuma amesema kuna watu wengine wamelipwa mijiti yao kumbe wanalipa wao mijiti kumbe wao hati hawana.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Waziri sote waungwana, sote binadamu serikali lazima ifike pahali ione huruma, sio sehemu kubwa sababu mheshimiwa tangu nakumbuka mimi kufahamu kule, kwa sababu kule ni maeneo ya kwetu *wallahi* kulikuwa na ng'ombe wawili mpaka leo hii nimekuwa mtu mzima. Halafu leo tunakwenda kuwanyima wananchi wameshapanda miembe, wameshapanda minazi wanavuna.

Mhe. Naibu Spika, watu wa Pangeni hatuwatendei haki naomba sana Mhe. Waziri tukae pamoja hata kwenda kwa Rais kwenda kumuomba jamani Mhe. Rais si mchoyo tatizo lenyewe, tunamuogopa tu kumuendea, hebu nipeni ruhusa mimi niende kama Rais nimwambie si nitamuomba. Nitamuomba na nitamwambia Mhe. Rais yah, nitamuomba siendi kumtukana eti lakini siipati nafasi nimeiomba nafasi hiyo kwenda kwa Rais tangu sina mvi mpaka sasa hivi naingia mvi sijapata kumuona Rais wangu.

Ni jambo ambalo linanisikitisha sana na linanivunja moyo, yule mimi ni Rais wangu mimi ndio mtendaji wake katika Baraza hili, lazima nikae nae na nizungumze nae siendi kumuomba kitu jamani mimi simpigi kirungu. Ninachokwenda kule ni kubadilishana nae mawazo Mhe. Naibu Spika mimi nina fikra, pengine mimi nina fikra kuliko waziri mwengine, fikra ninayo ya kumsaidia yeye tatizo liko wapi sijampata Mhe. Naibu Spika, labda leo atanisikia kesho atanita.

Naomba sana najua eeh mimi nishaomba sana kwa sababu sisi ni kitu cha kawaida tu, *wallahi* mimi siku moja nikikwambieni jambo nyinyi mnafikiri *joke*. Nilipokwenda Marekani nilikuta *queue* ya watu nikasema na mimi nijiingize. Nikajiingiza maana yake nimeshuka pale kile kituo changu mimi cha basi *tourism* limeishia pale Ikulu, basi nikaona watu wako kwenye *queue* na mimi nikaingia, kufika pale nikaambiwa *stop*. Nikauliza kwa nini unanisimamisha, akaniambia hawa watu wana *information* maalum ya kukubaliwa waende wakazungumze na Obama. Nikasema *alhamdulilah* nilishukuru pale wenzangu wanamuona Obama mimi Dkt. Ali Mohammed Shein nakosa kumuona. Si masihasara Mhe. Naibu Spika, niliona wivu nilikaa kimya kama niliyeonewa hivi jamaa hao wanapita wanakwenda zao *White House*, nimekaa nje wenzangu hao wanakwenda zao.

Sasa ingekuwa naingia bango kitita ningemuona lakini haturuhusiki sisi waheshimiwa kuingia kwenye bango kitita labda tugeuze sheria, sasa tugeuze sheria wawakilishi wa kamati nayo hiyo Mwanasheria hebu iangalie, tujaribu kuangalia sheria wana kamati tuingie kwenye bango kitita *wallahi* itakuwa nzuri sana. Mimi naamini itakuwa nzuri *is not joking,* si masihara tuingizwe na sisi mle kwenye bango kitita kamati *are you serious?* Kabisa tutaweza kusaidia lile suala kwa mheshimiwa wala hampati tatizo. Hatutogombana tena *backbencher* na mawaziri, hatugombani kwa sababu kwenye bango kitita mtatudanganya kwenye *paper* tukiondoka pale tumesharidhika tuna ugomvi gani tena pale.

Mhe. Naibu Spika, itakuwa hatuna ugomvi sasa mimi nafikiria niombe sana hili suala linakubalika tuweze tuwapunguze na tuwape zile sehemu kwa kuwa sasa hivi mnataka kuomba hati, kabla hamjapewa hati jamani wale watu wameumia sana, wakati ule ulikuwa msitu…

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa nimeshakupa dakika 30 sasa malizia dakika 5 kwa heshima.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante nakuheshimu sana Mhe. Naibu Spika, namalizia.

Kwa hivyo, mheshimiwa suala hili mimi limenisikitisha sana ninaomba sana Waziri na Naibu Waziri, Makamu wa Pili ambaye ni katika sehemu yake hebu tulivalie njuga tuwape hiki kijisehemu tuna hasira gani jamani, hatuathiriki kitu kijisehemu kidogo, mashamba yenyewe madogo sisi tuna shamba bahari. Maana yake shamba lake ukitizama hapo kuanzia hapa Chukwani mpaka Kwahani mbele kule ndio ukubwa wenu nyie, wale wana kijisehemu kidogo hebu tuwapeni jamani. Mimi ninaomba sana hili suala tukisema sisi serikali hatutoi, hatutoi yule mwananchi tutakuja kumvunja moyo, na ndio serikali yake hii.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika kwa kujali wakati wako ninaliomba sana suala hili tukae mimi nakuamini Mhe. Waziri, nimekusifu hapa uingie imani na wale wananchi, Mhe. Waziri uingie imani na wale wananchi. Twendeni tukakae pamoja na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya na Makamu wetu wa Pili tulifanye hili suala tuone jinsi gani mimi naamini ikifika pahala pakuwasaidia mtaweza kuwasaidia la mkikusudia kuwabena *famani-lahi* mimi huyo nishaukwepa msahafu zamani. Nishawasaidia, nishapiga kelele sasa ni jukumu lenu nyie, mimi sina jukumu. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika naunga mkono ripoti ya kamati. Ahsante sana.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji wa pili jioni hii ya leo, na sitozungumzia sana, nitakwenda moja kwa moja katika *paper* hii ya kamati pamoja na maagizo ya kamati na utekelezaji wa wizara.

Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja nataka niende katika ukurasa wa 5, agizo Nam. 3.

Mhe. Naibu Spika kamati iliagiza namna ya kutoa taaluma lakini kinachozungumzwa hapa ni kwamba taaluma za vikundi vya ufugaji. Sasa taaluma ni sehemu moja Mhe. Naibu Spika katika kusaidia wananchi wetu, lakini mimi nataka niiulize Serikali namna gani imejipanga kuwasaidia wananchi katika suala zima la kuwapa mifuko. Kwa sababu mtu anakwenda kuchukua taaluma lakini kama hana mifugo sijui taaluma hiyo itamsaidia vipi. Sasa mimi nataka kujua tu namna ya serikali ilivyojipanga katika adhma nzima ya kuwasaidia wananchi wetu, kuwapatia mifugo ili baadae hiyo taaluma iwasaidie kwa hiyo mifugo yao.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini niseme hivi? Sababu ya kusema hivi nafikiri tuna *reference* hapa kwamba hii wizara iliwahi kuja na mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe na waziri hapa akija atanisaidia mradi ule baada ya kumalizika maendeleo yake yakoje, kwa sababu ilikuwa kopa ulipe. Sasa ni ng'ombe wangapi ambao waliolipwa na unaendelea vipi katika kuwasaidia wananchi waliokuwa wanyonge katika vijiji vyetu vya aina mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi kirefu pamoja na kwamba mradi ule ulimalizika, lakini maana ya mradi kumalizika sio kumalizika kabisa kwa utekelezaji wa mambo yale. Mradi umalizike lakini hatua zinapaswa ziwepo kwa wale ng'ombe ambao wanalipwa fidia. Sasa mimi nataka kujua tu Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze nini maendeleo ya mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe ili zile taaluma zinazofanyika ziweze kusaidia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo nataka kulizungumzia katika ukurasa wa 7. Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 7 agizo la 8 naomba ninukuu kidogo tu Mhe. Naibu Spika.

> "Kwa kuwa wizara haina hatimiliki katika shamba la mifugo la Pangeni ingawa linamiliki kwa muda mrefu, sasa kamati inaagiza wizara kutafuta hati".

Jawabu limekuja chini hapo kwamba limeshatumiwa miaka 50 iliyopita.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi natapata kigugumizi sana kwa hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Naibu Spika, napata kigugumizi tatizo kwa nini inakuwa liko kwao tu, mashamba yote ya mifugo yamekuwa yakivamiwa na kama utaangalia kwa wao inakuwa ni masikitiko tu. Hata ukija ukiangalia katika suala la ukurasa wa 4 wanalalamika vile vile na wamesema kwamba wameshapeleka ripoti mpaka kwa Makamu wa Pili, lakini imeshindikana shamba lile wananchi kuondoka eneo la Maruhubi wale watu kuondoka kutumia eneo lile na linawapelekea maana kutokuleta kutekeleza majukumu yao vya kutosha.

Sasa mimi nakuwa napata mashaka kwamba tatizo usimamizi, tatizo wao wenyewe maana yake kwamba labda sasa hivi wameshaondokana na suala la ufugaji wamekwenda katika nadharia nyengine.

Hata kama watakuwa na nadharia ya ufugaji Mhe. Naibu Spika basi ile milki yako bado uwe nayo, tumepiga kelele sana katika suala la Tunguu na sijui hatma yake Mhe. Naibu Spika imefikia wapi kama limerejeshwa na kama limerejeshwa au kama lishapimwa na kama limepimwa nani kapewa. Mimi nafikiri atakapokuja Mhe. Waziri itabidi tuje tumuulize shamba lile kama limerejeshwa amepewa nani mpaka sasa hivi. Lakini sasa tunaanza kupata mashaka na maeneo mengine sasa hivi wanakwenda hivyo hivyo hatujui shamba la Kidimni nalo litakuwa liko katika hali gani.

Kwa hivyo, inavyoonekana ile dhamira hasa ya kuwasaidia wafugaji, ile dhamira hasa ya kuweka maeneo maalum kwa ajili ya ufugaji inaondoka. Sasa kama inaondoka ile dhamira ya kuweka maeneo maalum ya ufugaji sasa sijui hii Wizara ya Mifugo itakuwa inafanya nini Mhe. Naibu Spika.

Sasa mimi hili lilikuwa ni langu lakini la mwisho katika suala hili pia la maeneo haya ya viwanja, basi mimi ningewashauri wizara kama eneo la kupandisha ng'ombe sindano Maruhubi kama imeshindikana na wameshafika kwa Makamu wa Pili kutoa taarifa na imeshindikana watu wa pale kuondoka. Sasa mimi nawashauri watafute eneo wahame kwa sababu itakuwa yale majukumu yao hawawezi kuyafanya, athari zinakuwa zinatokezea basi mimi ningewashauri watafute eneo la mbali wahame na lile eneo nalo basi walitoe kwa serikali ili lifanyiwe shughuli nyengine. Vyenginevyo itakuwa ni ugovi tu wanabishana wao na wananchi, wananchi hawataki kuhama, wao kazi zao haziendi na kazi zao wanasema kwamba haidhuru kuingiliana na masuala ya kijamii, athari ya upandishiaji unakuwa na matatizo.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nina ushauri huo kwa serikali kama imeshindikana hiyo basi lile eneo walitoe nao watafute njia lirejeshwe ardhi na ardhi watafute pahala lipimwe ili liweze kufanyika shughuli nyengine za kijamii, vyenginevyo Mhe. Naibu Spika itakuwa halitokei tena. Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumze hilo tu katika Wizara ya Mifugo.

Mhe. Naibu Spika, jengine nataka nizungumzie katika suala hili la Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Katika wizara hii nina mambo kama matatu. Sina mambo mengi sana leo na leo ninajitahidi kujaribu kuishauri serikali na kuiagiza katika yale mambo mbali mbali. Kwa sababu watu walikuwa wanapiga kelele sijui watu wanataka unaibu waziri aa, hatutaki kitu, tunaisaidia serikali kwa pale ambapo tunahisi kuna haja.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa tatu (3) mimi napata mashaka na utekelezaji wa wizara na Mhe. Waziri atakapokuja ajaribu kutusaidia. Sasa hivi tukitaka tusitake pamoja na kwamba vyombo binafsi vinapiga hatua kubwa sana lakini na sisi kama serikali lazima tuwe na mipango mizuri ya kutoa ushindani kwa vyombo hivi binafsi.

Mhe Naibu Spika, sasa hivi Zanzibar itafikia pahala mwisho wananchi watakuwa hawapati taarifa za nchi yao, kwa sababu kumekuwa kunajitokeza ushindani katika majumba. Ukifungua televisheni ya Zanzibar, *ZBC* basi watoto wanahamaki sana katika majumba wanakwambia baba hiyo ondosha hamna kitu, huna unalolijua yaani tumepoteza mwelekeo kabisa. Tumepoteza mwelekeo katika kupanga vipindi, tumepoteza mwelekeo hata katika nadharia yaani hata sijui useme vipi Mhe. Naibu Spika, watu kabisa hawaitaki redio wala televisheni ya Zanzibar kwa sababu ya mtiririko mzima wa utangazaji wao.

Sasa wakati mwengine sisi wengine tunakuwa tunafuatilia mambo muhimu, wakati wa taarifa ya habari mtoto anakwambia fungua *ITV* maana yake unapewa tukio la papo kwa papo, inaweza kuwa mvua zimenyesha haraka maji pahali fulani yameingia, lakini leo hii sijui hata kama hiyo *ZBC TV* Zanzibar imeonesha angalau mafuriko tangu mvua zimenyesha. Tumeshaona *TBC* wameonesha mafuriko ya Kijangwani pale lakini hapa kwetu hii televisheni inafanya kazi gani.

Sasa hilo ni suala ambalo linafika pahala watoto wadogo wanasema weka habari muhimu. Kwa sababu kuna maeneo yanakuwa yana umuhimu kwetu sisi kama wanasiasa, sasa wewe unataka kufungua televisheni mwanao hataki *channel* ile mnakuwa mnagombana na mtoto kumkera unakuwa huwezi inabidi umridhie matokeo yake habari muhimu zinakuwa zinatupita.

Mimi napata mashaka sana hata katika huo ukurasa wa tatu (3) kama utausoma mwisho hapo katika kifungu cha 1 wanaelezea kuna baadhi ya vitu naomba ninukuu.

> "Katika kipindi hiki kinachoendelea Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia Shirika la Utangazaji *ZBC* imeweza kuweka majenereta katika vituo vyake mbali mbali vikiwemo Rahaleo, *Studio* ya redio *Karume House*, Kituo cha Televisheni Masingini na Kituo cha Kurushia matangazo ya televisheni Dole.
>
> Kituo cha kurushia matangazo cha Bungi katika mnara wa kurushia matangazo genereta limefanyiwa matengenezo na linafanya kazi vizuri, isipokuwa shirika linatafuta *wire* maalum kutoka kwenye jenereta hadi kwenye mitambo ya studio".

Mhe. Naibu Spika, mimi napata mashaka *wire* huo ni wa aina gani, unagharimu kiasi gani, unatoka nchi gani kwamba shirika zima linatafuta *wire* kutoka katika eneo moja na muda gani *wire* huo utapatikana. Mimi ndio nikasema kwamba bado hatujawa *serious* katika mambo yetu na utekelezaji wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi napata tabu sana na utendaji huu, sasa sijui ndio katika yale yale kwamba ah, twende tu mpaka limalizike, lakini namna ya utendaji wa taasisi zetu mbili hizi za *ZBC TV* na *ZBC Radio* bado kuna haja ya kufanya mikakati ya kutosha. Hili hata wafanyakazi wenyewe inafikia pahala linawarejesha nyuma na nilizungumza mwaka jana niliwataja wafanyakazi kwa idadi hapa namna tunavyokuwa na watu wazoefu, watu wenye uwezo, lakini namna ya kutokuwatunza na kutokuwapa vitendea kazi vya kutosha.

Kwa sababu mwandishi kama hujampa vitendea kazi unamkosesha sifa zake, inabakia tu anaendelea kuulizwa huyu ndiye mhariri gani, lakini hana zana. Matokeo yake ndio ya akina Marin Hassan na wengine watu ambao walikuwa wanatuvutia hapa tunapenda vipindi vyao. Tunapenda *speech* zao wote, wametukimbia. Sasa nikawa najenga hofu kwamba tutafikia pahala waziri atakuwa hana mtangazaji pale hata siku moja, itabidi sasa aanze kutafuta watu akamatie kamatie aendeshe taasisi yake. Kwa sababu watu hawana *mood* ya kufanya kazi, haya mambo ya kuchukua habari yanataka zana, yanataka vifaa.

Mhe. Naibu Spika, leo ukienda *studio* huko *camera* watu wananyang'anyiana; nina ushahidi wa kutosha nimeupata juzi Jumamosi nataka waandishi naambiwa mpaka warudi *Grand Palace* sijui *camera* hakuna. Haya ndio mashaka yenyewe ya nchi hii, yaani chombo cha serikali kinataka kutangaza habari ili jamii isome kitu tunachokifanya lakini hali ndio hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nataka niangalie ukurasa wa tano (5) na Mhe. Waziri namuomba aangalie sana. Kamati iliagiza kutoa kipaumbele kwa ununuzi wa vifaa vya kisasa hasa vipaza sauti kutokana na umuhimu wa idara.

Mhe. Naibu Spika, sifa za serikali hapa idara imeweza kununua vifaa vya vipaza sauti kama spika mbili, *stand* moja, *wire* wa *microphone roll* mbili, mabomba mawili. Sasa nilikuwa nasema pale pale kwamba bado kuna haja ya kujipanga hivyo umenunua *stand* moja Zanzibar nzima, mjini na vijijini itafanya kazi vipi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba sana wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo mimi katika mtu ambaye ananipa matumaini ya utendaji wa kazi ni Waziri wa Habari na sijasimama hata siku moja kumkosoa katika utendaji wa kazi, lakini napata mashaka na namna ya taasisi ilivyo na nampa pole katika hali hii ya utekelezaji katika taasisi yake.

Mhe. Naibu Spika, nimesema sina mengi ambayo ya kuchangia katika wizara hizi mbili, lakini zaidi nataka niseme tu kwamba, tusipofikia pahala tukawa na mipango madhubuti basi hatimaye *ZBC Radio* na *ZBC TV* Zanzibar itakuwa haina msikilizaji, itakuwa inapita hewani kama upepo.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nataka nizungumzie niliona katika kabrasha hii ya wizara ukurasa wa 14, mashirikiano ya chama cha mpira wa miguu Zanzibar, *ZFA* pamoja na wizara. Wameeleza sina haja ya kusoma na wamejinasibu namna wanavyoshirikiana na taasisi hii. Mimi hapa nimuombe Mhe. Waziri tu kwamba kama kuna mashirikiano basi azidishe, utata uliojitokeza karibuni kwa viongozi wa *ZFA* na kufikia pahala kupelekana Mahakamani suala lile limewa-*cost* vilabu vingi vya Zanzibar na vimerejesha nyuma suala la mpira wa miguu Zanzibar. Limewatia hasara wafadhili wengi ambao walikuwa wanavifadhili vilabu na sitegemei kama hasara walizozipata vilabu vile, serikali au chama cha mpira kama kitaweza kurejesha gharama za vilabu.

Mhe. Naibu Spika, mpira sasa hivi Zanzibar umekuwa kama kichekesho tu kwamba ah, kama suala la mpira lipo duniani na sisi tunalo limalizike basi, hatujaona dunia nzima mpira ukasimama kwa muda wa miezi mitatu. Ligi inasimama miezi mitatu watu wanasubiri vurumai zimalizike, ili baadae uambiwe ligi iendelee tena. Wachezaji watu waliowachukua wamewarejesha, gharama walizozipata hawajui wazifanye nini.

Sasa mimi hapa namuomba Mhe. Waziri kama kwamba kuna mashirikiano basi ayazidishe kwa sababu watu wengi kwa kipindi kirefu bado walikuwa wanaona serikali hawajaisikia kuzungumzia suala la kusimama kwa ligi, suala la kuvutana na kupelekana Mahakamani serikali kuingilia kati mgogoro ule na wakatafuta suluhu ili chama cha mpira kiweze kufanya kazi.

Tumewasikia sana kwa muda mrefu wadau ambao walijitokeza wakajiita sijui wapenda mpira, wao ndio waliokuwa wakiendesha makongamano. Wao ndio waliokuwa wakijaribu kupata ushauri kwa vilabu au kupata ushauri kwa waliofungua kesi Mahakamani hatimaye suala lile limefika pahala pazuri.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kwamba mashirikiano haya ya serikali na Chama cha Mpira yawe karibu ili mpira upate kurudi katika hadhi yake na sisi Zanzibar angalau tujitangaze. Katika hili pia nimuombe Mhe. Waziri kwamba sasa hivi umejitokeza mpira ule wa *football* wa ufukweni. Sisi kama Zanzibar sijui tunashiriki vipi kwa sababu suala lile linatangaza nchi ili kueleweka katika nchi za wenzetu juu ya suala zima la mpira wa soka la ufukweni.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja, ahsante sana.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa jioni hii na mimi kunipa fursa ya kuchangia mchango wangu mdogo sana katika wizara hizi mbili. Nataka nianze kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, katika agizo namba 5 wizara inasema imehamasisha uwepo wa ufugaji wa samaki wa maji baridi pamoja na kuwapa kipaumbele na mashirikiano kwa wale wote wanaoanzisha ujasiriamali na kupata misaada ya chakula na samaki.

Mhe. Naibu Spika, kama kuna pahala ambapo kuna watu walihamasika katika ufugaji wa samaki hawa wa maji baridi basi ni ndani ya wilaya yangu ya Wete. Wilaya hii ina mabwawa mengi sana ya samaki hawa na nathubutu kusema ni waanzilishi, ndani ya Jimbo langu la Ole kuna bwawa moja kubwa ambalo ni bwawa la mfano watu wengi wanakuja wakisoma kutoka hapo, jimbo la Mtambwe kuna mabwawa ya kufugia samaki hayapungui saba na wengi wao wakiwa ni wanawake kwa kufuga samaki, paa, wanafuga mpaka majongoo.

Sasa katika hili la wizara kuwapa misaada ya chakula na vifaranga Mheshimiwa hawa watu wanapata tabu na wanahangaika sana katika kutafuta vifaranga hivi, vifaranga vinawapa tabu havipatikani. Sasa ni kweli hili suala mwanzo wa kuja lilikuja kwa nguvu kubwa na watu wakalipokea wakaitikia mwito ule, wakafanya jitihada zao zote nguvu moja, mwanamke mwanamme kuchimba mabwawa yale, kutafuta wahisani wanaojua wakaja wakakagua na kuwaona kwamba tayari kile kima kinachotakiwa kishafikia. Wakafanya kufuga kwa muda mfupi lakini kutokana na kutopitiwa na uongozi wa wizara na kuwakagua kwa kuwapa angalau motisha, basi watu wale wamevunjika moyo kiasi kikubwa na lengo lile alilolitangaza Mhe. Rais hasa halikufikiwa.

Kwa hiyo, naiomba sana wizara katika hili wawahurumie wale watu wote waliopoteza nguvu zao katika majimbo yote yaliomo ndani ya Wilaya ya Wete katika kufuga. Ninamuomba Mhe. Waziri akipata muda hebu azunguke kule Pemba aje na nifuatane naye nimpeleke katika vikundi hivyo angalau akavione avisaidie japo kwa ushauri.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Idara ya Habari kwenye Kamisheni ya Utalii agizo namba 7, kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii, wawekezaji na mali zao. Mimi hapa nitakuwa na masikitiko makubwa mno, nasema hivi kwa sababu utalii ni utalii kwa wote ndio utalii uliotangazwa, tunategemea utalii ndio sekta inayotuingizia mapato ndani ya nchi yetu. Sasa mimi natoka ndani ya Wilaya ya Wete ambako kuna visiwa kikiwemo kisiwa cha Fundo na kisiwa cha Uvinje.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme wiki mbili zilizopita niliitwa na wanawake wa visiwa viwili hivi wakanilalamikia malalamiko yao mengi sana kuhusu ujenzi wa hoteli mbili katika visiwa hivyo vya Fundo na Uvinje. Hawalalamiki kwa sababu ya kujengwa hoteli, lakini kinachowasikitisha ni kutokushirikishwa au

kushauriwa katika ujenzi huo. Sasa kwa bahati mbaya sana na ni jambo la ajabu ambalo sijawahi kulisikia ndani ya nchi hii zinajengwa hoteli mbili hizo kwa mtutu wa bunduki Mhe. Naibu Spika, Uvinje kuna askari 20 na Fundo kuna askari 20 wanaolinda ujenzi ule.

Sasa nashangaa sana ujenzi huo unasimamiwa kwa mtutu wa bunduki, mwenye hoteli hizo ni nani na katika kujengwa huko watu bila ya mashauriano. Kwa sababu ninavyofahamu mimi mahoteli yote yanatakiwa serikali ipate faida iingize mapato na wale wananchi wazawa au wakaazi wa eneo lile nao pia wafaidike. Lakini kwa bahati mbaya kabla hoteli hizi hazijamaliza kwenye ujenzi inaonesha hivyo sasa sijui picha hii baada ya kumalizika ujenzi huo mashirikiano yatatoka wapi baina ya wananchi wa visiwa hivi na watalii tuliowakusudia waje pale wawekeze, ili serikali ipate faida na wananchi wetu pia nao wapate faida.

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo la kusikitisha, ni jambo ambalo linatuumiza sasa hapa naomba kwanza nimuulize Mhe. Waziri hoteli zote zilizopo Zanzibar ni hoteli ipi miongoni mwa hizi zilizokuwepo Zanzibar zilizojengwa kwa utaratibu huu wa mtutu wa bunduki?

Ikiwa hakuna Unguja, au hata huko Pemba ziko nyingi zishajengwa anambie kama ipo hoteli iliyojengwa katika utaratibu huo wa mtutu wa bunduki, kama hakuna kwa nini watu wa Pemba katika visiwa viwili hivi wadhalilishwe katika hali kama hii?

Mhe. Naibu Spika, nina wasiwasi alilolitangaza Mhe. Rais la utalii kwa wote hakubaliani na ujenzi huu wa mtutu wa bunduki na mimi kama mwanamke ninayetoka Wilaya ya Wete naungana na wanawake wenzangu wa Wilaya ya Wete sikubaliani na ujenzi huu wa kusimamiwa kwa mtutu wa bunduki.

Jambo lolote lenye maslahi na nchi yetu linatakiwa lifanywe kwa busara, haiwezekani kwa nini, kuna kosa gani lililokuwa haiwezi kutumika busara katika visiwa viwili hivi ikafikia wakati kujengwa hoteli zile kwa mtutu wa bunduki. Je, watu wa visiwa hivi watakuwa na imani gani na serikali yao na watakuwa na imani gani ya kupata angalau na wao ajira pengine baadae katika mahoteli yale wakati ujenzi unakuja kwa mtutu wa bunduki.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwambia sitaki niseme sana lakini hili limeniuma sana kwa sababu ni jambo ambalo nalijua na nimeliona na ni wanawake wenzangu walionisikitikia katika hili. Namuomba Mhe. Waziri na serikali kwa jumla watumie busara na hekima lakini hili la kufanya hivi halileti picha nzuri kwa wananchi wetu. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi kidogo ya kuweza kuchangia ripot hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa sitaki kuchangia lakini nitakuwa sitawatendea haki wanamichezo wa Zanzibar kama sikuchangia ripoti hii. Ukija katika ripoti hii ambayo tumeletewa na nikianza katika ukurasa wa nne (4) ambao unazungumzia suala la *ZBC TV* ambapo kamati au mapendekezo ya kamati ilisema kwamba, ifikirie kuanzisha *channel* nyengine na majibu ya wizara imesema kwamba kipindi hiki *ZBC* imeanza kufanya majaribio ya *channel* mbili ambayo inaitwa *ZBC 2*.

Sasa mimi sijawahi kuiona hiyo *ZBC 2,* lakini nimeweza kufuatilia nikaambiwa kwamba *ZBC 2* ipo lakini huwa inaonekana katika *channel* ya *Azam TV* pekee.

Sasa suala langu ni dogo tu kwa Mhe. Waziri kwamba kwa sababu malengo au hoja ya Kamati ni kuonaWazanzibari wanaona vipindi mbali mbali kupitia hiyo *channel II*. Sasa nimuulize tu Mhe. Waziri pengine baadae aje atueleze tu kwamba au wizara au shirika limejipanga vipi kuhakikisha kwamba hiyo *channel II* basi inaendana na wakati na hali ya kibiashara katika *channel* nyengine au mashirika mengine.

Nikija katika suala zima hili la maagizo ya kamati kuhusiana na masuala mazima ya *ZFA* ambayo ndiyo yaliyonifanya mimi nisimame kuchangia suala hili. Mhe. Naibu Spika, kuna maelezo ambayo yameelezwa ya kuutaka uongozi wa Chama cha Mpira wa miguu Zanzibar kuendelea kufanya kazi kwa pamoja na wadau, majibu yake Mhe. Waziri anijibu au Wizara inijibu kwamba pamoja na kamati zote za mpira kama vile Kamati za Waamuzi na nyengine, lakini mimi naona bado naona kwamba ushirikiano au uwezeshaji bado ni finyu ndio hata ukaona

kwamba Mhe. Ali Salum aliyemalizia muda wake alisikitika sana kuona hali halisi ya mpira wetu wa miguu Zanzibar, tulikotoka na tunakokwenda.

Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana kwa kuzingatia kwamba Zanzibar ni visiwa ambavyo vilikuwa na vipaji mbali mbali na mifano mingi ipo tu Mhe. Naibu Spika, kuna wachezaji wengi walitoka Zanzibar kwenda kucheza hata nchi za kiarabu huko zikiwemo Dubai, Saudia, Qatar na nchi nyengine na hapo Dar es Salamu kwa timu mbali mbali ambao wachezaji wetu walitoka hapa kwenda kucheza vilabu mbali mbali na ilikuwa inaleta sifa kubwa sana. Hivi majuzi Mhe. Waziri aliwahi kunijibu hapa kwamba vipaji vipo na sikatai kwamba vipaji vipo, lakini ule uendelezaji wenyewe kutokana na hali halisi ya uongozi wenyewe uliopo na wizara yenyewe sasa kuona kwamba labda kama mtoto yatima vile, unamwacha anafanya anavyotaka.

Sasa hapa kwa kweli mimi naona kwamba bado wizara haijawa makini katika kulisimamia na kuendeleza mchezo hususan katika mchezo huu wa mpira wa miguu.

Mhe. Naibu Spika, hata wewe unafahamu kwamba *ZFA* imejawa na migogoro takriban miaka mitano iliyopita. Hakutambulikani mpira unachezwa Zanzibar hakutambulikani wachezaji gani, hakutambulikani muendelezo gani katika masuala mazima ya kuinua soka la Zanzibar. Sasa mimi Mhe. Waziri ningependa tu aje atueleze hasa tatizo ni nini. Kwa sababu uchanguzi wa *ZFA* ulikuwa ufanyike Disemba lakini kutokana na mgogoro huu uliotokea hadi leo bado uchaguzi haujafanywa.

*ZFA* baada ya kujiongezea muda ya uongozi wao ambao umesema kwamba unao uwezo wa kufikia uongozi wao mwezi Aprili, lakini huko nyuma vyama vya Wilaya vimefanya uchaguzi na tayari vyama vya Wilaya vimeshapata viongozi wake. Sasa mgogoro huu Mhe. Naibu Spika, umetokana na viongozi wenyewe wa *ZFA* wanalana wao kwa wao. Sasa hili ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba wizara, Baraza kwa jumla kuona hadi leo mimi nasikitika sana...

**UTARATIBU**

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Naibu spika, kanuni kifungu cha 59 (4) ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kusema jambo lolote ambalo linangojea uamuzi wa Mahakama. *ZFA* iko Mahakamani na mambo ambayo wameshitakiwa na Jaji anayashughulikia ni matatu.

(1) Katiba ya *ZFA*.
(2) Uchaguzi wa *ZFA.*
(3) Ubadhirifu na *Auditing* ya Fedha.

Sasa utaratibu ambao nakusudia kusema ni kwamba ikiwa Mjumbe atalizungumzia suala la uchaguzi na suala la Katiba ya *ZFA* itabidi na mimi nilijibu jambo ambalo nahofu kwamba kinyume kwanza na kanuni na linaweza ku-*influence* kesi iliyoko Mahakamani.

Kwa hivyo, ningeshauri sana Mhe. Naibu Spika, kiti chako kitilie mkazo kanuni hii ili tumuache Jaji anayehusika na kesi hii awe na uhuru wa kushughulikia shauri hili. Nakushukuru sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa mchagiaji jambo liko Mahakamani halizungumzwi Barazani tungoje hukumu ya Mahakama. Kwa hiyo, kuna nafasi pana ya kuzungumza mengine nakuruhusu uendelee lakini la *ZFA* uliache.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, lakini katika maongezi yangu mimi sijazungumzia suala la Mahakama ingawa Mhe. Waziri amesema kwamba suala hili liko Mahakamani na mimi nakubali kwamba suala la uchaguzi liko Mahakamani, lakini kile kitu ambacho nilikuwa nakizungumzia ni sababu ambazo wizara wenyewe imehusika ndivyo ambavyo nilikuwa nazungumzia mimi.

Sasa yeye kama hataki tuzungumzie nadhani hapa ujumbe umeshafika na wananchi wapenda mpira wa miguu Zanzibar wemejua tatizo liko wapi. Tatizo liko kwa wizara yenyewe ambapo leo tumefikia hapa tulipofika. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika Chuo cha Uandishi wa Habari. Mhe. Naibu Spika, suala hili nataka majibu yake hapa Mhe. Waziri au majibu ya serikali nimesema kwamba niliko serikalini na maelezo kwamba Chuo cha Habari kimeazimwa na *FAWE,* hivyo kitakuwa vigumu *FAWE* kuhamishwa katika jitihada za kupatiwa chuo hicho eneo ili liwe na nafasi kutoka chuo kimepatiwa eneo jengine lililokuwa *Kilimani Bar*.

Sasa na ikiendelea hapa inasema kwamba ili kuhamia huko serikali imetoa fedha kwa ujenzi wa Chuo huko Kilimani na inandelea ambapo chuo kitahamia baada ya awamu ya kwanza ya ujenzi kukamilika.

Mhe. Naibu Spika, elimu kwa waandishi wa habari ni muhimu sana na mimi niipongeze serikali katika uamuzi huu na hasa kuhamisha chuo hichi na kukipeleka pale Kilimani. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua tu kwamba mipango hii au dhamira hii kuhakikisha kwamba chuo kile kinafanyika pale au kinajengwa pale kitachukua muda gani na lini hasa kitaanza. Kwa sababu hili ni jambo muhimu na niipongeze sana wizara pamoja na serikali kwa ujumla, lakini ni bidii na juhudi kubwa ambazo ningeiomba wizara kuhakikisha kwamba masuala haya yanakamilika kwa haraka ili waandishi wetu wa habari wapate elimu ya uhakika.

Kwa sababu katika ripoti hii pia imeeleza kwamba waandishi wa habari wengine wamekuwa wakisoma pia katika taarifa zao za habari kugusia katika sehemu mbali mbali, lakini watakaopata elimu ya kutosha na nadhani kwamba matatizo haya yataondoka na kuweza kushindana kibiashara na *TV* nyengine za ndani na za nje.

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa huo wa 10 Kamisheni ya Utalii. Mhe. Naibu Spika, kamati hapa iligusia suala la ulinzi kwa watalii ambao wanakuja katika nchi yetu. Kweli niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi katika kuimarisha ulinzi kwa kutumia Vikosi vyetu vya JKU, lakini Zanzibar tunategemea sana kupata pato kupitia sekta hii ya utalii na tujifunze katika nchi mbali mbali matatizo yametokea katika masuala haya ya ulinzi. Imewagharimu kupoteza mapato kwa nchi zao.

Zanzibar tulikuwa tunategemea kuingiza mapato kwa zao la karafuu, lakini sasa tunategemea utalii. Mimi nadhani tungeweza kuongeza bidii zaidi kuongeza nguvu zetu za ulinzi kwa watalii ambao wanakuja Zanzibar hususan katika sehemu za fukwe.

Mhe. Naibu Spika, tuombe Mwenyezi Mungu yasitokee yaliyotokea yametokea masuala mabaya sana kwa watalii ambao walifika katika nchi yetu. Niiombe sana wizara na nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja atueleze basi hasa mikakati gani zaidi kuhakikisha kwamba sekta ya utalii au watalii wetu wanapokuja nchini wanapata ulinzi wa uhakika na kuweza kuliongezea pato Taifa letu au nchi yetu.

Baada ya kusema haya Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, sheria zetu za kiislamu Mtume (*SAW*) anasema unapoliona ovu tumia mdomo wako au tumia mkono wako na ya tatu ulichukie ndani ya nafsi yako au ulikimbie.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikavuta pumzi zake ambazo ameniazima sijui saa ngapi atazihitaji. Wakati gani, dakika gani, mwezi gani, mwaka gani.

Vile vile, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa kamati hii kwa umakini wake wa hali ya juu aliouonesha katika kamati hii ikiwa pamoja na Wajumbe wake wote na watendaji wake na Makatibu wake.

Mhe. Naibu Spika, katika kitu kilichonisikitisha nitachukua kama dakika tano au kumi lakini jambo dogo ujenzi wa soko la Malindi. Hii ni aibu, karaha, haisemeki.

Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa Soko la Malindi ambao ukimalizika utakuwa umegharimu kiasi cha kiasi bilioni kumi na tano kwa sasa umesimama na kusimama kwa ujenzi huo ni *UNESCO* kushindwa kutoa kibali cha ujenzi wa soko hili kwa madai kwamba mchoro wa jengo hilo hauendani na majengo ya Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Spika, hii leo mtu keshatufadhili, lakini kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru Balozi wa Japan kwa msaada waliotoa *JICA* kama bilioni kumi na tano hebu tuangalie lile soko la samaki Malindi pale. Leo *UNESCO* sijui ndio nani au mdudu gani yuko kwake anakuja kutupangia maisha huku, tuangalie soko la samaki liko vipi,

mangapi hapa yamefuata *UNESCO*. Hatuwezi kufanya kazi kwa mazingira kama haya tumepata mfadhili atusaidie, leo riziki imekuja tunaipiga teke kwa sababu ya *UNESCO* katusaidia nini *UNESCO* katika mji huu.

Majumba leo yanaanguka katusaidia sisi kuezeka, watu wanafunikwa na vifusi tuishukuru hii Afisi ya Mhe. Haji Omar Kheri ndio inafanya kazi leo majumba yanaanguka ovyo *UNESCO* katusaidia nini. Mimi nije kuambiwa hasa faida iliyopatikana *UNESCO* mji huu yeye yuko kwake havujiwi, tuangalie wale wavuvi wanaburuza tu, uchafu mtupu hatuwezi kwenda kwa sababu hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa hili mimi nafikiri Wajumbe tutafute njia tumuone Mhe. Rais kwa suala hili bilioni kumi na tano tumesaidiwa kujenga soko, sababu gani za msingi kutuzuia *UNESCO*. Haielekei kitu kama hichi mtu yuko kwake watu wanaaibika, sisi maji hatuna, umeme wenyewe wa tabu faida gani tuliyopata *UNESCO* kwa kuwa ni mji, Muscat kajitoa ilipofikia hali kama hiyo akataka kuchimba mafuta yake, hii si kitu cha kuelekea lazima tuambizane ukweli faida gani tumeipata sisi, itwambie serikali Mji Mkongwe kuja watalii, majumba mabovu tunataka mji mpya sasa hatutaki kuwa na Mji Mkongwe tushafika pahali hatuwezi kwenda. Kitu cha kusikitisha soko la bilioni kumi na tano nani atatoa. Hili bwana tutakesha tutafute njia kwa hili!

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nije Afisi ya Magazeti ya Zanzibar Leo. Afisi bwana hairidhishi *Air condition* haina, ina dirisha moja tu jengo halikidhi waandishi wa habari ndio wanaotangaza habari zetu. Hawa ndio zikaonekana, bila ya wao hatuwezi kwenda, hatuwatendei haki, feni moja linafanya kazi mtafikiri Hospitali ya Mnazi Mmoja kitengo cha Sukari kuna feni sita moja tu ndio linafanya kazi.

Jengine niendelee kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umakini wake kwa wananchi wake jinsi anavyowajali aliagiza wizara nne kwenye soko la Mwani sijui kama wamekaa mpaka leo Wizara ya Biashara, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Wizara ya Wanawake na Watoto.

Leo wananchi mwani shilingi mia tano mateso wanayopata, mbona karafuu wananchi wakulima wanasaidiwa kupelekewa majamvi, kandili, karabai kukopeshwa kwa nini wananchi wa mwani hawataki kushughulikia suala la mwani, kwa nini haiwezekani, wananchi ndio hawa hawa serikali hii isingekuwepo hizi kazi tunazofanya sisi tunatumwa na wananchi, huyu bosi wetu ni mwananchi.

Mmeagizwa nyinyi wizara nne zikae zitafute suala la mwani. Leo kilio cha mwani mpaka leo kimefika wapi, mwani shilingi mia tano wananchi wanateseka, kwa nini hamtaki kuuthamini huu mwani serikali. Mfike pahali muwajali wananchi nguvu zao, watu wanaumia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapo nije na kuwatetea hawa waandishi wetu wa habari wa humu ndani maslahi yao ya muda mrefu. Hebu tuangalie hizi kazi wanazozifanya humu ndani maslahi yakoje kila mwaka tunapiga kelele na hili hasa si lako Mhe. Ali Said Mbarouk, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ibebe dhamana hii. Kila siku wananchi hawa wanafanya kazi katika mazingira tuwafikiri watu maslahi yao, baridi iliyokuwepo ndani na kazi zile wanazozifanya. Waandishi wa habari ni watu kutunzwa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije suala la viwanja vyetu vya mazoezi Mnazi Mmoja. Kweli Serikali haioni uchafu uliokuwepo pale. Viwanja vimefunikwa na maji miaka na miaka, karne na karne tunayokwenda nayo, mpira utachezwa kweli Zanzibar. Kweli suala kama lile, Serikali ilipotaka lake mbona imenunua meli, mazoezi yatafanywa vipi hapa. Tufike pahali tujali kiwanja cha mpira. Viwanja Mwenyezi Mungu katupa neema vipo pale pamoja, tunashindwa kukarabati maji yale, kuyaondosha maji yale.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo ninafikiri hapo na nimalizie kwa hapo na sitounga mkono hoja hii kama sijapata ufumbuzi wa kutosha wa soko la samaki, kwa sababu Mhe. Waziri anajua. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Sasa nafasi tunampa Mhe. Salim Abdalla Hamad na muda ukibakia tutampa Mhe. Hassan Hamad Omar.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Naibu Spika, na mimi ninashukuru kwa kupata nafasi ya kueleza machache maagizo ya kamati na utekelezaji wa wizara mbili; Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa kwa ruhusa yako naomba kuzungumzia machache kuhusu Wizara ya Mifugo na Uvivu kutokana na maagizo ya kamati na utekekelezaji kwa baadhi ya vifungu kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, tukifungua ukurasa wa nne katika karatasi ya wizara hii kuna agizo la kwanza ambalo agizo hili linatokana na maelekezo kuwa wizara ifanye marekebisho ya Sheria ya Mifugo ili iweze kuwadhibiti wafugaji wakaidi ambao wanakwepa kuipeleka mifugo yao katika chanjo ya kujikinga na maradhi ya wanyama.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa maelekezo ya utekelezaji ni kuwa sheria hii ambayo ni Sheria ya Raslimali ya Mifugo Na.11 ya 1999. Hivi sasa imo katika hatua za mwisho ya kufanyiwa marekebisho baada ya kupita kwa wadau na watendaji wa sekta ya mifugo, na hivi sasa sheria hiyo ipo kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria na kufanyiwa marekebisho ya mwisho kabla ya kuwasilishwa katika ngazi ya juu za maamuzi na hatimaye Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuzungumza kuwa wanyama hawa ni viumbe na wakati ni viumbe wanahitaji kupatiwa chanjo za kujikinga na maradhi. Kama hawakupatiwa chanjo hizi kuna hatari ya wanyama hawa kupata maradhi yenyewe na kwa yale maradhi ya kuambikiza wakaambukiza wanyama wengine. Kwa hivyo, urekebishwaji wa Sheria hii ya Raslimali ya Mifugo Na. 11 ya 1999 ni muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini kutokana na umuhimu wake mpaka leo sheria hiyo bado haijafika kwetu. Ina maana na hali inaendelea hivyo hivyo. Hapa naomba kupewa maelezo katika masuala mawili.

Moja, huu kwa hawa wafugaji unatokana na kitu gani. Kwa sababu mfugaji anataka mifugo yake iendelee iwe mizima afya nzuri izae na kadhalika apate faida. Ikiwa kuna ukaidi, ukaidi huu unatokea na sababu gani. Pengine je, si kwa sababu ya chanjo tu, wakati ile hali wafugaji hawa hawana pesa za kulipia ndiyo ukaidi huu ukaja huku bila ya sababu yoyote. Naomba nielezwe.

La pili, tokea kuanza kufanywa marekebisho kwa hatua ya kwanza ya sheria hii mpaka leo ni muda gani na tunatarajia lini sheria hii itamaliza kupita ngazi zinazohusika na kufika Baraza la Wawakilishi kwa kujadiliwa na kupitishwa kwa faida ya wafugaji wetu wote.

Mhe. Naibu Spika, halafu kuna maelezo hapa ya agizo la pili kwenye wizara hii hii ambalo linahusiana na eneo la mradi wa kupandisha ng'ombe wa sindano Marubuhi. Kwa mujibu wa maelezo ya agizo ni kuwa hili eneo ni la karantini na kuna watu wengine wanalitumia kinyume na inavyotakiwa.

Kesi zilikwenda kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ninashukuru kwa juhudi yake ya kutoa maagizo ya kupatiwa sehemu nyengine, na sehemu imepatikana lakini waliopewa wamekataa kuitumia. Hapa naomba nipewe maelezo. Hili eneo ni marufuku kwa kutumia kwa mambo mengine kama yepi, maana hayakuelezwa hapa ambayo mambo hayo yanahatarisha afya za madume hawa na kusababisha utoaji wa mbegu chache. Ni kazi gani nyengine wanazozifanya hawa ambazo hazitakiwi katika eneo ambalo limepigwa karantini.

La pili, ni kuwa kwa sababu eneo limepigwa karantini, limepigwa ili kuona kuwa mifugo ile iliopo ambayo inatupatia mbegu inaimarika na kunawirika, haipati matatizo yoyote na inatoa mbegu kwa mujibu inavyohitajika. Sasa ikiwa kule walipopewa hawakutaka na kama kweli wanarudi pale pale, hatuoni kuwa hivi ni kurudisha nyuma maendeleo ya mifugo.

Mimi ninavyojua haya madume yamenunuliwa kwa gharama kubwa sana na kama haikuchukuliwa hadhari ya kitaalamu kama ilivyoelekezwa, kuna hatari ya kupata hasara kubwa huko tunakokwenda na hii azma ya kunyanyua mifugo yetu ikapotea. Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, kupata maelezo. Kama kule hawakuridhika na wamerudi, kuna hatua gani wakati hapa ndipo pameshapigwa marufuku ili haya ambayo yalikuwa yatokezee yasiweze kutokeza.

Mhe. Naibu Spika, tukija katika agizo la tatu. Hili linahusian na taaluma ya vikundi mbali mbali vya wafugaji, kuhusiana na elimu ya ushirika, biashara na ufugaji. Hapa kutokana na maelezo ya kamati ni kuwa kamati imeiagiza wizara kuvipatia taaluma zaidi vikundi mbali mbali vya wafugaji kuhusiana na elimu ya ushirika na biashara na ufugaji.

Mhe. Naibu Spika, ukiachia mbali ushirika na biashara, mimi hapa naomba kupata maelezo kwa sababu katika kujibu Wizara imesema kuwa, "Idara inaendelea na kuwaelimisha wafugaji kuhusu utaalamu wa ufugaji wa kisasa", na wakaeleza waliokwisha kupatiwa mafunzo kwa Unguja na Pemba.

Nini tukisema ufugaji wa kisasa. Huu ufugaji unataka taaluma kubwa na kama siyo taalamu kama muasisi, kwa semina tu na warsha ndogo ndogo, maisha huwezi ukawa na uwezo na ujuzi unaohitajika katika kukabili ufugaji huu. Ufugaji wa kisasa unategemea kupata machotara mapya ni ya kitaalamu kweli kweli. Kwa hivyo mimi ningeliomba kujua, hii kuhusu ufugaji wa kisasa ambao unatolewa kwa semina tu watu waweze kuendelea. Ni upi ambao ni wa kitaalamu kweli kweli na hasa ukiangalia kuwa ufugaji katika nchi hii wa ng'ombe na wanyama wengine wamechukua muda mrefu sana na huko nyuma tumekuwa tumefeli na hivi tunajiendeleza, lakini bado hatujafika katika kiwango kinachohitajika, hii kutizama ni bado kitaaluma tupo nyuma. Hivyo naomba taaluma hiyo ya semina kwa mambo haya ya kitaalamu itasaidia vipi wafugaji wetu ili lengo lifanikiwe.

Mhe. Naibu Spika, tukija katika Wizara hiyo hiyo ya Mifugo na Uvivu, kuna agizo la tano. Agizo hili lipo kwenye ukurasa wa sita. Agizo la kamati linasema kuwa Wizara imfikirie mfugaji Ame Khamis Ame wa Kambi kwa kusaidia kufikisha umeme katika sehemu yake ya mifugo.

Mfugaji huyu Bwana Ame Khamis Ame ni mfugaji mkubwa sana tu, anafuga mifugo ya aina nyingi, kuku, mabata, mabata mzinga na kadhalika na anao wengi. Na tunajua umuhimu wa umeme katika mifugo. Tokea uzalishaji na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Huyu kaomba kufikishiwa umeme kwa sababu aweze kufanikiwa katika suala zima la ufugaji ili aweze kujikomboa kiuchumi na vile vile kufikiria jamii kupata haja zinazohitajika. Hivyo umeme huu ni gharama gani mpaka Wizara baada ya kupokea suala hili mpaka leo wameshindwa kupeleka eti bajeti ni finyu. Na wanasema wana tamaa ya kufanya hivyo katika bajeti inayofuata ya 2014/2015 na wakati ni kawaida yetu, bajeti zetu kuwa finyu kutokana na hali yetu ya kifedha ilivyo. Kwa hivyo ana uhakika gani kama atapata tena finyu kwa kipindi hichi kinachofuata karibuni ataweza kumsaidia Bwana Ame huyu ili asije akaathirika kwa kukosa umeme katika mifugo yake.

Mhe. Naibu Spika, tukiendelea na Wizara hii lipo agizo la sita na lipo kwenye ukurasa wa sita, kuna jengo lile ambalo kamati imeomba likamilishwe. Kumbe jengo lishajengwa kwa matofali na limeshaezekwa lakini sasa anatafutwa mzabuni wa kukamilish sehemu iliyobakia. Naomba maelezo aliyejenga ni nani na sasa ikabidi kutafutwa mzabuni mwengine.

Hiyo ni (a). Kuhusu (b) mpaka sasa hivi jengo hili limeshatumia kiasi gani ya fedha na linatarajia kutumia fedha kiasi gani. Na (c) linatarajiwa kupatikana wakati gani.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuna hati miliki na hii ni agizo la nane la kamati kwa wizara hii. Agizo limeeleza kuwa kwa kuwa Wizara haina hati miliki katika shamba la mifugo la Pangeni ingawa linalimiliki kwa muda mrefu sasa, kamati inaiagiza wizara kutafutiwa hati hiyo haraka ili kuepusha uvamizi wa eneo hilo unaoendelea.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya utekelezaji ni kuwa hili shamba lilipimwa au lilikwisha kupimwa miaka hamsini iliyopita ambayo baadhi yetu humu hatujafika na kuwa shamba hili waliohusika walikwishakulipwa tokea mwaka 1959. Kwa hivyo, watu wamekwishakulipwa na shamba limekwishakupimwa na *beacons* zilikwishakuekwa. Ni sababu zipi za msingi hasa kwa Wizara inayohusika na kutoa hati miliki mpaka miaka yote hiyo ikawa bado shamba hili halijapata hatimiliki, kiasi ambacho watu wanalivamia na *beacons* zinaondolewa, hali ambayo hairidhishi. Ni sababu zipi hasa muda wote huo, tokea mwaka 1959 ambapo watu baada ya kulipwa mpaka leo ikawa hati miliki hiyo haijapatikana. Naomba maelezo.

Mhe. Naibu Spika, kuna agizo hapa la kwanza kwenye ukurasa wa nne ambayo sasa hii ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi, aah! hii nimeshamaliza. Kuna agizo hapa Mhe. Naibu Spika, la tano ukurasa wa tisa ambalo agizo hili linaeleza kuwa linahusiana na ufugaji wa samaki katika maziwa; yaani maji baridi.

Agizo hili ambalo lipo kwenye ukurasa wa tisa lina maelezo marefu tu, tena maelezo makubwa tu lakini sitaki nirejee kutokana na kuwa limeshaelezwa. Mimi ningeomba kujua tu tulihamasisha hapa wananchi kujiingiza katika ufugaji wa samaki na kuna mabwawa mengi tu ya samaki wa maji chumvi. Mabwawa yale yalianza kufuatiliwa vizuri hasa hii Wizara ilipoanza na ilipokuwa mpya. Ninampongeza Mhe. Said Ali Mbarouk kwa hayo na

tulishuhudia kazi ngumu ya watu waliokuwa wakiifanya ili kujikwamua kiuchumi na tuliona kuwa kuna ulazima wa wafugaji hawa lazima wasaidiwe ndiyo wataweza kufanya hii kazi.

Imepotea moja kwa moja, watu hawashughulikiwi tena na miradi mingi imekufa kabis kabisa kama Mhe. Farida Amour Mohammed alivyoeleza. Hivi sasa tunaingia katika ufugaji wa maji baridi. Ni sababu zipi zilizotufanya tukashindwa katika ufugaji wa maji wa chumvi na wananchi walijitahidi sana kuitikia wito, ikawa sasa tunajiingiza katika maji baridi. Kwa nini kule tulifeli na vipi huku tutaweza kufanikiwa, kwa sababu ninavyojua kwa mazingira ya Zanzibar mabwawa ni kidogo si kama katika ufugaji wa maji ya chumvi.

Halafu ninashukuru Wizara imechukua juhudi kubwa sana. Inatengeneza chakula hichi wa samaki wa maji baridi ambacho asilimia 30 ni uwanga au *starch*, asilimia 40 ni *protein*, asilimia 25 ni *vitamin* pamoja na ma-*iodine* mengine na asilimia 5 tu ndiyo mafuta. Hiki ni chakula cha jumla kwa aina ya samaki mbali mbali wanaofugwa katika maji baridi. Hivi kumbe viumbe vyengine wanahitaji *protein* zaidi kuliko *starch* tofauti na sisi wanadamu. Kwa hivyo, naomba utaalamu wa chakula hiki kinachotengenezwa, isije ikawa kinatengenezwa kwa samaki fulani lakini samaki fulani kwa vile ni tofauti kimaumbile ikawa chakula hichi hakimfai. Naomba maelezo ya kitaalamu ili niridhike.

Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi sasa nimalize Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Naibu Spika, nianze na agizo la kwanza na agizo hili lipo ukurasa wa tatu wa kabrasha hili tulilopewa. Agizo hili ni kuwa kamati; agizo la 1(a) inasema; "Ihakikishe inaweka majenereta ya uhakika katika studio za *ZBC* na kadhalika". Utekelezaji imeelezwa majenereta yaliyonunuliwa na moja lililotengenezwa, lakini yote ni katika Kisiwa hichi cha Unguja, wakati Pemba tuna *studio* kubwa tu na fahamu zangu ni kuwa jenereta iliopo ni mbovu *no economic*, hata kufanya kazi haifanyi ijapokuwa ni nzima kutokana na kuwa inatia hasara sana. Je, na kule kulifikiriwa kupelekwa jenereta nyengine, sina makubwa hapa.

Halafu jengine Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu kamati imeiomba Wizara kuongeza *channels*, na Wizara imeongeza *channel* moja ile inayoitwa *ZBC 2* na *channel* hii inapatikana katika king'amuzi cha Azam. Lakini siku moja niliiona hii *channel* haina tofauti na ile *channel* ya *Clouds*. Ni magoma, tena magoma yaliyokuwa hayastahamiliki na utamaduni wetu. Halafu hizo nyimbo zinazotiwa na hiyo michezo inayochezwa hazitazamiki kabisa.

Mimi swali langu kipindi kile nilikiona siku ile au ndiyo kinaendelea, ndiyo utamaduni wetu unavyokwenda wakati sisi tumetunga sheria juzi ya kulinda utamaduni wetu lakini ikiwa *ZBC 11* ndiyo vile vile, ni sawa sawa ni bora kama ingelikuwa haipo. Kama ndiyo vile ilivyo hivi sasa. Diamond, Davido, sijui nani hiyo sijui, hiyo ndiyo wala siyo utamaduni wetu wala haisaidii kitu. Kwa hivyo, kama kuna mengine *okay* lakini kama ni ile tu mimi mwenyewe naona bado tumeweka *channels,* lakini tumeharibu zaidi utamaduni zaidi wetu na tunalipeleka Taifa kule ambako siko.

Halafu Mhe.Naibu Spika, kwa kumaliza liko hili agizo nambari 1 (g) na lipo kwenye ukurasa wa tano. Kutokana na matatizo ya wenzetu wanaofanya kazi humu na wanahitaji kulipwa, kamati imetoa agizo kuwa kwa mujibu wa maelezo yaliomo humu ikutane na wahusika ikiwa ni Makatibu Wakuu; yaani Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi, (OR), Makamu wa Pili wa Rais na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ili hili suala kulipatia ufumbuzi.

Lakini majibu badala ya Makatibu waliagizwa na kamati, ni Mawaziri ndiyo waliokaa wa Wizara hizo husika. Naomba nielezwe ilikuwaje hawa Makatibu Wakuu, kamati kidogo ilitoa agizo siyo sahihi hawakuangalia mbali, haiwahusu mambo haya mpaka ikaonekana kwa katika utekelezaji wakutane Mawaziri wenyewe, wakati Mawaziri wanao watendaji wao wakuu walioainishwa na kamati.

Mhe. Naibu Spika, halafu hili suala mimi nataka niulize, hivyo ni fedha kiasi gani inayodaiwa hivi sasa, kwa sababu ni muda mrefu. Jengine ni sababu zipi zilizopelekea kuwaajiri watu kufanya kazi ikawa hawalipwi na baada ya mazungumzo ya hao Mawaziri kwa nini wakaliweka suala hili kuwa litajadiliwa katika kipindi cha fedha cha 2015/2016, kwa nini iwe hivyo. Kuna kitu gani kilichoweka kikwazo. Naomba kupata majibu hasa kwa sababu kama wanaohusika watapatiwa fedha ni hatua kubwa sana ya *ZBC* kuweza kufanya shughuli zake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuna agizo la nambari 10 (a) liliopo ukurasa wa kumi na nne la kabrasha la Wizara hii ambalo agizo hili linazungumzia sana kuhusu uongozi wa sasa wa *ZFA* uwe karibu zaidi ya uongozi wa *TFF* na kuhakikisha kwamba mgao Zanzibar unapatikana.

Lakini jibu liliopo ni kuwa juhudi mbali mbali zimechukuliwa na uongozi wa sasa wa *ZFA* kwa kufanya vikao mbali mbali kwa nia ya kuendeleza mchezo huu nchini.

Mhe. Naibu Spika, agizo ilikuwa siyo nia ya kuendeleza mchezo, agizo ilikuwa kuhusu mgao. Kwa hivyo mimi nahisi majibu siyo sahihi kutokana na suala lenyewe, suala linazungumzia mambo ya mgao kuwe na mashirikiano ya kuendeleza mpira. Naomba nipate maelezo zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea.

**Mhe Naibu Spika:** Mheshimiwa.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Nikae kitako.

**Mhe. Naibu Spika:** Eeh! Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa michango yenu, lakini pia kwa kunipa ushirikiano kumaliza ripoti iliyokwisha na sasa tumeanza nyengine na tukiajaliwa tutaendelea kesho. Tunao wachangiaji saba, sita tayari bado saba, na wengine wanaotaka wataendelea hiyo kesho kuleta majina baada ya maswali na majibu.

Baada ya hayo naahirisha kikao chetu hichi tukijaaliwa hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 24/03/2015, saa 3:00 barabara za asubuhi.

*(Saa 1:42 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24/03/2015 saa 3:00 asubuhi)*